# Nipashe

Jumatano Januari 1, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580116

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US







MENEJIMENTI NA WAFANYAKAZI WA THE GUARDIAN LIMITED WANAWATAKIWA WATANZANIA NA WASOMAJI WETU KWA UJUMLA HERI YA MWAKA MPYA 2020




## Mabalozi wamlilia mama wa mwandishi Erick Kabendera

UKURASA 3



# Kigwangalla amaliza mwaka kwa uchungu

- **JPM** amtaka kupatana na Katibu Mkuu wake, awapa siku 5 vinginevyo...*Uk.2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**TRC YALIPA MAMILIONI KISA KUKWAMA TRENI**

SHIRIKA la Reli nchini (TRC) limelipa zaidi ya Sh. milioni 10 kusafirisha abiria pamoja na watumishi 648...

UKURASA WA 5

**MAJALIWA AKATISHA LIKIZO ZA WATUMISHI**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza watendaji wote wa serikali walioko likizo warejee kazini mara...




DK. KIGWANGALA PROF. MKENDA

## Deni la Taifa lafikia tril. 54/-

UKURASA 3

# ACT - Wazalendo yaanika mbinu ya kuibwaga CCM

UK. 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO **KMC YAWATOA HOFU MASHABIKI** UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Kigwangalla amaliza mwaka kwa uchungu

**Na Mwandishi Wetu**

NI kumaliza mwaka kwa uchungu. Ndivyo ambavyo mtu anaweza kueleza kutokana na onyo la Rais John Magufuli alilolitoa kwa vigogo wa ngazi za juu wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Vigogo hao ni Waziri Dk. Hamisi Kigwangalla na Katibu Mkuu wake, Prof. Adolf Mkenda, ambao wametakiwa kuondoa tofauti zao vinginevyo atatengua uteuzi wao.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo jana, alipokuwa akizungumza na maofisa na askari wanyamapori na Hifadhi ya Misitu wa Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo, ambako alitembelea na kujionea vivutio vya utalii.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Gerson Msigwa, kwa vyombo vya habari jana, ilisema katika salamu zake, Rais Magufuli amelipongeza Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) kwa kazi nzuri ya uhifadhi, kukuza utalii na kuchangia mapato ya serikali.

Hata hivyo, taarifa hiyo ilisema Rais ameelezea kusikitishwa kwake na uhusiano mbaya uliopo kati ya Dk. Kigwangalla na Prof. Mkenda, hali inayosababisha baadhi ya shughuli za wizara kusuasua.

"Ninafahamu watendaji wenu wa juu, Katibu Mkuu na Waziri kila siku wanagombana, na ninawatazama taratibu. Nilishampa kazi Katibu Mkuu Kiongozi awaite awaeleze, lakini wasipobadilika nitawaondoa.

"Hilo ni lazima nilizungumze kwa dhati, siwezi kuwa na watendaji wa kuteua mimi halafu kila siku wanagombana, kuna mambo mengi hayaendi. Katibu Mkuu hamheshimu waziri na waziri naye hataki kwendana na Katibu Mkuu. siwezi kuvumilia hilo.

Kwa hiyo nalizungumza hili siku ya leo tarehe 31 ya mwezi wa 12 (2019), kwamba wajirekebishe na ikiwezekana wajirekebishe ndani ya siku tano, wawe wanasalimiana, wanazungumza, mimi ninafahamu nina vyombo ninajua nani hafai zaidi," alisisitiza Rais Magufuli.

Pia Rais Magufuli aliiongezea muda Bodi ya Tanapa iliyomaliza muda wake chini ya Mwenyekiti Jenerali mstaafu George Waitara kutokana na kuridhishwa na kazi nzuri zilizofanywa na Tanapa chini ya uongozi wa bodi hiyo, ikiwamo kuunda Jeshi Usu la Askari Wanyamapori na Hifadhi ya Misitu, na ametaka Tanapa iendelee kupiga hatua kwa maslahi ya taifa.

Rais Magufuli alisema Tanzania yenye hifadhi za taifa 22, imetoa zaidi ya asilimia 32.5 ya eneo la ardhi yake kwa ajili ya hifadhi na kwamba imefanya hivyo kwa maslahi ya Watanzania na watu wote duniani wanaotembelea hifadhi hizo.

Alimpongeza Kamishna wa Uhifadhi wa Tanapa, Dk. Allan Kijazi na Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo, Kamishna Msaidizi

INAENDELEA UK. 8



Rais John Magufuli akiwa na familia ya watalii kutoka Ufaransa ya Arnaud de Vanssay aliokutana nao wakati akitembelea Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo jana. **PICHA: IKULU**

# ACT-Wazalendo yaanika mbinu ya kuibwaga CCM

**Na Salome Kitomari**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kuwa kitakuwa mstari wa mbele kutengeneza umoja imara utakaokiondoa Chama Cha Mapinduzi madarakani kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Aidha, ili kufanikisha hilo chama hicho kimevitaka vyama vya upinzani kuweka kando tofauti zao na kuangalia maslahi yanayowaunganisha ya kuing'oa CCM madarakani.

Kauli hiyo ilitolewa jana kwa nyakati tofauti na Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe na Mshauri Mkuu wa chama hicho, Maalim Seif Sharif Hamad, wakati wakihutubia taifa kupitia vyombo vya habari.

Maalim Seif alisema ACT -Wazalendo inautangaza mwaka 2020 kuwa ni mwaka wa kuing'oa CCM na kwamba wataongoza juhudi za kuhakikisha kwa kuunda umoja wa dhati utakaovishirikisha vyama vyote vya siasa, asasi za kiraia, vyama vya kitaaluma na makundi yote ya kijamii kujenga umoja utakaowaongoza Watanzania kufanikisha lengo.

"Nitoe wito kwa viongozi wezangu na vyama vyetu vya siasa, pamoja na changamoto kadhaa zilizopo miongoni mwetu na vyama vyetu bado maslahi yanayotuunganisha kwa madhumuni ya kuing'oa CCM ni makubwa zaidi kuliko tofauti zetu. Ni wakati wa kuziweka tofauti zetu pembeni ili kuwaunganisha Watanzania pamoja kuing'oa CCM 2020," alifafanua.

Kwa mujibu wa Maalim Seif, mwaka huu utakuwa ni mwaka ambao Watanzania wataandika historia ya kwenda kuyazika madhila na kujiletea mabadiliko mema yatakayobadilisha maisha yao.

"ACT-Wazalendo kama chama makini cha siasa tumejipanga kikamilifu kutekeleza wajibu wetu katika kuyafikia mabadiliko wanayoyataka Watanzania. Hivi sasa tumo katika maandalizi ya Ilani za uchaguzi za chama zitakazotumika kusaka ridhaa ya Watanzania na Wazanzibari kupitia Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2020," alieleza.

Alisema viongozi hao kwa pamoja watakuwa na ziara ya kusikiliza "Listening Tour" ambayo lengo lake ni kuwashirikisha wananchi katika maandalizi ya Ilani kwa kusikiliza maoni yao kuhusu maeneo wangependa kuyaona yanazingatiwa katika ilani hizo.

**ZITTO AUTAMANI URAIS**

Kwa upande wake Zitto, kwa mara nyingine alieleza matamanio yake ya kuwa Rais wa Tanzania iwapo atapata ridhaa hiyo, na kwamba angependa kushiriki kwa dhati kuleta mabadiliko wanayoyastahili Watanzania.

"Naumizwa sana na hali ngumu ya maisha kwa Watanzania, kwa sasa si suala la nani anakuwa mgombea urais bali nguvu ya pamoja ya wadau na watu wote wenye nia ya kuiondoa CCM madarakani waseme nani anafaa kupeperusha bendera ya umoja huo," alisema na kuongeza:

"Napenda sana kuwa Rais wa

INAENDELEA UK. 8

## Mafuriko yakosesha makazi familia 75

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

FAMILIA 75 katika eneo la Serengeti Halmashauri ya Mji wa Bunda, hazina mahali pa kuishi baada ya nyumba zao kukumbwa na mafuriko yaliyotokana na mvua zinazoendelea kunyesha wilayani hapa.

Sambamba na mafuriko hayo, kaya hizo zimekumbwa na maji yanayotoka kwenye mto ulioko jirani na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, alisema hayo jana kwenye kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, kilichofanyika katika ukumbi wa halmashauri hiyo mjini hapa.

Alisema tayari kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo, imewatembelea wakazi wa eneo hilo na kuwapa pole ikiwa ni pamoja na kuwapatia chakula cha msaada kilichotolewa na serikali.

Alisema kwa sasa waathirika hao wanaishi kwa majirani ambao nyumba zao hazikukumbwa na mafuriko hayo pamoja na kwa jamaa zao.

Hata hivyo, Bupilipili aliwataka wananchi wilayani hapa kutojenga nyumba zao katika maeneo ambayo ni hatarishi. Naye Diwani wa Kabarimu, Pastory Ncheye, alisema kata yake pia imekumbwa na changamoto hiyo. Ncheye alisema iwapo mvua zitaendelea kunyesha inawezekana yakatokea maafa makubwa katika kata hiyo, kwa kuwa maji yamekuwa yakiingia hadi kwenye nyumba za watu kutokana na ubovu wa miundombinu ya barabara.

Alisema maji yamekuwa yakipita hadi juu ya barabara kuu ya Mwanza-Musoma na hali hiyo inaweza kusababisha daraja lililoko katika eneo hilo kusombwa na maji na kuhatarisha maisha ya watu wanaopita katika barabara hiyo, wakiwamo wanaotumia vyombo vya moto, baiskeli au wanaotembea kwa miguu.

Kutokana na hali hiyo, diwani huyo aliomba serikali kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), kuchukua hatua za makusudi haraka ili kuiondoa changamoto hiyo kabla madhara hayajatokea.

## HABARI KITAIFA

# Mabalozi wamlilia mama wa mwandishi Kabendera

**Na Moshi Lusonzo**

BALOZI mbalimbali za nchini zimetuma salamu za rambirambi kutokana na kifo cha mama wa mwandishi wa habari za uchunguzi, Erick Kabendera, Verdiana Mjwahuzi, aliyefariki dunia jana.

Verdiana (81), alifikwa na umauti katika Hospitali ya Amana jijini Dar es Salaam usiku wa kuamkia jana wakati akipatiwa matibabu.

Ilielezwa kuwa mama huyo alipelekwa hospitalini Jumamosi, hali yake ilipobadilika alipokuwa nyumbani, kisha kufariki dunia wakati mtoto wake, Kabendera akiwa rumande akikabiliwa na mashtaka matatu, likiwamo la uhujumu uchumi.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, mabalozi wa Marekani, Uholanzi na Uingereza nchini, walisema wamehuzunishwa na kifo cha mama wa mwandishi huyo na kuiomba familia kuwa na uvumilivu katika kipindi hiki kigumu.

Ubalozi wa Marekani nchini uliandika: "Tunatoa rambirambi kwa Erick Kabendera na familia yake kwa kuondokewa na mama yao mpendwa Verdiana Mjwahuzi. Tunamwombea pumziko la amani."

Balozi wa Uholanzi nchini, Verheul Jeroen, aliandika katika ukurasa wake wa Twitter akitoa salamu zake kwa Kabendera, akieleza kuwa mwaka 2019 umekuwa mbaya kwa mwandishi wa habari huyo."Ubalozi wa Uholanzi umetuma salamu za mwaka mpya kwa mwandishi Eric Kabendera. Mwaka 2019 haukuwa mzuri kwako, tunatuma salamu za pole kwako na familia kwa ujumla kwa huzuni ya kuondokewa na mama yenu mpendwa Verdiana Mjwahuzi. Tunakutakia kila mafanikio kwa mwaka mpya 2020," Balozi Jeroen aliandika.

Balozi wa Uingereza nchini, Sarah Cooke, pia alisema amesikitishwa na taarifa za kifo cha Verdian, akisema: "Nimesikitishwa kusikia kifo cha Verdiana Mjwahuzi, mama wa Erick Kabendera. Nampa pole Kabendera na familia yake katika kipindi hiki kigumu."

Siku chache kabla kifo chake, Verdiana alimwomba Rais John Magufuli, amsamehe mtoto wake huyo, Kabendera, akieleza kuwa mwandishi huyo wa habari za uchunguzi ni nguzo muhimu ya ustawi wa familia yake.

"Mheshimiwa Rais na yeye ni mtoto kama walivyo watoto

INAENDELEA UK. 8



Rais wa Zanzibar ambaye ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Ali Mohamed Shein, akimkabidhi zawadi mwanafunzi bora wa kike ngazi ya Shahada ya Kwanza ya Jiografia na Taaluma ya Mazingira, Aisha Omar Makame. **PICHA: IKULU**

# Deni la Taifa lafika tril. 54/-

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amesema Deni la Taifa limeongezeka na kufika Sh. trilioni 54.84 Novemba 30, 2019 kutoka Sh. trilioni 49.08 Novemba 30, 2018.

Dk. Mpango aliyesema hayo alipowasilisha taarifa yake ya jana mbele ya waandishi wa habari jijini hapa kuhusu hali ya uchumi wa taifa mwaka 2019 na tathmini ya awali ya utekelezaji wa bajeti kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2019/2020.

Alisema kiwango hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 11.7, akibainisha kuwa katika deni hilo, Deni la Nje ni Sh. trilioni 40.39 na Deni la Ndani ni Sh. trilioni 14.44.

Alisema ongezeko la deni hilo linatokana na riba ya mikopo ambayo mikataba yake iliingiwa zamani na mikopo mipya yenye masharti nafuu na ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Waziri huyo alisema itaendelea kuhakikisha fedha zilizokopwa zinatumika kujenga rasilimali ambazo ni msingi wa kuongeza uwezo wa kuzalisha mali na kuendeleza taifa na uwezo wa kulipa mikopo hiyo.

Alibainisha kuwa mikopo hiyo ilitumika kugharamikia ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, ujenzi wa mitambo ya kufua umeme na utekelezaji wa miraji ya maji.

Mtaalamu huyo wa uchumi alisema matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanywa Desemba 2018, inaonyesha deni ni himilivu kwa muda mfupi, wa kati na mrefu kwa kuzingatia vigezo muhimu vinavyotumika kimataifa.

Alisema Tanzania bado ina uwezo wa kuendelea kukopa ndani na nje ya nchi ili kugharamia shughuli zake za maendeleo na kulipa mikopo inayoiva kwa kutumia mapato yake ya ndani na nje kwa wakati.

Waziri Mpango alibainisha kuwa mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya mamlaka ya serikali za mitaa katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2019, yalifikia Sh. trilioni 8.501, sawa na asilimia 94.4 ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 9.01 katika kipindi hicho.

Alisema mapato ya kodi yalikuwa Sh. trilioni 7.179, sawa na asilimia 95.5 ya makadirio ya kipindi hicho ya Sh. trilioni 7.514 .

Aliongeza kuwa mapato yasiyo ya kodi yalifika Sh. trilioni 1.013, ikiwa ni asilimia 86.5. ya lengo la makusanyo ya Sh. trilioni 1.17 yaliyokusudiwa.

Alisema makusanyo ya mapato kutoka taasisi za mashirika ya umma kwa mwaka 2018/2019, yalikuwa Sh. trilioni 1.053 kutoka katika taasisi na mashirika 79 kati ya mashirika 266 yaliyopo hadi kufikia siku ya kuwasilisha gawio kwa Rais John Magufuli Novemba 24, 2019.

Alisema mapato ya mamlaka ya serikali za mitaa ni Sh. bilioni 309.4 ikiwa ni asilimia 95 ya lengo la kukusanya Sh. bilioni 325.6.

Alibainisha kuwa Septemba 2019, mapato ya kodi yalivunja rekodi ya makusanyo tangu uhuru wa nchi, baada ya kukusanya Sh. trilioni 1.7.

Kuhusu tathmini ya Shilingi ya Tanzania, Dk. Mpango alisema imeendelea kuwa tulivu, akibainisha kuwa tangu Julai hadi Novemba 29, 2019, Dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa Sh. 2,291 ikilinganishwa na Sh. 2,276 katika kipindi kama hicho mwaka 2018.

# Mkurugenzi ataja mbinu za kudhibiti rushwa ya ngono

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Kampuni za Lusesa SLC na ZACH Traders Co. Ltd, Zacharia Mpopo, ameishauri serikali kutilia mkazo katika kudhibiti mitindo ya ovyo ya uvaaji kwa wanafunzi wa elimu juu, akiamini ni njia sahihi ya kudhibiti rushwa ya ngono iliyomea kwa wasomi wa vyuo vikuu.

Mpopo alipiga simu jana kwenye ofisi za Nipashe kueleza anachokifahamu kuhusu kadhia ya aina hiyo ya rushwa kuingia katika mustakabali wa elimu nchini, baada ya gazeti hili kuchapisha ripoti maalum kwa siku tatu mfululizo kueleza kwa kina namna rushwa hiyo inavyofanyika.

Katika ushuhuda wake, mkurugenzi huyo aliyedai anaishi karibu na Hosteli za Mabibo za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alidai amekuwa akiwaona mabinti wanaotoka na kuingia ndani ya hosteli hizo wakiwa na mavazi yasiyofaa.

"Ninawapongeza sana Nipashe kwa jinsi mlivyochambua suala hili. Hii mada ni nzuri sana, lakini nimeona hatua zinazochukuliwa na serikali zinamlenga hasa mhadhiri, huku chanzo chenyewe ambacho ni mabinti zetu walioko chuoni, kikiachwa.

"Mavazi wanayovaa wanafunzi wa kike wa vyuo vikuu ni hatari sana. Kama hatutaweka kanuni kali za kuyadhibiti, ni wazi kwamba rushwa hii itaendelea kuwapo vyuoni, mabinti zetu wanavaa nguo ambazo zinawaonyesha maungo yao kwa kila kitu.

"Hawa wahadhiri pamoja na kwamba kuna miiko ya kazi, lakini nao ni binadamu, wana udhaifu. Mwanafunzi anaingia chuoni akiwa na vazi linalochora maumbile yake yote. Hicho ni kishawishi kwa walimu na wanafunzi wenzake," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mbali na mavazi, anaamini uzembe wa baadhi ya wanafunzi katika kujisomea na kupenda kile alichokiita mambo makubwa ya kitajiri, vinasababisha wanafunzi kutumbukia kwenye vitendo vya aina hiyo ya rushwa.

"Mbaya zaidi, vijana wetu wa siku hizi wanataka mambo makubwa. Binti yuko chuo kikuu anashindwa kutambua hali ya familia yao, anataka simu ya gharama kubwa. Matokeo yake ni kuzama kwenye dhambi ya rushwa ya ngono," alisema.

Tanzania ina vyuo vikuu ambavyo tayari vimeweka udhibiti katika mavazi kwa wanafunzi na wafanyakazi wake, lakini hivi karibuni kuliripotiwa matukio ya baadhi ya wahadhiri wake kulalamikiwa kwa madai ya kuomba rushwa ya ngono kutoka kwa wanafunzi wao.

# TRC yalipa mamilioni kukwama treni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Reli nchini (TRC) limelipa zaidi ya Sh. milioni 10 kusafirisha abiria pamoja na watumishi 648, wa treni ya Delux waliokwama katika Stesheni ya Dodoma kutokana na mvua kubwa zilizonyesha na kusababisha reli kuchimbika.

Abiria hao waliokuwa wakitokea Kigoma kuelekea jijini Dar es Saalam walikwama toka juzi jioni jijini Dodoma kutokana na reli kujaa maji eneo la Zuzu na Kigwe mkoani hapa, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Akizungumza jijini hapa jana, Mkuu wa Kituo cha Dodoma, Rose Ngauga, alisema wameamua kuwasafirisha abiria hao ili kuepuka kukaa sana katika kituo wakati matengenezo yakiendelea katika maeneo ambayo tatizo hilo limetokea.

"Abiria wameanza kuondoka katika eneo la Dodoma wanaelekea katika sehemu ambazo walitakiwa kwenda, na kiasi cha fedha ambacho tumewalipa ni kama kurejeshea nauli zao ili wafike kule walikopanga," alisema Ngauga.

Akitoa ufafanuzi kuhusiana na tatizo hilo, Mhandisi Happiness Henry, alisema baada ya kugundua katika stesheni za Kigwe na Zuzu kuna maji yamejaa, waliamua kuzuia treni hiyo ya Delux ili kupisha marekebisho yanayofanywa na mafundi yakamilike.

"Kuna kilomita 361 na 364.7 maji yanafloo juu ya reli ambapo wataalamu wameenda kufanya marekebisho ili safari za kawaida ziendelee," alisema.

"Kilomita 482 .7 hadi 482.9 eneo la Kigwe, maji yamejaa na kuchimbua tuta la reli na eneo la Gulwe Godegode hatujui ni muda gani mvua ilivyonyesha imejaza mchanga juu ya reli," alisema mhandisi huyo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, aliwataka abiria hao kuwa na imani kwa shirika hilo kwa sababu linawajali wateja wake ndio maana amewatafutia usafiri mbadala ili wafike wanakokwenda.

"Naomba niwapongeze TRC jijini Dodoma, mmefanya mawasiliano vizuri kuhakikisha mnalinda usalama wa abiria kwa kuzuia treni hiyo kutokana na mvua zinazonyesha," alisema Katambi.

Alisema TRC inaendelea na ukarabati wa stesheni ambazo zimeleta tatizo kutokana na mvua zinazonyesha.

Mmoja wa abiria hao, Shabani Kiembe, aliipongeza serikali kutokana na kujali abiria wake baada ya kuona wamekwama na kuwatafutia mbadala wa usafiri ili kufika katika maeneo waliyopanga.



Kamishna wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Jaji mstaafu Harold Nsekela, akiangalia baadhi ya watumishi waliofika kurejesha fomu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwenyekiti halmashauri kortini tuhuma za uvamizi

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, Peter Maloda, pamoja na Ndekwamima Usukani wamepandishwa kizimbani kwa tuhuma za kuvamia shamba la Tungu Ntengwa.

Akiwasomea mashtaka yao, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Choma, Simon Malima, alisema tukio hilo lilitokea Desemba 16, mwaka jana saa 3:00 asubuhi katika Kijiji cha Choma.

Alisema washtakiwa Maloda ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Choma (CCM) na Usukani, walikutwa wakilima shamba la Ntengwa mkazi wa kijiji hicho.

Hakimu Malima alisema pia washtakiwa wote walitenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 299 sura ya 16 A Kanuni ya Adhabu iliyofanyiwa mapitio mwaka 2002 inayozuia kufanya makosa kama hayo.

Hata hivyo, baada ya washtakiwa hao kusomewa shtaka lao, walikana kutenda kosa hilo na kwamba hata kabla ya kuahirisha kesi, hakimu alitangaza kujitoa katika usikilizaji wake.

Kwa mujibu wa hakimu huyo, sababu zilizomfanya kujitoa ni kutokana na mmoja wa watuhumiwa kuwa ni jirani yake, hivyo anaweza kushindwa kutenda haki katika uamuzi.

Kutokana na uamuzi huo, alisema tayari ameshamwomba Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Igunga kupeleka hakimu mwingine wa kuisikiliza.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Januari 7, mwaka huu, itakapoanza kusikilizwa na hakimu mwingine atakayepangwa.

Washtakiwa wote wako nje kwa dhamana ya Sh. 500,000 kila mmoja na mdhamini mmoja.

# Wanakijiji wafanya tathmini walivyonufaishwa uwekezaji

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

WAKAZI wa Kijiji cha Magenge Wilaya na Mkoa wa Geita chenye utajiri wa dhahabu, wameukaribisha mwaka mpya kwa kufanya tathmini kupitia mkutano wa hadhara kuhusiana na walivyonufaika na uwapo wa wawekezaji kijijini hapo.

Aidha, waliwatahadharisha wasio tayari kuchangia kuwa watawanyima ushirikiano.

Mkutano huo uliotanguliwa na kikao cha ndani cha serikali ya kijiji hicho kwa kumtaja mwekezaji wa Kampuni ya Genge Tatu Ex-Tech kuwa mwekezaji mdogo mzawa wa mfano kwa kutumia zaidi ya Sh. milioni 20 kuchangia katika elimu na afya, hivyo kuwapunguzia mzigo wa kuchangia.

Miongoni mwa miradi inayodaiwa kuchangiwa na mwekezaji huyo ni ujenzi wa nyumba za walimu wa shule ya msingi ya kijiji hicho na ujenzi wa zahanati ya kijiji, hivyo kusaidia kupunguza changamoto zilizokuwapo katika sekta za elimu na afya kwa muda mrefu.

Mathias Masalu, mwenyekiti wa kijiji, amesema ni wajibu kwa wawekezaji katika maeneo waliyowekeza kumuiga mwekezaji huyo, Jumanne Yusuph Mtafuni kutokana na kusaidia jamii bila kusukumwa.

Wanakijjiji hao pia walimpongeza Rais John Magufuli kwa usimamizi wa raslimali tangu alipoingia madarakani kuhakikisha wananchi wanaufaika na uwapo wa rasilimali hizo mbali na serikali kunufaika kupitia kodi.

Magenge Chiza Joseph, Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, alisema manufaa yaliyopatikana ni makubwa kutokana na uwapo wa mwekezaji huyo.

Matafuni akizungumza na wananchi katika mkutano huo, aliwashukuru kutokana na kuutambua na kuuthamini mchango wake katika shughuli za kijamii, hivyo kuahidi kuendelea kuchangia huduma za jamii ikiwamo sekta ya maji.

Haya hivyo, aliwaomba wawekezaji wengine kuchangia ili kuisaidia serikali katika kuwasogezea huduma za kijamii wananchi.



Bajaj ikiwa imebeba mizigo juu na abiria ndani yake ikipita bila kujali sheria za usalama barabarani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa akatisha likizo za watumishi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza watendaji wote wa serikali walioko likizo warejee kazini mara moja ili kukamilisha miradi yote ya ujenzi wa miundombinu ya shule.

Amesema miradi hiyo inapaswa kukamilika mapema ili kuwezesha wanafunzi waliochaguliwa kuanza masomo ya kidato cha kwanza kutokukosa kwa sababu ya ukosefu wa miundombinu hiyo.

Majaliwa aliyasema hayo jana, alipofanya ziara kukagua ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani Ruangwa.

Alisema agizo alilolitoa kwa wakuu wa mikoa Desemba 29, mwaka jana, kuhusu usimamizi wa miundombinu ya shule ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, liko pale pale kwa sababu serikali haitaki kuona wanafunzi wakipishana katika kuanza masomo.

Miradi ambayo Waziri Mkuu aliitembelea ni ujenzi wa shule ya msingi ya Ng'au ambayo ipo katika hatua za mwisho kukamilika, ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (Veta), Hospitali ya Wilaya ya Ruangwa na Shule ya Sekondari ya Lucas Maria.

Waziri Mkuu alisema serikali inatoa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, hivyo ni lazima viongozi katika maeneo husika wahakikishe wanashirikiana katika kusimamia utekelezaji wake.

Alisema wanafunzi wanatakiwa kuanza masomo mwanzoni mwa mwezi huu, hivyo ni lazima usimamizi ukaongezwa katika baadhi ya maeneo ambayo miundombinu yake bado haijakamilika ili kuwahi masomo.

Akiwa katika Shule ya Sekondari ya Lucas Maria, Waziri Mkuu alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Andrea Chezue, ahakikishe mafundi wanafanya kazi usiku na mchana.

"Shule zinakaribia kufunguliwa na baadhi ya majengo kama bwalo, maabara na nyumba za walimu hayajakamilika, mafundi hawapo eneo la ujenzi na serikali imetoa fedha. Nataka kazi hii ikamilike mapema kwani hakuna sababu," alisema.

Wakati huo huo, wananchi wa Wilaya ya Ruangwa wamepongeza na kumshukuru Rais John Magufuli kutokana na miradi ya kimkakati inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Wananchi hao wakiwamo vijana wanaojenga Chuo cha Veta, walitoa pongezi na shukurani hizo mbele ya Waziri Mkuu baada ya kumaliza kukagua mradi wa ujenzi wa chuo hicho. Mafunzo yatakayotolewa chuoni hapo ni pamoja na ufundi uashi, seremala, magari, ushonaji nguo na Tehama.

Kadhalika, vijana hao wamewashauri vijana wenzao wajitokeze na kuchangamkia fursa za ajira zinazopatikana katika maeneo yao kupitia miradi mbalimbali inayotokelezwa na serikali ili waweze kujikwamua kiuchumi.

# Magereza yajipanga kuzalisha chakula kwa wafungwa

**Na Lucas Mboje,** DODOMA

JESHI la Magereza limejipanga kwa mwaka 2020 kuendelea na utekelezaji wa jukumu la uzalishaji wa chakula cha kutosha cha wafungwa kwa kutumia rasilimali zilizopo katika jeshi hilo ili kufikia azma ya serikali ya awamu ya tano ya kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa kwenye magereza.

Akizungumza na maofisa na askari wa jeshi hilo katika Baraza Maalumu la kufunga mwaka 2019 na kuukaribisha mwaka mpya jana jijini Dodoma, Kamishna Jenerali wa Magereza nchini, Phaustine Kasike, alisema jeshi hilo limejiwekea mkakati maalumu wa kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa kwenye magereza.

Katika kulifanyia kazi suala hilo, Kamishna Jenerali Kasike, alisema mavuno yameongezeka katika msimu wa kilimo 2018/2019, jeshi hilo limezalisha chakula cha wafungwa katika magereza 10 ya kimkakati (Songwe, Mollo, Ludewa, Arusha, Pawaga, Idete, Kitete, Isupilo, Kitai na Kitengule).

"Kupitia Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza (SHIMA), jeshi limelisha unga wa mahindi kwa wahalifu magerezani kwa kipindi cha mwaka mzima katika mikoa ya Lindi, Ruvuma, Mtwara, Rukwa, Njombe na Katavi. Vile vile, katika mikoa mingine shirika limelisha unga kwa miezi mitatu hadi sita," alisema Kamishna Jenerali Kasike.

INAENDELEA UK. 8



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Karibu Mwaka 2020

**LEO** tumeuanza Mwaka Mpya wa 2020. Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uzima, hivyo kuvuka mwaka 2019.

Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa wenzetu wengi hawakufanikiwa kuuvuka mwaka uliopita, kutokana na sababu mbalimbali kama ajali na magonjwa.

Mwaka jana ulikuwa na mafanikio na changamoto kadhaa. Kwa mfano baadhi ya majanga yaliathiri baadhi ya watu ikiwamo ajali ya lori la mafuta iliyoua zaidi ya watu 100 katika Manispaa ya Morogoro.

Aidha, mwaka jana mvua kubwa zilizonyesha kuanzia Septemba hadi jana ziliua watu kadhaa, wengine kukosa makazi na kuharibu mazao pamoja na miundombinu kama madaraja na barabara.

Mvua hizo kwa mujibu wa wataalamu, chanzo chake ni matokeo ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaendelea kusababisha athari maeneo mbalimbali duniani.

Hata hivyo, kuna mafanikio lukuki ambayo nchi yetu imeyapata kiuchumi, kijamii na kisiasa. Tulishuhudia uchumi wa taifa ukiendelea kukua, kuwa imara na kuwa tulivu. Mbali na athari za mvua, maeneo mengi ya nchi yalikuwa na chakula cha kutosha, hivyo kuwaepusha wananchi kuathiriwa na uhaba.

Kadhalika, tulishuhudia serikali ikiendeleza kasi ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, ikiwamo mikubwa. Itakumbukwa kuwa mwaka jana ndipo ulipozinduliwa ujenzi wa bwawa kubwa la kuzalisha umeme wa megawati 2,100 wilayani Rufiji Mkoa wa Pwani.

Mwaka huo huo tulishuhudia pia serikali ikizindua rada nne za kisasa kwa ajili ya usalama wa anga katika viwanja vya ndege kadhaa nchini sambamba na barabara za lami, miradi ya maji, vituo vya afya na hospitali katika mikoa kadhaa.

Vita dhidi ya rushwa iliendelea ambapo kesi kadhaa za watuhumiwa wa makosa makubwa zilifunguliwa mahakamani, huku wengine kukiri na kulipa faini kisha kuachiliwa.

Tanzania kwa mwaka jana iliendelea kung'ara kisiasa na kidiplomasia baada ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mwaka wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Sadc), ambapo Rais John Magufuli alishika nafasi ya uenyekiti kwa mwaka mmoja.

Vilevile, mwaka jana nchi yetu ilifanya uchaguzi wa serikali za mitaa, ambao uliwahusisha viongozi wa vijiji, mitaa na vitongoji walipatikana. Hata hivyo, kasoro iliyojitokeza na kuzua malalamiko mengi ni vyama vya upinzani kususia kwa madai ya kukiukwa kwa taratibu zilizosababisha wagombea wao wengi kuenguliwa.

Tunapouanza mwaka 2020, hatunabudi kujitafakari upya ili kuzika tofauti zilizojitokeza mwaka jana zinazikwa, ili nchi yetu iendelee kuwa na umoja, amani na mshikamano.

Tunasema hivyo kwa sababu mwaka 2020 utakuwa ni mwaka wa uchaguzi, ambapo vyama vya siasa vitakuwa vinashindanisha sera, ilani, mikakati na mipango kwa ajili ya kupata ridhaa ya wananchi.


Ili uchaguzi huo wa madiwani, wabunge na rais uwe huru na haki pamoja na kuendeleza umoja, amani na mshikamano wa kitaifa, mamlaka zinazohusika zihakikishe haki inatendeka kwa kila upande na mazingira ya ushindani yanakuwa sawa.

Wananchi kwa upande wao hawanabudi kutimiza wajibu kwa kuheshimu na kufuata sheria za nchi. Ni matarajio yetu kuwa kila mmoja akitimiza wajibu wake, uchaguzi wetu utakuwa mfano katika jumuiya ya kimataifa.

Suala lingine la msingi ni kila mmoja kwa nafasi yake kufanyakazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo binafsi na taifa kwa ujumla. Wote wanaostahili kulipakodi wahakikishe wanafanya hivyo kwa hiari ili kuiwezesha serikali kuongeza wigo wa mapato, na kutekeleza miradi ya maendeleo pamoja na huduma za msingi kwa wananchi wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Operesheni usafi mitaro nchini, wakati wake sasa

Na Raphael Kibiriti

**KUNA** mengi ambayo serikali ya awamu ya tano inazidi kujijengea uhalali kwenye suala zima la utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazokabili wananchi katika suala zima la kujenga ustawi na maendeleo ya jamii ya Kitanzania.

Ninaweza kuzungumzia maeneo mengi kuanzia kwenye suala zima la kupambana dhidi ya rushwa na ufisadi, watumishi hewa, uhalifu hususani unyang'anyi, ujambazi na ujangili.

Lakini hata katika suala la kuboresha hali ya miundombinu ya barabara, vituo vya afya, ukarabati na ujenzi wa madarasa, maabara, maktaba, utoaji wa elimu bure kwa kutaja baadhi ya mambo.

Muungwana anaona haya yote ni katika ile dhima ya kutekeleza majukumu na wajibu wa serikali hii kwa wananchi wake.

Na hiyo ni kwa mujibu wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo Rais na timu yake, waliinadi wakati wa kampeni za kutafuta ridhaa ya kuongoza taifa hili.

Kama nilivyosema hapo juu kuna mengi ambayo yametekelezwa na serikali hii, lakini kwa makusudi maalumu Muungwana amevutiwa zaidi kuzungumzia operesheni mbili ambazo kwa mtazamo wake zimeiongezea alama serikali ya awamu ya tano.

Zimeiongezea alama mbele ya macho ya wananchi na hasa wenye mapenzi mema kwa ustawi wa taifa na raia wake, lakini pia hata katika suala la usafi wa mazingira na uhai wa viumbe vinavyoyategemea mazingira hayo.

Operesheni ya kwanza anayoirejea Muungwana ni ile iliyochukuliwa na serikali mwaka 2017 inayofahamika hadi leo kama operesheni 'piga marufuku viroba' vilivyokuwa maarufu katika maeneo mbalimbali nchini.

Kupitia kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, serikali ilipiga marufuku uzalishaji, uuzaji, uingizaji na matumizi ya pombe inayofungwa kwenye pakiti za plastiki kwa jina la viroba kuanzia Machi Mosi, mwaka 2017.

Aidha, ikaweka wazi kwamba ambaye angebainika kuvitumia angewajibishwa kwa kulipa faini, kufungwa jela au vyote kwa pamoja.

Ilichukua hatua hiyo kwa nia nzuri ya kulinda afya ya Watanzania, hususani vijana ambao ndiyo nguvukazi ya taifa hili wanaotengeneza sehemu kubwa ya idadi ya Watanzania takribani milioni 55 kwa hivi sasa.

Kwa wanaokumbuka hali ilipokuwa imefikia wakati huo kiasi kwamba viroba vilienea kila kona hata kwa watoto wa shule za msingi ambao nao walianza kuvitumia kwa sababu ya urahisi wake wa kuvibeba, kwani iliwezekana hata kuviweka mfukoni na kutembea navyo.

Madhara ya viroba yalikuwa mabaya sana kwa afya na maendeleo ya Watanzania kwani mbali na ajali za barabarani zilizotokana na uendeshaji wa kizembe hasa kwa madereva wa bodaboda, pia yaliharibu mazingira kutokana na kuzagaa kwa vifungashio hivyo.

Operesheni ya pili ambayo imeendelea kuipa alama serikali hii ni iliyochukuliwa na serikali hivi karibuni ambayo imepiga marufuku uzalishaji, uingizaji, usafirishaji nje ya nchi, usambazaji, uuzaji na matumizi ya mifuko aina ya plastiki maarufu kama 'Rambo' iliyokuwa ikitumika kubebea bidhaa kuanzia Juni Mosi.

Katika operesheni zote mbili, serikali ilitoa maelekezo na hatua madhubuti itakazochukua kwa wote ambao wangekaidi maelekezo yake.

Kama nilivyosema hapo juu, kufanikiwa kwa operesheni hizi kunaonyesha kwamba serikali hii inapoelekeza marufuku dhidi ya dosari fulani iliyo na madhara kwa watu wake, wananchi wanaelewa na kutekeleza.

Wanafanya hivyo kwa sababu wanajua haina simile katika kuchukua hatua.

Wakati Muungwana akipongeza umadhubuti wa serikali katika kusimamia masuala yenye tija kwa wananchi, anatoa wito operesheni kama hiyo sasa ielekezwe katika usafi wa mitaro kwenye majiji na miji, hasa jiji la Dar es Salaam, lenye hali mbaya katika eneo hilo.

Muungwana ana imani kwamba serikali ikielekeza nguvu kwenye eneo hili la mitaro katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, suala la mlipuko wa magonjwa kama kipundupindu na homa ya Dengue iliyopo sasa yatakwisha.

# MJADALA & BARUA

## Watu wa aina hii wachukuliwe hatua kali

**Mhariri,**

*UKISOMA vitabu vya dini na hata kusikiliza mahubiri na mawaidha ya viongozi wetu wa dini ni dhahiri utapata jinsi ambavyo misahafu na maelekezo ya viongozi hao inavyosisitiza juu ya umuhimu wa kulinda uhai wa binadamu.*

*Inafafanuliwa kwamba uhai wa binadamu ni lazima ulindwe kwa kuwa ndivyo yalivyo maagizo ya Muumba na kwamba hata sheria, kanuni na taratibu mbalimbali katika jamii na makabila zinasisitiza juu ya hilo.*

*Ninaandika katika ukurasa huu kuelezea namna ninavyochukizwa na watu ambao hutupa watoto ovyo jalalani .Tatizo hili kimsingi liko sana kwa wasichana ambao matukio mengi yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara juu yao katika vyombo vya habari.*

*Ninawatahadharisha watu wanaofanya unyama huo wakumbuke kwamba Mwenyezi Mungu anawaona.*

*Ninaomba kwa serikali yetu tukufu iwachukulie hatua kali watu wa aina hii wasiothamini kabisa uhai wa binadamu.*

**John Ngosha- Mipa, Shinyanga**

## Kero hii ya kuvuta sigara hadharani ikomeshwe

**Mhariri,**

*NAOMBA unipatie nafasi kwenye gazeti letu linalotupatia fursa sisi wasomaji wake ya kueleza dukuduku na kero mbalimbali zinazotukabili katika jitihada za kuhakikisha kuwa tunapiga hatua kubwa za kimaendeleo kama watu binafsi na taifa kwa ujumla.*

*Kero niliyonayo kwa leo ni ile ya watu wanaovuta sigara kila mahali hata kwenye sehemu za wazi au za umma ambazo kimsingi haziruhusiwi kwa wavutaji kufanya starehe yao hiyo.*

*Tabia hii inakera katika mazingira yoyote kwa sababu inasumbua wengine wasio wavutaji wa sigara, hali inayowasababishia adha isiyokuwa na sababu, eti tu kwa baadhi ya watu kuendeleza starehe zao.*

*Ikumbukwe kuwa kwa mujibu wa utafiti toka vyanzo mbalimbali vya kiafya, inabainishwa kwamba moshi wa sigara unapomfikia mtu asiyevuta, humuathiri zaidi kiafya kuliko hata huyo mtumiaji mwenyewe.*


*Ninaomba mamlaka zinazohusika zisaidie kulimaliza tatizo hili sasa kwa kuchukua hatua za kuwakamata na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria wale wote wanaozidi kuvuta sigara sehemu za wazi ama za umma.*

**Lalida Bukuzu- Songea**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Taasisi zitoe elimu sahihi ya mpigakura, si vinginevyo




**Na Sabato Kasika**

**WAZIRI** Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, amezionya asasi za kiraia zilizopewa jukumu la kutoa elimu ya mpigakura kutokisemea chama chochote cha kisiasa.

Badala yake zinatakiwa kuelekeza wananchi umuhimu wa kujiandikisha, kupiga kura na kuwachagua viongozi wanaowataka na si kuwashawishi ili wampigie kiongozi, ambaye asasi hizo zinamtaka.

Anazitaka asasi hizo kuwaelekeza Watanzania kujua umuhimu wa kujiandikisha, kupigakura na kuwachagua viongozi wanaowataka wenyewe bila kuwapo kwa ushawishi wa aina yoyote.

Hivyo ndivyo alivyoagiza Waziri Mkuu wakati akizindua rasmi uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpigakura akiwa mkoani Kilimanjaro. Uboreshaji huo unakwenda sambamba na utoaji wa elimu hiyo, ambayo inatolewa na asasi 28 zilizopewa vibali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na kutangazwa Juni mwaka huu.

"Tume imetoa vibali vya kutoa elimu ya mpigakura kwa baadhi ya asasi za kiraia, rai yangu kwa asasi zilizopata vibali hivyo, kuendelea kutoa elimu hiyo kwa wananchi kwa kuzingatia mwongozo," anasema Majaliwa.

Anafafanua kuwa mwongozo umetolewa na NEC, hivyo asasi hizo zisikisemee chama chochote cha kisiasa, bali zielekeze wananchi umuhimu wa kujiandikisha, kupigakura na kuwachagua viongozi wanaowataka wenyewe na siyo kuwashawishi ili wampigie kiongozi ambaye asasi hizo zinamtaka.

Anasema, zikifanya hivyo zinakuwa zimejiepusha na ushabiki wa kisiasa na kufanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa na mwisho wa siku Watanzania watajitokeza kwa wingi kuchagua viongozi wanaowataka.

Anaamini kwamba wananchi wakipata elimu kuhusu uboreshaji wa daftari hilo, watahamasika kutumia haki yao ya katiba ya kujiandikisha na hatimaye kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Nikumbushe tu kwamba siku, ambayo asasi hizo zikikabidhiwa jukumu la kutoa elimu ya mpigakura, ziliagizwa kuzingatia mambo muhimu ili kufanikisha kazi hiyo, ikiwamo kufuata sheria, kanuni na taratibu na kutojihusisha na itikadi za kisiasa, udini, ukanda na ukabila.

Hadi sasa zinaendelea kuonywa kutojiingiza katika mijadala ya kisiasa na ushabiki na kutakiwa kufuata miongozo, ambayo zimepewa na NEC, lengo likiwa ni utoaji wa elimu kufanyika kwa ufanisi.

Hivyo kwa kauli ya Waziri Mkuu ambayo inaendelea kusisitiza kile ambacho NEC imekisema, basi wahusika wasikie na kuzingatia ili uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura ufanyike kama inavyotakiwa.

Asasi hizo zikienda kinyume na hayo, basi zijue kwamba zitakuwa zimechangia kuvuruga maana halisi ya elimu hiyo ya mpigakura inayokusudiwa kuwafikia wananchi.

Kushabikia vyama vya siasa katika utoaji wa elimu ya uraia ni sawa na kufanya kampeni, hivyo asasi zifanye kazi zake na kuwaachia wanasiasa kampeni zao wakati muafaka kufanya hivyo utakapotimia.

Watanzania na hasa vijana walioitimiza umri wa miaka 18 au wale ambao watatimiza umri huo ifikapo Oktoba, 2020 wahamasishwe kujitokeza kwa wingi na kujiandikisha katika daftari hilo.

Hayo ni miongoni mwa yale, ambayo Waziri Mkuu amesisitiza, na kusema vijana ndio walengwa wakuu kwa vile wanaingia kwa mara ya kwanza katika uchaguzi, hivyo ni muhimu kuyazingatia ili elimu hiyo iwe na matokeo mazuri.

Kama anavyosema Waziri Mkuu, bila kujiandikisha hawataweza kutumia haki yao ya msingi ya kuchagua viongozi wanaowataka, na kwamba kujiandikisha kwao kutawahakikishia ushiriki wao katika uchaguzi wa viongozi.

Walengwa pia wasiwe tayari kusikiliza mambo ambayo yataelezwa yakiwa kinyume na malengo la elimu ya mpigakura, vinginevyo wanaweza kuingizwa katika mtego bila wao kujua.

Watoaji wa elimu ya mpigakura watakaoweka pembeni, sheria, kanuni na taratibu na kujihusisha na itikadi za kisiasa, udini, ukanda na ukabila, waogopwe kama ukoma ili wasilipeleke taifa kubaya.

Ikumbukwe kuwa Watanzania wanaunganishwa na Utanzania wao, siyo kwa itikadi za kisiasa, udini, ukanda na ukabila, hivyo jambo la muhimu ni kuendelea kuwaunganisha kama walivyo.

Vilevile wapo baadhi ya Watanzania ambao hawana dini wala hawako kwenye vyama vya siasa, lakini wote wanaunganishwa na Utanzania wao na siyo ukanda, ukabila, udini wala itikadi za vyama vya siasa. Kwa maana hiyo watoaji wa elimu, ambao hawatazingatia mwongozo kama wanavyotakiwa, basi waogopwe kama ukoma ili wasilipeleke taifa kubaya, kwani watakuwa wanalenga kuwagawa Watanzania.

Niseme tu kuwa hata wanasiasa nao wanatakiwa kuhakikisha kwamba mambo yote ya kisiasa wanayosimamia, kuyatetea na kuyasifia yanatakiwa kuwakilisha maslahi ya Watanzania wote kwa ujumla.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# ACT-Wazalendo yaanika mbinu ya kuibwaga CCM

INATOKA UK. 2

Tanzania ila siyo suala la mimi kupenda bali ni kuangalia muktadha na mambo mengi, kama viongozi wenzangu wataona naweza kubeba jambo hilo nitafanya hivyo kwa manufaa ya Watanzania," alifafanua Zitto alipoulizwa kama ana nia ya kugombea nafasi hiyo.

Kwa upande wake Maalim Seif, alisema bado hajafanya maamuzi ya kugombea urais, na kwamba inahitaji tafakari ya kina na muda wa kutosha ikiwamo kujipima binafsi, kuangalia mazingira, kushauriana na viongozi wa chama na maoni ya wananchi kama anafaa kugombea nafasi hiyo.

Kuhusu mipango ya 2020 kwa Tanzania Bara, Zitto alisema ACT-Wazalendo imedhamiria kuijenga Tanzania inayopaa kiuchumi, yakubuni na kutekeleza sera zitakazohakikisha uchumi shirikishi unaozalisha ajira.

"Ni muhimu wananchi kufahamu kuwa tutapokea uongozi wa nchi wenye changamoto lukuki zinazotokana haswa na muundo wetu wa idadi ya watu na maandalizi yetu ya kukabiliana na baraka hizo za idadi kubwa ya Watanzania," alisema.

Kwa mujibu wa Zitto, kuna wanafunzi wa shule za msingi wapatao milioni 11 na watafikia milioni 16 ifikapo mwaka 2025, na kwamba inatakiwa kuongeza vyumba vya madarasa 24,000 kila mwaka, na pia kunahitajika kuongeza shughuli za uchumi ili Watanzania wapate ajira, kwa kuwa wataingiza watu milioni 1.6 kwenye soko la ajira kila mwaka tofauti na sasa ni watu 70,000 ndiyo wanapata ajira.

"Nataka chama chetu kiongoze serikali itakayovutia uwekezaji kutoka nje... ili kuongeza mitaji nchini na kupanua shughuli za uzalishaji mali, tuongeze idadi ya watalii nchini kufikia milioni sita kwa mwaka ili kutengeneza ajira nyingi na bora, na pia kuongeza mapato ya fedha za kigeni," alibainisha.

Alisema anataka chama kiongoze serikali itakayotekeleza sera sahihi zitakazojenga uwezo wa kufaidika zaidi na rasilimali za madini, misitu, mafuta na gesi.

Kwa mujibu wa Zitto ambaye ni Mbunge wa Kigoma Mjini, uchumi wa watu ndio unaojenga taifa imara na siyo uchumi wa serikali, na kwamba chama hicho kitajenga uchumi wa wananchi kupitia vyama vya ushirika, jumuiya za wafanyabiashara na vyama vya wafanyakazi.

Naye Maalim Seif alisema Tanzania wanayoiwaza ni yenye huduma bora za kijamii, kwa kutoa elimu bora, na inayokwenda na wakati, inayozalisha wahitimu wenye weledi, ubunifu na uwezo katika nyakati hizi za sayansi na teknolojia.

Alisema Tanzania yenye wakufunzi wa kutosha, madarasa na vitendea kazi, huku mkazo ukiwekwa zaidi kwenye elimu ya ufundi, ikiwamo kuwa na huduma bora na nafuu za afya, inayojikita kwenye kuwakinga na kuwatibu wananchi, kwa kuwa na zahanati, vituo vya afya na hospitali za kutosha, zenye watendaji wenye sifa, vitendea kazi na vifaa tiba vya kutosha.



Wakazi wa jijini Dar es Salaam wakiwa wamejipanga foleni kwa ajili ya kujiandikisha kupata vitambulisho vya Taifa Nida katika Viwanja vya Mnazi Mmoja jana. **PICHA NA JUMANNE JUMA**

# Magereza yajipanga kuzalisha chakula kwa wafungwa

INATOKA UK. 5

Alisema kuwa kuna mkakati wa muda mrefu wa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia vyanzo vya maji vilivyopo katika maeneo mbalimbali ya magereza na jeshi hilo, tayari limekamilisha andiko linalohusu mapindizi ya kilimo na tayari limewasilishwa serikalini katika hatua mbalimbali za ngazi ya uamuzi.

Akizungumzia mafanikio mengi ya kujivunia kwa mwaka 2019, Kamishna Jenerali Kasike alisema kumekuwa na mwitikio mkubwa miongoni mwa maofisa na askari katika kuishi na ajenda mahususi ya jeshi hilo kuhusu umuhimu wa kubadilika kimtizamo, kifikra na utendaji kama nguzo ya mabadiliko katika jeshi hilo.

"Naomba nisisitize kuwa bado tuendelee kuishi na ajenda hii ya mabadiliko ya kimtizamo na kifikra katika mwaka mpya 2020 kwa kufanya kazi kwa weledi, ubunifu katika maeneo yetu ya kazi. Tradition die hard", alisisitiza Kamishna Jenerali Kasike.

Mafanikio mengine aliyoyaainisha ni pamoja na utekelezaji wa agizo la serikali kuhusu kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa, ujenzi wa nyumba za watumishi wa jeshi hilo katika maeneo mbalimbali nchini kwa njia ya ubunifu, udhibiti wa uingizaji wa vitu visivyoruhusiwa gerezani kwa kufunga kamera za CCTV katika baadhi ya magereza pamoja na kuhakikisha kuwa wafungwa waliopo gerezani wanafanya kazi.

"Shirika la Magereza limefanikisha utaratibu wa kuingiza miradi yake yote katika mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ya serikali (GePG) na hivyo kuziba mianya ya upotevu wa mapato. Pia, shirika hilo limetoa mchango wake serikalini kiasi cha Sh. milioni 130 kwa mwaka 2019," alisema.

Alitaja changamoto zinazolikabili jeshi hilo ikiwamo ufinyu wa bajeti, uhaba wa vitendea kazi mbalimbali kama vile magari, vyombo vya mawasiliano, pia changamoto za makazi na uchache wa nguvu kazi ya maofisa na askari katika jeshi hilo.

# Kigwangalla amaliza mwaka kwa uchungu

INATOKA UK. 2

wa Uhifadhi, Fredrick Mofulu kwa kazi nzuri ya kudhibiti ujangili katika Hifadhi ya Taifa ya Rubondo, kutunza mazalia ya samaki na ndege ambao husafiri kutoka nchi mbalimbali duniani na kutunza uoto na wanyama mbalimbali waliomo katika hifadhi hiyo.

Aliahidi kuwa serikali itatoa Sh. bilioni mbili kwa ajili ya kununua kivuko chenye uwezo wa kuchukua watu 100 na magari manne ili kurahisisha usafirishaji wa watalii wanaoingia na kutoka katika Hifadhi ya Taifa ya Rubondo wakiwa na magari yao.

Rais Magufuli alisema kwa sasa Tanzania ina bustani za wanyamapori 23, mashamba ya wanyama 20 na ranchi sita na ametoa wito kwa Watanzania wakiwamo wastaafu katika tasnia ya wanyamapori kujitokeza kuanzisha bustani za wanyamapori, mashamba ya wanyama na ranchi ambazo zitasaidia kuvutia watalii na kuongeza kipato.

Mapema akimkaribisha Rais Magufuli, Kamishna Kijazi alimshukuru kwa juhudi zake za kutilia mkazo shughuli za uhifadhi na kupanua maeneo ya uhifadhi kutoka hifadhi 16 mwaka 2015/2016 hadi kufikia hifadhi 22 hivi sasa na ameahidi kuwa Tanapa itahakikisha hifadhi hizo zinatunzwa kwa manufaa ya taifa.

Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo, Kamishna Msaidizi Mofulu, alisema hifadhi hiyo yenye ukubwa wa kilometa za mraba 456.6 ina wanyama mbalimbali wakiwamo sokwe, pongwe, swala, tembo, twiga na pia ni mazalia ya samaki wa Ziwa Victoria na ndege mbalimbali, na kwamba katika kipindi cha kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2018/19 idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi hiyo imeongezeka hadi kufikia 5,700 kwa mwaka, walioingiza Sh. bilioni 1.4 katika Pato la Taifa.

Rais Magufuli amekuwa Rais wa kwanza kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo, akiwa madarakani.

# Mabalozi wamlilia mama wa mwandishi Kabendera

INATOKA UK. 3

wengine, hata kama ni mkubwa, ni mzazi na analea watoto. Namwomba anionee huruma. Angalia maisha yalivyo magumu, dawa sipati, naomba Rais anisaidie kama anavyosaidia wazazi wake," alisema.

Erick Kabendera alikamatwa Julai mwaka jana na baadaye kufikishwa mahakamani akikabiliwa na mashtaka ya utakatishaji fedha, kukwepa kodi na kuongoza kikundi cha uhalifu.

Tayari mawakili wake wamefungua majadiliano na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ili kukiri makosa na kuomba msamaha, utaratibu ambao ulipendekezwa na Rais Magufuli mwishoni mwa mwaka jana kwa washtakiwa mbalimbali wanaokabiliwa na mashtaka ya uhujumu uchumi.

# Wafagilia ununuzi kilo 250,000 tumbaku

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa Chama cha Msingi Ngokolo, Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameipongeza kampuni ya Petrobena kwa kununua tumbaku kilo 250,000 iliyokuwa imebaki na kugawa pembejeo za kilimo hicho kwa msimu ujao kwa wakati.

Pongezi hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa chama hicho cha msingi, Ally Hamisi, wakati akizungumza na vyombo vya habari katika ofisi za chama kikuu cha ushirika wilayani Kahama (KACU), ambapo alisema wakazi wengi wa Halmashauri ya Ushetu wanategemea kilimo cha tumbaku kwa maisha yao.

Alisema awali wakulima wa tumbaku walikuwa wameshakata tamaa ya kuendelea kulima zao hilo baada ya kuona tumbaku ambazo inayozalishwa nje ya kilimo cha mkataba inakosa soko na kutaka kujikita kwenye kilimo cha pamba.

Aidha, Hamisi alisema, Chama cha Msingi Ngokolo kinawanachama hai 295 ambao baada ya kununuliwa kwa tumbaku iliyokuwa imebaki kilo 250,000 na Petrobena, wakulima hao wamelima zaidi ya hekta 220 za tumbaku kwa ajili ya msimu ujao.

"Wakulima wangu walipoteza imani ya kuendelea kulima tumbaku baada ya tumbaku iliyozidi kwenye mikataba yao kukosa masoko, na kutishia kukimbilia kwenye kilimo cha pamba...sasa tumepata kampuni ya Petrobena imerudisha imani ya wakulima na kujitokeza kwa wingi kulima tena," alisem Hamisi.

Hamisi aliomba uongozi wa kampuni hiyo kukiruhusu chama hicho kuongeza uzalishaji kutokana na ukubwa wa chama hicho, na kuongeza kuwa msimu ujao wanamatarajio ya kuzalisha kilo 700 ambazo zitakuwa na ubora unaohitajika kwenye soko la dunia.

Mwenyekiti wa KACU, Emmanuel Charahani, aliipongeza kampuni hiyo kwa kusambaza pembejeo kwa wakulima na kwa kufuata kalenda tena kwa bei ya chini ambayo itampatia faida mkulima.

Hata hivyo, Charahani aliutaka uongozi wa kampuni hiyo kuelekea katika maeneo mengine kununua na kugawa pembejeo kwa wakulima katika maeneo ya Chunya, Kigoma, Mpanda na Serengeti ambapo nao wana changamoto ya ukosefu wa kampuni ya ununuzi wa zao hilo.

Pia aliwataka wakulima mkoani Shinyanga kuendelea kulima tumbaku yenye ubora ili kampuni ziendelee kujitokeza kwa wingi kununua tumbaku, na kuongeza kuwa zinapojitokeza kampuni kwa wingi ndivyo mkulima anavyopata faida.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu jeshi hilo kuimarisha ulinzi Mwaka Mpya katika maeneo mbalimbali ya jiji. **PICHA NA JUMANNE JUMA**

# Wazazi, walezi waonywa ulinzi watoto ufukweni

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera limetoa wito kwa wazazi na walezi kutoruhusu watoto kwenda katika sehemu za fukwe za Ziwa Victoria na kuogelea bali kuambatana na waangalizi kuangalia usalama wao.

Uimarishwaji wa ulinzi katika maeneo mbalimbali ya jamii nyakati za sikukuu Krismasi na Mwaka Mpya 2020 ni maagizo yaliyotolewa na Inspekta Jenerali wa Polisi, Simon Sirro, alioutoa akiwa mkoa wa Pwani Desemba 20, mwaka jana.

Akizungumza na wanahabari Mjini Bukoba, Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alisema muda wa kufungwa maeneo ya fukwe ni 12:00 jioni.

Malimi alisema jeshi hilo litafanya doria nyakati za usiku na mchana katika mikusanyiko ya watu kwenye fukwe za ziwa, kumbi za starehe na kuzungukiwa askari wa doria.

Aidha, alisema ametoa maelekezo kwa wamiliki wa maeneo hayo kuimarisha ulinzi wao wa ndani.

Alisema pia wananchi waweke ulinzi wa makazi yao kuepusha udokozi wa mali.

# Wanawake wanolewa kugombea uongozi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Pemba, kinaendelea kuielimisha na kuihamasisha jamii kuhusu ushirikishwaji wa wanawake katika uongozi, ili kuondoa mfumo kandamizi dhidi yao katika masuala ya uongozi.

Akizungumza katika mdahalo wa kuwahamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi uliofanyika katika ofisi ya Tamwa Mkanjuni Chakechake, mkufunzi kutoka Kituo cha Huduma za Sheria, Siti Habib Mohamed, alisema Tamwa imeona kwamba ipo haja kuongeza uhamasishaji ili kuelezea suala hilo.

Alisema bado wanawake wapo nyuma katika uongozi, idadi yao ni ndogo katika vyombo vya kutoa maamuzi, hivyo Tamwa kwa kuliona hilo wanaendelea kuielimisha na kuihamasisha jamii, ili kuondoa mfumo kandamizi uliopo na kuleta usawa kati ya wanawake na wanaume katika mambo mbalimbali, ikiwamo la uongozi.

"Tamwa imeona ipo haja ya kuongeza uhamasishaji ili wanawake wagombee, kwani kuna ukandamizwaji wa wanawake katika masuala haya ya uongozi," alisema.

Siti alieleza kuwa wanawake wana upendo na maumivu, hivyo huweka usawa kwa watu wote na watakapokuwa viongozi ni wepesi wa kuleta maendeleo. Ali Mbarouk Omar kutoka Klabu ya Waandishi wa Habari Pemba (PPC), alisema, Tamwa inatoa elimu hiyo kwa lengo la kuleta mabadiliko na mafanikio ndani ya jamii.

"Wanawake wana uwezo wa kuleta maendeleo kwa haraka, tushirikiane tuwachague wanawake ili kupata maendeleo haraka," alisema. Aliwataka wanawake hao kuwa tayari na kuacha tabia ya kudharauliana, badala yake kila mmoja aone anaweza kuleta mafanikio.

"Uongozi unahitaji uvumilivu, ustadi, pia uendane kutokana na mienendo ya kisiasa na hali halisi ilivyo, usiwe mbaguzi, uthamini na upende watu," alisema Ali.

Akifungua mdahalo huo, Mratibu wa Tamwa-Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema wanaihamasisha jamii ili kuondokana na dhana potofu ya kuwa mwanamke hawezi kuongoza, kwani jamii kubwa imemuona ni mama wa nyumbani hastahili kuwa kiongozi, jambo ambalo sio sahihi.

"Tunatoa elimu kwa jamii ili kuona ifikapo mwaka 2020 wanawake wanaingia kwa wingi majimboni kuchukua fomu za kugombea nafasi uongozi," alisema.

Aliwataka wanawake kutovunjika moyo kwa zile changamoto wanazokumbana nazo, badala yake wazifanye kuwa ni fursa kwao ili waweze kufanikiwa. Akichangia, Katibu wa CUF Wilaya ya Wete, Sharif Seif Haji, alisema mwanamke ni mwenye ushawishi mkubwa, hivyo atakapopata uongozi, anaamini mafanikio yatapatikana kwa haraka.

Mwenyekiti wa vijana Jimbo la Wete kupitia Chadema, Asha Seif Massoud, alibainisha kuwa mwanamke anapokuwa kiongozi huleta usawa katika familia na jamii kwa ujumla. Naye Mwenyekiti wa mabaraza ya vijana CCM Wilaya ya Micheweni, Said Saleh Salum, aliomba Tamwa kuzidi kuwaelimisha wanawake hasa vijijini, ili waelewe na wajitambue kwamba na wao wanaweza kuwa viongozi.

Amira kutoka Wilaya ya Wete, Asya Ibrahim, aliwataka wanawake ambao watafanikiwa kuwa viongozi, wajitambue na wajue wajibu wao kwa waume zao na familia, hiyo itawajengea heshima zaidi.

Mdahalo huo uliwashirikisha viongozi wa dini na vyama vya siasa Mkoa wa Kaskazini Pemba, na uliandaliwa na Tamwa kwa Ufadhili wa UN WOMEN.

# Wacheza 'pool', bao wakati wa kilimo kukiona

**Na Tiganya Vincent,**
TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, amepiga marufuku watu wazima na vijana kucheza michezo mbalimbali ikiwamo pool, bao na karata nyakati za asubuhi ili kutumia muda huo kwenye shughuli za kilimo na uzalishaji mali.

Hatua hiyo itasaidia kukabiliana na udhururaji na uzembe unaofanywa na baadhi ya vijana nyakati ambazo wanatakiwa kuwa shambani kulima mazao kwa ajili ya maendeleo yao.

Mwanri alitangaza marufuku hiyo wilayani Kaliua wakati wa ziara yake ya kuhamasisha kilimo bora na ufanyaji wa kazi kwa bidii.

Alisema watu wanaoshinda wakicheza michezo mbalimbali wakati wenzao wako shambani wakilima ndio wanakuwa wa kwanza kudai chakula cha msaada pindi wanapokabiliwa na njaa.

Mwanri aliwataka viongozi kuanzia ngazi ya wilaya hadi vitongoji kuhakikisha hakuna vijana ambao watakuwa mitaani wakicheza michezo mbalimbali wakati wanapaswa kuwa shambani.

Aliongeza kuwa watu wa aina hiyo ndio wanasababisha ucheleweshaji wa maendeleo na wakati mwingine wanakuwa wa kwanza kuomba chakula cha msaada pindi wanapokuwa hawana chakula.

"Ni marufuku kucheza pool, karata na bao wakati huu...ni lazima watu wote wenye uwezo wa kufanyakazi wawe mashambani...michezo hiyo ianze nyakazi za jioni...tukiendekeza michezo hiyo nyakati za kilimo," alisema na kuongeza:

"Tabora tutabaki watazamaji wa maendeleo wakati mikoa mingine inapiga hatua sisi tutabaki kulalamika kwa sababu ya kuendekeza michezo nyakati za kilimo."

Aliongeza kuwa baadhi ya watu wa aina hiyo wakati mwingine ndio wanahisiwa kujihusisha na vitendo vya uhalifu ukiwamo wizi na ukabaji kwa kuwa hawana shughuli ya kujipatia kipato halali.

"Hivi kijana ambaye kila siku yuko kwenye bao, karata anapata wapi pesa za kujikimu yeye na familia yake, ni lazima tujiulize vijana, ndio wazazi wa sasa wanajibika kubeba majukumu ikiwamo kufanyakazi kwa bidii kwa ajili ya ustawi wao na watoto wao," alisisitiza.

Alisema ni lazima kila mtu mwenye uwezo wa kufanyakazi kuhakikisha kuwa anafanyakazi halali na kuwa na uhakika wa chakula cha kutosha, na kuwa na ziada itakayomsaidia katika shughuli za maendeleo yake.



Mwendesha pikipiki maarufu 'Bodaboda' Mkazi wa Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya, akiwa amepakia watoto watatu juzi, kitu ambacho ni hatari na Jeshi la Polisi limekuwa likipiga marufuku vitendo hivyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Bil. 1/- kukopesha wanawake, vijana

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

MIKOPO ya zaidi ya Sh. bilioni moja itatolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza ifikapo mwaka 2020 kuwawezesha kufanya kazi zitakazowakwamua kiuchumi.

Hayo yalibainishwa na Mbunge wa Ilemela, Angeline Mabula, katika ziara ya kutembelea vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na kuzungumza na vikundi katika kata za Kawekamo, Kiseke, Ilemela, Pasiansi na Nyasaka.

Alisema Sh. milioni 600 zimekopeshwa, huku Sh. milioni 538 zinatarajiwa kuongezwa, hivyo kufikia mwaka 2020 Sh. bilioni 1.138 zitatolewa.

Alisema vikundi 671 vya halmashauri hiyo vilipatiwa elimu ya mikopo na biashara kutoka kwa ofisi ya mbunge, ingawa changamoto iliyopo ni vikundi vingi kutokuwa na ofisi, kutorejesha kwa wakati, huku akifafanua umri wa kundi la vijana wanaopaswa kupata mkopo ni mwenye miaka 18 hadi 35.

"Ili wanavikundi msikwame kurejesha mkopo mnatakiwa muwe na kikundi kinachofanya shughuli moja, mnaofahamiana kitabia pamoja na kutengeneza bidhaa tofauti na za vikundi vingine kwa ajili ya kupata fursa ya masoko," alisema na kuongeza:

"Kuweni wabunifu katika biashara zenu huku halmashauri ikiendelea kutoa elimu ya mikopo na biashara, hata kama mtu hataki kukopa halmashauri."

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, ambaye ni Ofisa Ardhi na Mipango Miji, Shukrani Kyando, alisema, serikali ilitoa maelekezo ya fedha hizo za asilimia 10 kwa ajili ya mikopo ya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu kufunguliwa akaunti yake maalumu, hivyo halmashauri hiyo imetekeleza agizo hilo, na kuwa mpaka sasa akaunti ipo tayari na watu watarejesha na kukopa kupitia akaunti hiyo.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii, ambaye ni Mratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake Manispaa ya Ilemela, Amina Bululu, aliwataka wanavikundi wa makundi hayo matatu yaliyotengewa jumla ya asilimia 10 kuhakikisha akaunti zao za vikundi kuwa hai, kupata usajili wa Manispaa, kuwa na mradi wa pamoja, kulipa ada ya kikundi, na kutoa taarifa kila baada ya miezi mitatu.

Kudra Nyahonge, Richard Kashinje na Godfrey Julius, baadhi ya wanavikundi walioshiriki walisema wanaume ndio wamekuwa chanzo cha kuwakwamisha wanawake kwani wanachukua fedha na kushindwa kurejesha kutokana na kutozifanyia biashara.

Vikwazo vingine ni baadhi ya viongozi kutokuwa waaminifu kwa kugawana fedha za mikopo ya kikundi husika na deni likibaki kwa kikundi chote pamoja na baadhi yao kukimbia na kusababisha wanakikundi kumchangia pamoja na huku maofisa maendeleo kutowatembelea.

# Kiwango ukeketaji chaishtua UNFPA

**Na Sabato Kasika**

MWANAMKE mmoja kati ya 10, wenye umri wa miaka 15 hadi 49 nchini, amefanyiwa ukeketaji nchini, asilimia 35 kati yao wakiwa wamekeketwa, kabla ya kufikia umri wa mwaka mmoja.

Takwimu hizo ni za Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA), ambapo Mwakilishi Mkazi wa shirika hilo nchini, Jacqueline Mahon, anasema ukeketaji umeenea maradufu katika maeneo ya vijijini kwa asilimia 13 kuliko mijini, ambako ni asilimia tano kwa mujibu wa utafiti uliofanya.

Akizungumzia takwimu za Juni 2018, Mahon alisema ongezeko la idadi ya watu linahatarisha maendeleo na juhudi zilizofikiwa za kutaka kukomesha vitendo vya ukeketaji nchini.

"Hii inatokana na uhalisia kwamba wasichana wako hatarini kukeketwa zaidi, hivyo kupungua ukeketaji kuliko shuhudiwa, hakutoshi kuleta uwiano wa uongezeko la idadi ya watu linalotarajiwa," anasema Mahon.

Anafafanua kuwa ukeketaji umejikita kwenye kanuni na taratibu za kijamii, imani za kitamaduni, vichocheo vya kiuchumi na unaonekana kutumika kama njia ya kudhibiti hamu ya kujamiiana kwa wanawake.

Mahon anasema katika jamii nyingi inachukuliwa kama jambo la muhimu kwenye shughuli za jando na unyago, simulizi potofu kuhusu ukeketaji zimekuwa zikirudiwa na mara nyingi kiasi cha kusadikiwa ukweli wake.

Aidha, anaitaka jamii kutumia njia mbadala kwenye sherehe za jando na unyango, programu hizo zizingatie makundi mbalimbali yanayojihusisha na ukeketaji wakiwamo ngariba.

"Kuna maeneo salama yanayopaswa kuanzishwa kwa ajili ya wasichana waliopo hatarini, pia mipango ya sekta ya afya inayotakiwa kujumisha mikakati ya kuzuia na kutokomeza ukeketaji," anasema.

Anaongeza kuwa njia mbadala katika kutekeleza shughuli za unyago kama sehemu ya programu pana ya kukomesha ukeketaji, zaweza kutumika na kutoa msaada wa kuongeza idadi ya wasichana kukwepa ukatili huo.

"Wasichana wanaweza kushiriki kwenye programu hiyo na kuhakikisha upatikanaji wa msaada wa kisaikolojia kwao na kwa wazazi wao, kwani hii ni ni sehemu ya programu pana inayoungwa mkono na UNFPA, ambayo inahusisha kujenga uwezo wa vyombo vya habari, polisi, mahakama, walimu na waganga wa jadi, katika kuzuia ukeketaji," anasema.

# Bawasa wajisifu kuokoa fedha

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Babati (Bawasa), imesema miradi mingi ya maji inayotekelezwa wilayani Babati inasimamiwa na wao badala ya makandarasi ili kuokoa gharama.

Hayo yalisemwa jana mjini Babati na Mkurugenzi Mtendaji wa Bawasa, Mhandisi Iddy Msuya, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake.

Alisema Bawasa pia inatekeleza agizo la Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, alilolitoa Dodoma hivi karibuni, kuwa mamlaka zote zisiwape kazi makandarasi wenye miradi ya maji kuanzia mitatu, kwa sababu wanashindwa kuisimamia.

"Hili tumelisimamia kwa sababu wengi wakiwa na miradi mingi wanashindwa kutekeleza kwa wakati, lakini hawa watu wanakuwa na gharama kubwa tofauti na sisi wenyewe Bawasa tukitekeleza," alisema.

Alisema kwa upande wao hawana mkandarasi anayetekeleza miradi zaidi ya mitatu, kwa sababu mingi wanafanya kazi ya kusimamia wenyewe.

"Tunafanya hivi kwa sababu tunafahamu ukitaka chakula kizuri, lazima upike mwenyewe, hivyo hata katika miradi tukitaka mzuri lazima tusimamie wenyewe," alisema Mhandisi Msuya na kuongeza:

"Tulianza kulifahamu hili na kutekeleza kwa kusimamia miradi yetu wenyewe toka mwaka 2016/2017 na mfano mzuri kuna mradi mmoja (hakuutaja), ulitakiwa kugharimu Sh. bilioni moja kama tungempa mkandarasi, lakini Bawasa tuliutekeleza wenyewe na tulitumia Sh. milioni 500," alisema. Mkurugenzi huyo alisema wanapofanya hivyo, inawasaidia kupunguza gharama za mabomba kwa kuwa wakitumia makandarasi, wanaambiwa gharama za mradi kubwa kwa sababu ya ununuzi wa mabomba uko juu.

Mkazi wa Babati, Imani Kalikawe, alisema kama Bawasa wanasimamia wenyewe miradi ya maji wataendelea kuona matokeo mazuri na miradi haitachelewa kwa kuwa wana hofu ya kukalipiwa na viongozi wao wa juu, tofauti na mkandarasi ambaye anaangalia mkataba wake.

Jackline Bahati, aliishauri serikali kujiridhisha kuhusu uwezo wa makandarasi wanaowapatia ujenzi wa miradi ili wananchi wapate majisafi na salama kwa wakati.



Wanaushirika wa Mirerani Multipurpose Cooperative Society Ltd wa Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wakiwa kwenye kikao. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanawake, vijana wanolewa uchaguzi mkuu

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WANAWAKE na vijana wanaojipanga kuwania nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu mwaka 2020 katika Mkoa wa Arusha, wametakiwa kujiamini na kuacha woga ili washinde nafasi watakazowania.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Mkoa wa Arusha, Anna Msuya, alisema hayo katika mafunzo ya kukuza ushiriki wa wanawake na vijana, katika uongozi kutoka wilaya za mkoa huo yaliyoandaliwa na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA). Msuya alisema, endapo makundi hayo mawili yana nia ya dhati ya kushika nafasi za uongozi, hususani udiwani, hawana budi kuwa na ujasiri, wajiamini na kuacha uoga, kwa kuwa wasitegemee uchaguzi huo utakuwa mwepesi. "Nawaomba muwe na mkakati na mbinu za kupambana kupata uongozi katika uchaguzi huo na kwa vyovyote mtakutana na makundi yatakayowatisha na mengine kuwakatisha tamaa, lakini mtakutana na watu wenye uzoefu katika siasa," alisema.

Msuya aliwasisitiza kuwa katika kuwania uongozi, ni vyema wakazingatia maadili na kuepuka makundi maovu na kuachana na tabia zisizokubalika katika jamii ikiwamo ya ulevi wa kupindukia na uzinzi.

Alisema wanawake wana changamoto kubwa zaidi kuliko vijana, kwa kuwa licha ya kuingia katika uongozi, bado watalazimika kutekeleza majukumu yao ya asili, ambayo aliyataja kuwa ni pamoja na kutumikia taifa, mume, watoto na jamii. "Ni vyema kuiandaa familia kabla ya kuingia katika uongozi, tuna mifano mingi tu ya baadhi ya wanawake walioingia katika uongozi, baadaye familia zao zilivurugika na kusambaratika kabisa," alisema.

Naye mkufunzi wa mafunzo hayo, ambaye ni Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Arusha, Firmin Nnko, alisema kupitia mafunzo hayo, anaamini vijana na wanawake hao wameiva na hivyo katika maeneo wanayotoka kutapatikana viongozi bora watakaoitumikia vyema jamii. Nnko alisema vijana na wanawake hao wanaandaliwa bila kujali itikadi ya vyama vya siasa wanakotoka kwa kuwa katika kuhudumia jamii hahitaji vyama.

Mratibu wa mafunzo hayo, kutoka TAWLA Mkoa wa Arusha, Silvia Mwanga, alisema mafunzo hayo yanafanyika kupitia mradi wa kukuza ushiriki wa vijana na wanawake katika uongozi (WYPRE).

"Kupitia mradi huu tumeandaa mafunzo kwa vijana na wanawake wanaoonyesha nia ya kutaka kugombea nafasi za uongozi na tumeanza kwa ngazi za udiwani na baadhi walishawahi kugombea katika chaguzi zilizopita," alifafanua.

Alizitaja changamoto kubwa walizobaini kwa wanawake ni pamoja na kutokujiamini, rushwa ya ngono na familia zao kutokupendezwa na wao kujitosa katika siasa, pamoja na vita iliyopo miongoni mwa wanawake wenyewe.

Mafunzo hayo yamewashirikisha viongozi watarajiwa wa makundi ya wanawake na vijana kutoka katika Halmashauri za Wilaya ya Longido, Arusha, Meru, Monduli, Karatu na Arusha Jiji.

## Wafugaji kunufaika elimu ufugaji kisasa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAFUGAJI zaidi ya 7,000 kutoka mikoa minne ya Arusha, Tanga, Mwanza na Dar es Salaam, wanatarajia kunufaika na elimu ya ufugaji bora wa kisasa, utakaowakwamua kiuchumi.

Akizungumza jana jijini hapa, kwenye kikao cha kuweka mikakati ya kuwafikia wafugaji hao, kupitia elimu kwa njia ya radio, Ofisa Mradi wa Shirika la Radio kwa wakulima (Farm Radio International), Eliakunda Urio, alisema, wanafanya kazi na wakulima na wafugaji, kwenye maeneo ya mradi, ili kuhakikisha wakulima na wafugaji wanafikia malengo yao kwa kupata elimu iliyo bora.

Urio alisema, wafugaji hao watakaonufaika, wamekuwa wakifanya shughuli zao katika ufugaji wa ng'ombe, kuku, mbuzi na kondoo na watapata elimu ya mifugo hiyo, na matumizi sahihi ya dawa za kudhibiti magonjwa.

Alisema wamefikia hatua ya kutumia vyombo vya habari, kwa kuwa ni nyenzo muhimu inayotatua changamoto ya uhaba wa wataalamu wa maofisa ugani inayowakabili wakulima na wafugaji nchini, kwa kuandaa vipindi vinavyotoa fursa kwa walengwa kuwasiliana moja kwa moja na wataalamu. Ofisa Msaidizi Kitengo cha Radio ya Shirika hilo, Clara Moita, alisema elimu hiyo inatolewa kupitia mradi wa miezi sita wa afya ya mifugo na wamekuwa wakitoa mafunzo kwa waandaaji wa vipindi kabla ya kuanza kutekelezwa kwa vipindi hivyo kwa wakulima.

Clara alisema elimu wanayoitoa kwa wakulima na wafugaji kupitia radio, imeleta mafanikio makubwa, kutokana na kuwafikia wakulima wengi, hasa waliopo vijijini na kwa wakati mmoja na hatimaye kuongeza pato kutokana na kufuga na kulima kisasa.

Naye mfugaji wa kuku kutoka Nyamagana, mkoani Mwanza, Betty Masumbigana alisema, wanakabiliana na changamoto nyingi katika ufugaji wao, ikiwamo magonjwa yanayoshambulia mifugo mara kwa mara, na kupitia vipindi hivyo, wameona manufaa makubwa kutokana na kupata ushauri jinsi ya kufuga kutoka kwa wataalamu waliobobea.

Alisema kupitia vipindi hivyo vimeleta matokeo chanya, ambayo kwa asilimia kubwa yameanza kuziba pengo, baina ya wakulima, wafugaji na wataalamu wa ugani.

# Majina 3 wagombea M/kiti UVCCM kupigiwa kura

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

VITA ya nani atakuwa mrithi wa aliyekuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), katika Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Wilson Mushi, inahitimishwa rasmi leo, baada ya majina ya wagombea watatu kupelekwa kwa wajumbe wa mkutano mkuu maalum kupigiwa kura.

Jana, Katibu wa UVCCM wa wilaya hiyo, Bulugu Magege, alieleza Nipashe kwa njia ya simu kuwa uchaguzi huo mdogo wa marudio unafanyika katika mji mdogo wa Sanya Juu ambako wajumbe wa mkutano mkuu 271, wataamua nani anafaa kuwaongoza kwa kipindi kilichobakia.

"Ni kweli tuna uchaguzi wa mwenyekiti wa wilaya, tunajaza nafasi ya Mushi ambaye aliajiriwa serikalini kuwa Ofisa Mtendaji wa Kata (WEO). Tayari wagombea wamepatikana na leo (jana) wanapigiwa kura kumtafuta mwenyekiti mpya," alisema.

Aliwataja wanaowania kiti hicho kuwa ni John Barakael Mushi, Gema Michael Mtui na Yohana Lengere. Kabla ya kuelekea katika uchaguzi huo, Magege alionya kuwa uchaguzi unaofanyika ni kama mchezo wa kirafiki, kwa kuwa wote ni wana-CCM na hakuna sababu ya kuwapo na hila, fitina, wala kuvunjana miguu kwa wagombea na wafuasi wao wanaowaunga mkono.

Kwa mujibu wa Magege, wajumbe wa mkutano mkuu maalum jana walikutana kwa ajili ya ajenda moja ya uchaguzi wa kujaza nafasi ya Mwenyekiti UVCCM wa Wilaya ya Siha. Uchaguzi huo unavuta hisia hasa kutokana na wagombea wa nafasi hiyo kuonyesha hamasa kubwa wakati wa kuchukua na kurudisha fomu.

Licha ya kuwapo uchaguzi huo mdogo, wakati wagombea wote wanarudisha fomu zao za kuomba nafasi hiyo kumekuwapo na usiri mkubwa tangu siku ya mwanzo ya kutoa fomu hadi siku ya uchaguzi huo unafanyika.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kilimanjaro (CCM), Jonathan Mabihya, akizungumzia uchaguzi huo alisema, "suala la uchaguzi ndani ya chama na hasa UVCCM, wajumbe wa mkutano mkuu maalum wanapaswa kutambua dhamana waliyopewa ni kubwa hivyo ni jukumu lao kuhakikisha wanawachagua viongozi bora watakaowatumikia.

"Wasichague tu kiongozi kwa kuangalia dini, kabila wala rushwa na badala yake, wawachague viongozi wenye moyo wa dhati wa kukitumikia chama na kukiletea maendeleo."



Mchungaji Enock Makundi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Dayosisi ya Kaskazini (KKKT-DK), akizungumza na vijana wa Shirikisho la Jukwaa la Vijana kutoka madhehebu ya dini mbalimbali mkoani Kilimanjaro (Kilimanjaro Youth Interfaith Forum), namna ya kudumisha amani na upendo nchini na kuboresha miradi mbalimbali ya maendeleo ya jukwaa hilo. **PICHA: JAMES LANKA**

## TGNP Mtandao yanoa viongozi wapya utawala bora

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MTANDAO wa Kijinsia Tanzania (TGNP Mtandao), umekamilisha kazi ya kuwanoa viongozi wapya wa vijiji na wajumbe wa serikali za vijiji vya Maua na Uchau Kusini, Moshi Vijijini kuhusu dhana ya utawala bora.

Kwa mujibu wa Ofisa Mwandamizi wa TGNP, Deogratius Koyanga, viongozi hao walijengewa uwezo kwa siku kadhaa ili waweze kuendesha vijiji vyao vizuri na kitaalamu, huku wakijua sheria na taratibu.

"Tulipokuja kijijini kwa ajili ya mapumziko ya sikukuu za mwisho wa mwaka, wadau wa maendeleo kutoka mashirika ya kiraia tulijitolea kuwanoa viongozi wapya wa vijiji ili waweze kuendesha vijiji vyetu vizuri na kitaalamu wakijua sheria na taratibu.

"Kuna suala zima la uibuaji wa miradi ya maendeleo na namna ya kuisimamia iwe endelevu na pia nimepata nafasi ya kusisitiza ulinzi wa mtoto wa kike asipate mimba, kwa sababu inamuweka katika nafasi ya kukatisha masomo yake."

Kuhusu mafunzo hayo, Koyanga alisema wamefarijika kama wadau kuwajengea uwezo viongozi hao kuhusu utawala bora na haki za binadamu.

Alisema miongoni mwa mambo waliyojifunza ni pamoja na maana ya utawala bora, faida za utawala bora, athari za kukosa utawala bora, misingi ya utawala bora, nguzo za utawala bora, haki za binadamu, misingi ya haki za binadamu, vyanzo vya haki za binadamu, uhusiano kati ya haki za binadamu na utawala bora na misingi ya utoaji wa haki.

Zaidi Koyanga alieleza: "Naamini kwamba mafunzo hayo yatawasaidia kujenga jamii ambayo misingi ya utawala bora na haki za binadamu inakuzwa, inalindwa, inazingatiwa, inatekelezwa na kuhifadhiwa."

Pamoja na mambo mengine, viongozi hao walipewa mafunzo ya ushiriki wa wanawake katika uongozi ikiwamo siasa.

# Tagoane yawakatia watoto 100 wenye VVU bima afya

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WATOTO 100 wanaoishi na virusi vya Ukimwi katika Wilaya ya Siha, sasa wana uhakika wa kuzifikia huduma bora za afya katika maeneo yao, baada ya Mtandao wa Wasanii wa Muziki wa Injili nchini (Tagoane), kuonyesha upendo wao kwa kuwaunganisha na huduma hiyo.

Akiwa katika Wilaya ya Siha, Rais wa Tanzania Gospel Artists Network, Dk. Godwin Maimu, alisema waliona hawawezi kuendelea kuwaacha watoto wanaosumbuliwa na maambukizi ya Ukimwi kutaabika kutokana na maradhi mbalimbali ambayo gharama zake za tiba ni kubwa.

Maimu alitoa taarifa yake jana kuhusu sadaka yao kwa vijana hao, wakati wa kongamano la upendo lililofanyika katika Usharika wa Nasai wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Kongamano hilo liliyakutanisha makundi maalumu ya yatima, watu wenye ulemavu, wajane, wazee na wanaoishi na virusi vya Ukimwi.

"Hatuwezi kuwaacha watoto wanaosumbuliwa na maambukizi ya Ukimwi kuendelea kutaabika kutokana na maradhi mbalimbali ambayo gharama zake za tiba ni kubwa, wengi huathirika zaidi kutokana na kushindwa kumudu gharama za tiba, hivyo Tagoane tumeona kwa kuanzia tuwakatie bima za afya watoto hawa 100 ili waweze kutibiwa mahali popote," alisema Dk. Maimu.

Dk. Maimu alisema watoto yatima waliofaulu kuingia kidato cha kwanza mwaka 2020, Tagoane itawanunulia sare za shule, madaftari, kalamu na vifaa vingine vyote vinavyohitajika kwa ajili ya taaluma.

Katika hatua nyingine, Tagoane pia inatarajia kujenga shule maalum kwa ajili ya watoto yatima na wanaoishi na virusi vya Ukimwi katika Wilaya ya Siha, ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua watoto wote nchi nzima.

"Lengo la kujengwa kwa shule hiyo maalum ni watoto hao waweze kutimiza ndoto zao, huku wakijengwa kisaikolojia kutokana na ukweli kuwa wapo watoto wenye ulemavu na wenye uwezo mzuri wa kielimu, pamoja na ndoto zao za kujiendeleza, lakini wanashindwa kutokana na matatizo waliyonayo," alisema Rais huyo.

Akizungumza katika kongamano hilo, Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, alipongeza Tagoane kwa kuwasaidia watoto 100 wanaoishi na virusi vya Ukimwi kwa kuwakatia bima ya afya, kwa kuwa watakuwa na uhakika wa matibabu muda wote.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Siha, Marko Masue, aliitaka jamii kutokuwaficha watoto wenye ulemavu ndani, badala yake wawatoe ili waweze kunufaika na huduma zinazotolewa ikiwamo ya elimu na matibabu.

"Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa kuna watoto yatima zaidi ya 1,000 na watu wenye ulemavu 355 katika Wilaya ya Siha, lakini bado kuna changamoto ya jamii inaonekana kuwatenga. Ni matumaini yangu kupitia kongamano hili litawaibua ili waweze kupata huduma hizo muhimu," alisema Masue.

TUJIKUMBUSHE



Ukurasa 18

**Oscar Salathiel Kambona**

Wenye sifa tutumie fursa hii kujiandikisha kwenye Daftari



Ukurasa 19



Ukurasa 17

**Wanajeshi 27 wahukumiwa kifo mauaji ya mwandamaji**


# siasa

JUMATANO JANUARI 1, 2020

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 20

**Ajira za watoto zinakiuka haki zao, zipigwe vita**

UCHAGUZI MKUU 2022:

## Wanasiasa 'waivamia' Magharibi ya Kenya

• Mudavadi, Wetangula waendelea kumtesa Odinga

**Na Mashaka Mgeta**

WANASIASA nguli kutoka ukanda wa Magharibi mwa Kenya, Kiongozi wa Chama cha Amani National Congress, Musalia Mudavadi na mwenzake wa Ford Kenya, Moses Wetang'ula wameukosoa mpango wa kuwaingiza wakazi wa maeneo ya ukanda huo kwenye mtego wa kisiasa usiokuwa na tija kwao.

Ingawa ukanda huo hautajwi kuwa na kura nyingi kama ilivyo kwa bonde la ufa na ukanda wa kati, lakini wanasiasa wake ni miongoni mwa wenye ushawishi mkubwa kwa siasa za majukwaani nchini humo.

Hivi sasa, kambi za wanasiasa wa Kenya wakiwamo wawili wanaotarajiwa kuibua ushindani mkubwa katika Uchaguzi Mkuu

**INAENDELEA UK.16**



Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya. **PICHA: MTANDAO**

**Tujenge amani kama siri ya Tanzania ya viwanda** Ukurasa 14

# Tujenge amani kama siri ya Tanzania ya viwanda



Rais John Magufuli (wa tatu kulia), akifungua moja ya viwanda vilivyojengwa hivi karibuni. **PICHA: MTANDAO**

**Na Dk. Felician Kilahama**

NI vema na haki kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mema mengi anayotutendea na kipekee kwa zawadi ya uhai, maana ni kwa neema yake sisi tunapumua.

Vilevile, kwa taifa letu kusherehekea vizuri na kwa amani Uhuru wa Tanganyika (Tanzania Bara) uliopatikana Desemba 9, 1961 wakati bendera ya Waingereza ilipoteremshwa na kuipandisha ya Tanganyika.

Hata hivyo, Tanganyika iliungana na Zanzibar Aprili 26, 1964 na kuanzisha taifa moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa miaka 55 ya Muungano.

Historia inaonyesha kuwa Waingereza walitawala Tanganyika baada ya vita ya kwanza ya Dunia kumalizika Novemba 11, 1918.

Kabla ya hapo eneo la Tanganyika lilikuwa chini ya utawala wa Wajerumani kama sehemu ya eneo la Afrika Mashariki lililojulikana kama German East Afrika (Deutsch Ostafrica).

Baada ya Vita Kuu ya Dunia kumalizika mataifa yaliunda umoja uliojulikana kama "The League of Nations" na chombo hiki kilitarajiwa kuleta umoja na kudumisha amani duniani.

Kwa upande mwingine, sehemu iliyokuwa ikitawaliwa na Wajerumani iligawanywa hivyo kuanzisha nchi tatu za Afrika Mashariki na kuwekewa mipaka ipasavyo.

Pamoja na Waingereza kuitawala Kenya kama koloni lao, pia walikabidhiwa madaraka ya kuisimamia Tanganyika kwa niaba ya umoja huo na mwaka 1922 (mwaka aliozaliwa Baba wa Taifa Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere), eneo ambalo Waingereza walilokabidhiwa kulisimamia kwa niaba ya "The League of Nations", wakaliita "Tanganyika".

Mwaka 1939 ilizuka tena vita ya pili ya dunia wakati Waingereza wakiwa bado wasimamizi wa Tanganyika.

Vita iliisha mwaka 1945 na mataifa yakaanzisha Umoja wa Mataifa (United Nations-UN) Makao Makuu yakawa Jiji la New York, Marekani (USA).

> "Historia inaonyesha kuwa Waingereza walitawala Tanganyika baada ya vita ya kwanza ya Dunia kumalizika Novemba 11, 1918.

Mabadiliko kutoka "the League of Nations" kuwa Umoja wa Mataifa (UN) yalilenga zaidi kuwepo na nguvu ya pamoja katika kuhakikisha kunakuwapo amani na usalama duniani.

Wakati huo, Tanganyika iliendelea kuwa chini ya uangalizi wa Waingereza na kupewa hadhi ya "United Nations Trusteeship" na jina kuwa "Tanganyika Territory".

Kenya na Uganda zilibaki kuwa makoloni ya Waingereza.

Pamoja na Tanganyika Territory kuwa chini ya uangalizi (trusteeship), bado Waingereza walitutawala kama koloni lao maana haikuwa rahisi kuiona tofauti kati ya uangalizi kwa mfumo wa "United Nations Trusteeship" na mamlaka kamili ya kumiliki na kutawala (colonial administration).

Kiuhalisia Wajerumani walikalia ardhi ya Tanganyika kwa kipindi cha miaka 27 na pia Waingereza kipindi cha miaka 42; jumla miaka 69 taifa likiwa chini ya wakoloni.

Wakati Desemba 9, 2019 Tanzania ilisherehekea miaka 58 ya Uhuru wa Tanganyika katika Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza; tuna kila sababu ya kujivunia uhuru wetu.

Tunapolinganisha mafanikio yetu kwa miaka 58 na yaliyopatikana kwa miaka 69 ya ukoloni kuna tofauti kubwa. Maendeleo makubwa yamepatikana ndani ya miaka 58 ya kujitawala.

Baba wa Taifa; Hayati Mwalimu Nyerere mwanzoni mwa uhuru alikuwa na kauli mbiu kama: Uhuru na Amani, Uhuru na Umoja, Uhuru na Kujitegemea, Uhuru na Kazi.

Vilevile, alituasa kwamba hatutakuwa na uhuru kamili iwapo nchi jirani zitaendelea kutawaliwa na wakoloni. Kwa hali hiyo alimaanisha kuongeza nguvu katika harakati za ukombozi barani Afrika. Ili kufanikisha hili kwanza, alikubaliana na marehemu Abeid Amani Karume kuunganisha Tanganyika na Zanzibar, hivyo kuzaliwa taifa la Tanzania.

Maana ya fanikio hilo muhimu na kwa namna ya pekee jitihada zilifanyika tukaunganisha nguvu na kuanzisha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) lenye nguvu kamili.

Isitoshe baada ya kupata uhuru, Mwalimu Nyerere aliona wananchi wengi wanaishi mbalimbali (wametawanyika) kiasi cha kukosa huduma za kijamii.

Hivyo alianzisha mfumo wa Vijiji vya Ujamaa na kukawepo na kaulimbiu: "Ujamaa ni Utu" na baadaye kukawepo Sera ya Ardhi ya Vijiji pia Sheria ya Ardhi ya Vijiji.

Madhumuni hayo yote yakiwa kuviwezesha vijiji kujiletea maendeleo endelevu.

Hivyo tukasema: "Uhuru na Maendeleo" na kwa kupitia huduma za kijamii kama elimu (kisomo cha watu wazima kikawekewa mkazo, na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kuanzishwa).

## AFYA

Vilevile, huduma za afya, maji, miundombinu zikawekewa mkazo ili kuharakisha maendeleo ya jamii nzima.

Baada ya kufanikiwa kuanzisha vijiji, ikafuata azma ya kuhakikisha taifa linapata chakula cha kutosha.

Hivyo kilimo na ufugaji vikapewa msukumo wa kutosha na kukawepo msemo wa: "Siasa ni Kilimo" tokomeza njaa.

Taifa likajenga maghala makubwa ya kuhifadhi nafaka (Silos) na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Magharibi ikawa vinara kwa kuzalisha nafaka kwa wingi.

Kadhalika, Hayati Mwalimu Nyerere alikazania umoja wa kitaifa na kudumisha amani nchini.

Kiswahili kikapewa mkazo ili kuunganisha makabila zaidi ya 120 kuwa kitu kimoja na kwa maendeleo ya taifa. Juhudi hazikuishia hapo tu bali Mwalimu alifuta utawala wa kijadi kupitia machifu.

Vilevile, akaanzisha shule za sekondari za kitaifa ambazo zilichukua wanafunzi toka mikoa yote (mfano, Kibaha Sekondari).

Hali hiyo iliwezesha wanafunzi toka mikoa mbalimbali kukaa pamoja hivyo kupelekea kujenga umoja wa kitaifa na kuishi kwa upendo bila kujali walikotoka.

Mafanikio kwa awamu ya kwanza ni pamoja na kuleta uhuru si tu kwa nchi yetu bali kwa Bara zima la Afrika; ikatujengea umoja wa kitaifa na kuimarisha nguvu za vijiji pamoja na kufuta ujinga kupitia elimu ya watu wazima.

Vilevile, viwanda vingi kikiwamo Kiwanda cha Urafiki vilianzishwa, kujenga Reli ya Tazara pamoja na bomba la mafuta kwenda Zambia (TAZAMA pipeline).

Awamu za serikali zilizofuata tangu ya pili (baada ya Mwalimu kung'atuka madarakani mwaka 1985) na sasa ya Awamu ya Tano; viongozi wake kwa pamoja wamechangia sana maendeleo ya taifa letu ndani ya kipindi cha miaka 34 iliyopita.

Huduma za kijamii zimekuwa zikiimarika mathalani, hali ya upatikanaji wa dawa na vifaatiba imekuwa mzuri; shule nyingi zimejengwa na karibu watoto wanaostahili kwenda shule wanafanya hivyo.

Sasa watoto wanasoma katika shule za serikali bila kudaiwa karo; miundombinu imeboreshwa na inaendelea kuboreshwa zaidi hasa wakati huu wa Serikali Awamu ya Tano; hali ya upatikanaji majisafi inazidi kuboreshwa na huduma za umeme sasa mpaka vijijini.

Ni mengi ambayo yamefanyika katika kipindi cha miaka 58 ya uhuru na sasa tutarajie makubwa zaidi kupitia Sera ya Uchumi wa Viwanda na Uwekezaji ya Serikali iliyo madarakani.

Tanzania kufikia kipato cha kati ifikapo 2025 ni jambo linalowezekana, kikubwa ni amani na uzima tele. Na kupitia afya njema na nguvukazi tuliyonayo na kila mtu akifanya kazi kwa bidii, tukiongozwa na kaulimbiu: "Hapa Kazi Tu" tutaweza kufanikisha malengo yetu. Mwenyezi Mungu ibariki Tanzania na watu wake.

***Mwandishi anapatikana kupitia***

***P.O. Box 79011, Dar-es-Salaam, Tanzania, fkilahama@gmail.com; +255756007400; +255714250050;***

# Uamuzi wa CCM sare zake ni sawa kabisa

• Wanachama wenye mapenzi na chama hicho watazinunua tu

**Na Sabato Kasika**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimetangaza utaratibu mpya kuhusu sare zake, kwamba katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, hazitatolewa bure kama zamani, badala yake kila mwanachama atajinunulia.

Inaelezwa kuwa uamuzi huo unalenga kupunguza matumizi kwa kuwa chama hicho tawala, kimejipanga kutumia gharama ndogo katika uchaguzi huo wa rais, wabunge na madiwani.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bshiru Ally, hayo ni maelekezo ya Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Dk. John Magufuli, kwamba utaratibu huo ni mpya tofauti na chaguzi zilizopita.

"Matarajio yangu uchaguzi ujao tutatumia pesa kidogo, na tumeshasema hatutanunua tisheti za kuwagawia wanachama wakati wa uchaguzi," Dk. Bashiru anakaririwa na vyombo vya habari akisema.

Anasema, kila uchaguzi mkuu, CCM ilikuwa ikitoa sare nyingi za bure kwa wanachama na mashabiki wake, lakini sasa hilo halipo tena, badala yake kila mwanachama atatakiwa kujinunulia mwenyewe.

Uamuzi huo ninauona kama kipimo kwa wanachama na mashabiki wa chama hicho kuonyesha ni jinsi gani wanakipenda chama chao na wanaweza kutoa fedha zao kununua sare badala ya kusubiri kupewa bure.

Wale ambao wana mapenzi ya dhati, ni lazima watatoa fedha zao kununua sare hizo, lakini wanaoshabikia tu wanaweza kukwepa gharama hizo, ambazo kimsingi zinalenga kutunisha mfuko wa chama.

Kuandaa sare kwa gharama kubwa ya fedha na kisha kuzigawa bure ni hasara, hivyo hatua ya kuamua kuziuza inalenga kupunguzia chama hicho matumizi makubwa yasiyo ya lazima.



Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally. **PICHA: MTANDAO**

### CCM MPYA

Kwa sasa kuna mabadiliko makubwa ndani CCM, ambapo wanachama wanaweza kuvaa sare na kutembea nazo mitaani bila kuzomewa kama ambavyo ilijitokeza miaka ya nyuma.

Hii inatokana na chama kurudishwa kwa wanachama na kuondoa aina zote za kero zikiwamo za rushwa ambayo ilichangia kukidhoofisha na kusababisha baadhi ya watu kukidharau.

Matajiri ndio walikuwa wakituhumiwa kukihodhi huku wanachama wakiachwa pembeni kana kwamba hawana haki na chama hicho, lakini sasa kimerudi kuwa cha wakulima na wafanyakazi.

Kwa hiyo zile alama zake mbili za jembe na nyundo sasa zimerejea kwenye lengo lake halisi la Chama Cha Mapinduzi, ambalo kuwa chama cha wakulima na wafanyakazi.

Vitu vingine vya msingi, ambavyo CCM inavisimamia ni umoja na mshikamano miongoni mwa Watanzania, utu wema na kuwajali wanyonge, ambao ndio wengi katika nchi hii.

> Kama chama kitafumbia macho rushwa, itafika wakati nafasi za uongozi zitatangazwa kwa mtindo wa zabuni. Mwenye pesa nyingi ndiye atakayeshinda zabuni ya uongozi.

Hizo zote ni juhudi za Rais John Magufuli, ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Taifa, aliyerejesha imani ya Watanzania kwa chama hicho, ambacho siku za nyuma kilianza kudharaulika.

Uamuzi wake wa kuikarabati CCM na kuwa mpya, umesaidia kuondoa kero mbalimbali za wanachama hali ambayo imeongeza imani kwa wanachama, ambao huenda walitamani kukihama.

Kwa jinsi kilivyojiimarisha upya, hata uamuzi uliochukuliwa wa kutogawa sare bure hauwezi kuumiza wanachama wa kweli, na badala yake watazinunua, ili kusaidia kutunisha mfuko wa chama.

### ILIVYOKUWA

Mwenyekiti mstaafu wa CCM Taifa na Rais wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete, katika uongozi wake, aliwahi kukemea rushwa ndani ya chama hicho na 'kutabiri' kwamba ikiendelea kitaanguka.

Kutokana na hali hiyo, aliamua kumpa makamu wa mwenyekiti wa CCM, mzee Philip Mangula, jukumu la kushughulikia viongozi wa CCM wanaokula rushwa.

Hiyo ilikuwa ni mwaka 2013 wakati akifunga mafunzo maalum ya siku nne kwa makatibu wa mikoa na wenyeviti wa wilaya wa chama hicho nchini na kuwataka watendaji kuacha tabia ya rushwa.

Katika utabiri wake, Dk. Kikwete akasema, iwapo CCM haitakomesha rushwa itanusurika, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, na kama itanusurika, basi mwaka huu haitapita kwenye uchaguzi mkuu.

Rushwa iliyokuwa ndani ya CCM iliwatisha hata makada wake na waliona hatari ya chama kuwakumbatia baadhi ya wenye pesa wanaotuhumiwa kwa rushwa na kugeuza rushwa kama mfumo wa kupata uongozi katika chama.

Wengine walifikia kuonekana wao ni zaidi ya chama na walisikilizwa kwa lolote wanaloamua, hali ambayo ilichangia kukidhoofisha na kuchukiwa na baadhi ya wanachama wapenda haki.

Rushwa hiyo ndiyo iliyomfanya Katibu Mkuu mstaafu wa CCM, ambaye sasa ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Philip Mangula afunguke mambo mazito baada ya kukumbana nayo.

"Kama chama kitafumbia macho rushwa, itafika wakati nafasi za uongozi zitatangazwa kwa mtindo wa zabuni. Mwenye pesa nyingi ndiye atakayeshinda zabuni ya uongozi," alisema Mangula.

Alikumbana na hali hiyo wakati akiwania nafasi ya Uenyekiti wa CCM Mkoa wa Iringa, lakini akajikuta akikumbana na vigingi hivyo vya rushwa ambavyo vilimwangusha.

Hata hivyo, mwenyekiti wa sasa wa CCM taifa, aliliona hilo mapema na kulishughulikia, angalau tatizo hilo la rushwa ndani ya CCM limepungua kama siyo kumalizika kabisa.

Uamuzi wake unakwenda kwa kuzingatia ahadi za mwanachama, ambazo baadhi yake na hasa ya nne, ambayo inakemea rushwa, kwani inatambua kuwa rushwa ni adui wa haki.

Kutokana na hatua hizo za kupambana na rushwa ndani ya CCM, sasa chama kimeonekana kuzaliwa upya na kuongeza imani kwa wanachama wake, hivyo inawezekana kikawa na nafasi nzuri katika uchaguzi ujao.

Heshima ambayo CCM imejenga upya, inakifanya chama hicho kuwa na ujasiri wa kuamua kama ambavyo kimesema kwamba sare zake sasa zitauzwa, hakuna mwanachama kupewa bure.

Kwa vyovyote mwenye mapenzi na chama ni lazima atanunua tu ili kukitangaza kupitia sare hizo, ambazo kimsingi nazo zina mchango, katika kuhamasisha na kuingiza wanachama wapya ndani ya chama.

UCHAGUZI MKUU 2022:

# Wanasiasa 'waivamia' Magharibi ya Kenya

• Mudavadi, Wetangula waendelea kumtesa Odinga

INATOKA UK.13

wa 2022, Raila Odinga na William Ruto, zimejielekeza Magharibi mwa Kenya kutafuta uungwaji mkono.

Odinga ni kiongozi mwandamizi katika Chama cha Orange for Democratic Movement (ODM), wakati Ruto ni Makamu wa Rais wa Kenya. Wawili hao walikuwa pamoja katika Uchaguzi Mkuu wa 2007 uliozua ghasia zilizomfikisha Ruto na wenzake watano akiwamo Uhuru Kenyatta, kushtakiwa kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai (ICC) huko The Hague, Uholanzi.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wa Magharibi mwa Kenya wanaopatikana watu wa jamii ya Waluhya, Philip Masinde, pia amejiunga na Mudavadi na Wetangula kujitenga na mpango huo unaohusisha kufanya mkutano mkubwa na pamoja na kutoa matamko yenye mwelekeo wa kisiasa.

Kwa mujibu wa gazeti la The Standard la Kenya, Gavana Wycliffe Oparanya wa kaunti ya Kakamega, anayetokana na ODM, alitangaza Desemba 26, mwaka jana kuwa jamii ya Waluhya na wananchi wengine wa ukanda huo, watashiriki mkutano mkubwa wa hadhara.

Mkutano huo utakaofanyika Januari 18, mwaka huu kwenye uwanja wa Bukhungu II uliopo katika kaunti hiyo, unatajwa kuwa sehemu ya mkakati wa kisiasa kutafuta kuungwa mkono kuelekea Uchaguzi Mkuu ujao nchini humo.

Kwa mujibu wa Oparanya, tukio hilo litakuwa fursa kwa viongozi wa kisiasa kuweka mkakati na kukubaliana namna ya kusonga mbele kisiasa.

Gavana Oparanya alikutana na Odinga kijijini kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi nchini humo, Francis Atwoli. Atwoli ni mmoja wa Wakenya wanaotambulika kwa kuwa na ushawishi mkubwa kwa watu.

Mkutano huo wa Kakamega unazidisha hisia zilizopo kuhusu mpango wa Odinga kuwania urais kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2022 na kumfanya Oparanya kuwa msemaji kwa watu wa ukanda huo.



Musalia Mudavadi (kushoto) na mwenzake Moses Wetang'ula. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### WETANGULA AHOFIA KUGAWANYIKA

Kwa upande wake, Wetang'ula ambaye pia ni Seneta wa Bungoma, anakosoa kufanyika kwa mkutano huo kwa madai kuwa "utawachanganya na kuwagawa watu wa umoja wa Mulembe".

Seneta huyo anasema Atwoli hana mamlaka ya 'Msemaji wa Waluhya' na kuwaitisha watu kwenye mkutano.

"Anachokifanya ni kujaribu kuwaleta tena watu waliopitwa na wakati. Nimekutana na Mudavadi na tumekubaliana kuiunganisha jamii yetu (Waluhya) na ukanda wote wa Magharibi mwa Kenya," anasema.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wa Magharibi mwa Kenya, Masinde amesema hakuna mazungumzo yaliyofanyika kuhusu mkutano wa Bukhungu II.

"Tulikuwa huko na tuliondoka kabla ya Odinga na ujumbe wake kuwasili. Majadiliano yetu yalihusu ripoti ya mpango wa kuwapatanisha Wakenya (BBI) kwa sababu tulijulishwa na Oparanya na Atwoli kuwa Rais Uhuru Kenyatta na Raila watatutembelea mwezi Januari," anasema.

> Mudavadi ana uwezo kutatua matatizo ya kiuchumi tunayokabiliana nayo nchini mwetu...anaweza kushughulikia ugumu wa ki-fedha unaotukabili.

### WAMALWA AMTABIRIA MEMA MUDAVADI

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ukaguzi, Eugene Wamalwa, anaamini uwezekano wa kufanyika makubaliano ya kisiasa kati ya Rais Kenyatta na Mudavadi.

Akizungumza kwenye tamasha la utamaduni wa Wamaragoli uliofanyika kwenye uwanja wa manispaa ya Mbale, Wamalwa akasema ziara ya Rais Kenyatta kwenda kufungua kambi ya Modika iliyopo Garissa akifuatana na Mudavadi, inaweza kutoa taswira ya mwelekeo wa jambo ambalo Wakenya wanaliratajia kwa siku za baadaye.

"Rais ndiye mwenye mpira mikononi mwake, huenda anaweza kuutupa kwa Mudavadi,"



Kiongozi wa upinzani Kenya, Raila Odinga.

anasema Wamalwa ambaye pia anawahimiza wanasiasa wa ukanda wa Magharibi mwa Kenya kuwa umoja thabiti na kulenga masuala yenye msingi.

Anasema lazima wanasiasa hao wachagize ukuaji wa eneo la ukanda huo na kuwafikia rafiki zao. Pia kuwa na nguvu zaidi za kisiasa, kufika na kujenga ushawishi kwenye maeneo mengine nchini humo ili kufikia lengo la kuchukua nafasi za juu (kiutawala).

Wamalwa anasema mwanasiasa kinara wa ODM, Odinga na mwenzake wa chama cha Wiper, Kalonzo Musyoka, walijipanga na kufikia nafasi za karibu sana na urais, kwa sababu walijua wanachokitaka.

"Wawili hao, Raila na Kalonzo siyo wajinga, wameshikana mkono na Rais kwa sababu wanajua maana ya kufanya kazi na serikali. Mudavadi kama anataka kufikia huko atambue kwamba ukanda wa Magharibi mwa Kenya pekee hauwezi kumfanya awe Rais," anasema.

Wamalwa anasema Mudavadi anapaswa 'kupasua anga' nje ya chama chake cha ANC na kutafuta watu wengi zaidi wa kumuunga mkono kwenye ukanda huo na Kenya kwa ujumla wake.

Wabunge wa Lugari, Ayub Savula, Titus Khamala (Lurambi) na Omboko Milemba (Emuhaya) wametangaza azma ya 'kumpigia debe' Mudavadi kwenye 'kona zote za Kenya.

Savula anasema, "Mudavadi ana uwezo kutatua matatizo ya kiuchumi tunayokabiliana nayo nchini mwetu...anaweza kushughulikia ugumu wa ki-fedha unaotukabili."

### MUDAVADI NA RUTO

Naibu Kiongozi huyo wa ANC anaelezea uwezekano mkubwa wa Mudavadi kufanya kazi kwa pamoja na Naibu Rais wa Kenya anayetarajiwa kuwania urais 2022, William Ruto.

Wabunge wengine waliokuwapo Mbale na majimbo yao kwenye mabano ni John Bunyasi (Nambale), Ernest Ogesi (Vihiga), Alfred Agoi, (Sabatia) na mwakilishi wa wanawake kaunti ya Vihiga, Beatrice Adagala.

### ODINGA AWEKA KAMBI

Kwa upande wake, Odinga na sehemu ya wabunge kutoka ukanda huo walikutana hivi karibuni nyumbani kwa Atwoli huko Kakamega.

Ingawa taarifa zaidi kuhusu masuala waliyojadiliana hazikuwekwa wazi, Atwoli na Oparanya walijitokeza na kutangaza kuhusu kufanyika kwa mkutano wa Januari 18, mwaka huu.

Wengine waliohudhuria mkutano huo ni Seneta wa Kakamega, Cleophas Malala, mwakilishi wa wanawake, Elsie Muhanda, Katibu Mkuu wa ODM, Edwin Sifuna na mbunge wa kuteuliwa, Wilson Sossion. Kwenye mkutano huo, Raila alifuatana na mke wake, Ida Odinga.

> Rais ndiye mwenye mpira mikononi mwake, huenda anaweza kuutupa kwa Mudavadi.

Wakati akitangaza mkutano huo wa Januari 18, mwaka huu, Oparanya akasema utawashirikisha viongozi wote kutoka kaunti nne zilizopo kwenye ukanda huo ambazo ni Kakamega, Vihiga, Busia na Bungoma.

Akasema wakati wa mkutano huo, watajielekeza zaidi katika kutanuliwa nafasi za utawala wa Kenya kwa kuanzisha nafasi ya Waziri Mkuu na nafasi mbili za Naibu Waziri Mkuu.

Naye Atwoli, anasema mkutano huo utasaidia kuwabaini watu watakaowania nafasi mbalimbali za uongozi kwenye Uchaguzi Mkuu ujao.

Kuhusu kugawanyika kwa jamii ya Waluhya, Atwoli anasema, "ni mtazamo unaoletwa na vyombo vya habari, lakini Waluhya tuna umoja kwa asilimia 100 na tutathibitisha hilo Januari 18."

## Wanajeshi 27 wahukumiwa kifo mauaji ya mwandamaji



Waandamanaji Sudan wakishangilia wakati hukumu ikitolewa. **PICHA: MTANDAO**

MAHAKAMA moja ya Sudan imewahukumu adhabu ya kifo maofisa 27 wa vikosi vya usalama kwa kumtesa na kumuua mwandamanaji mmoja wakati wa maandamano ya kumpinga aliyekuwa kiongozi wa muda mrefu Omar al-Bashir.

Kifo cha mwandamanaji Ahmed al-Khair, aliyekuwa mwalimu wa shule, wakati alipokuwa kizuizini mwezi Februari kilikuwa suala muhimu na ishara katika maandamano hayo ambayo hatimaye yalisababisha jeshi kumwondoa al-Bashir madarakani.

Hukumu hizo zinazoweza kukatiwa rufani, ndizo za kwanza kuhusiana na mauaji ya waandamanaji katika mapinduzi hayo.

Katika kesi dhidi ya vikosi vya usalama iliwasilishwa katika Mahakama ya Omdurman, mji ndugu wa Khartoum, ambako waandamanaji kadhaa walikusanyika nje ya mahakama, wakidai haki kwa ajili ya al-Khair.

Al-Khair alikamatwa Januari 31 katika mkoa wa Mashariki wa Kassala na akaripotiwa kufariki siku mbili baadaye. Mwili wake ulipelekwa kwenye hospitali ya eneo hilo ambako familia yake ilisema ulikuwa na michubuko. Kwa wakati huo, polisi ilikanusha kufanya kosa lolote ikisema kifo chake kilitokana na ugonjwa, bila kutoa maelezo yoyote.

Mahakama hata hivyo imesema kuwa mwalimu huyo alipigwa na kuteswa wakati akiwa jela. Watu 27 waliohukumiwa ni polisi waliokuwa kwenye gereza ambalo al-Khair alizuiliwa au majasusi wa eneo hilo.

Aidha, Mahakama mjini Khartoum mwezi uliopita ilimkuta al-Bashir na hatia ya makosa ya utakatishaji fedha na rushwa, na kumhukumu kifungo cha miaka miwili kwenye gereza lenye ulinzi mdogo.

Amnesty International na makundi mengine ya haki za binadamu yametoa wito kwa serikali mpya kuviwajibisha vikosi vya usalama kwa kuwaua watu wakati vilipofanya juhudi za kuyavunja maandamano dhidi ya utawala wa kijeshi, na hasa wale waliohusika na ukandamizaji mbaya dhidi ya waandamanaji waliokuwa wamekita kambi nje ya makao makuu ya jeshi mjini Khartoum Juni mwaka juzi.

Tangu Desemba mwaka juzi, karibu waandamanaji 200 wameuawa nchini Sudan. Sudan iko chini ya shinikizo kubwa la kimataifa na kikanda kufanya mageuzi. Huku uchumi ukiwa ukingoni, kuporomoka, serikali mpya ya inafanya juhudi kutaka Sudan iondolewe kwenye orodha ya wabaya wa Marekani ya mataifa yanayofadhili ugaidi ili iweze kupokea msaada wa kigeni unaohitajika kwa kiasi kikubwa. **DW**

TUJIKUMBUSHE

# Oscar Salathiel Kambona

- Akiwa Waziri wa Ulinzi, alifanikiwa kuzima maasi ya 1964
- Alifariki Julai 1997 Uingereza, mwili ukarejeshwa na kuzikwa nchini



Oscar Kambona enzi za uhai wake. **PICHA: MAKTABA**

OSCAR Salathiel Kambona, alikuwa Waziri wa kwanza wa Mambo ya Nje wa Tanganyika, na mmojawapo wa viongozi maarufu nchini mwanzoni mwa utawala wa Awamu ya Kwanza wa Rais, Mwalimu Julius Nyerere.

Alizaliwa Agosti 13, 1928, katika kijiji cha Kwambe karibu na Mbamba Bay, kandokando ya Ziwa Nyasa, wilayani Mbinga, jirani na mji wa Songea, Kusini mwa Tanganyika kwa wakati huo.

### ALIFARIKI UINGEREZA, JULAI 1997

Alizaliwa katika familia ya kidini, baba yake David Kambona, akiwa mchungaji wa madhehebu ya Anglikana.

Baba yake alikuwa miongoni mwa wachungaji wa kwanza Waafrika kulitumikia kanisa la Anglikana, wakati nchi ikiitwa Tanganyika.

Kambona alipata masomo ya elimu ya msingi, kijijini kwao akisoma chini ya mwembe. Mti huo bado upo hadi leo.

Alifundishwa na wazazi wake, pamoja na mjomba wake ambao walikuwa walimu kwa wakati huo.

Baadaye alipelekwa Shule ya kati ya St Barnabas Middle School, iliyokuwa Liuli, Kusini mwa Tanganyika, si mbali na nyumbani kwao.

Aliendelea na masomo katika Shule ya Sekondari ya Alliance, iliyokuwa mjini Dodoma.

Kasisi Mwingereza wa kanisa la Anglikana, ndiye aliyelipa gharama za masomo kwa ajili ya Kambona, kutokana na baba yake kutomudu gharama za karo ya shule.

Karo ya shule ilikuwa, paundi 30 kwa mwaka.

Inasemekana Kambona alimfurahisha Kasisi huyo kutokana na uwezo wa kusali sala ya Bwana, kwa lugha ya Kiingereza kwa ufasaha.

Baada ya masomo Dodoma, aliendelea na masomo mjini Tabora, kwenye Shule ya Wavulana (Tabora Boys Senior Government School), ambako alionana kwa mara ya kwanza na Mwalimu Nyerere, ambaye alikuwa akifundisha katika shule ya St. Mary's, kwa wakati huo, iliyokuwa ikimilikiwa na Kanisa Katoliki, mjini Tabora.

### KAZI ZA SIASA

Aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa chama cha Tanganyika African National Union (TANU), wakati wa harakati za kutafuta Uhuru wa Tanganyika, na alifanya kazi kwa karibu na Mwalimu Nyerere, ambaye alikuwa Rais wa TANU, chama kilicholeta Uhuru wa Tanganyika.

Uhuru wa Tanganyika ulipatikana Desemba 09, 1961 kutoka kwa Mwingereza.

Viongozi hao wawili walikuwa maarufu, wakiwa mstari wa mbele katika mchakato wa kuiandaa Tanganyika, kujipatia uhuru wake kuanzia miaka ya 1950.

Kambona alikuwa kiongozi mwenye kipaji kikubwa na alikubalika na viongozi wengi wa vyama vya ukombozi wa Afrika, waliokuwa Dar es Salaam. Walimpa heshima kubwa akimfuatia Nyerere, baada ya uhuru.

Ni kiongozi aliyeng'ara miongoni mwa kundi la wanasiasa wa Tanganyika (baadaye Tanzania), na iliaminika kuwa angeweza kurithi nafasi ya u-rais wa nchi, endapo Nyerere angeamua kutogombea au kwa sababu yoyote ile.

> Ni rahisi zaidi kutumia mfananisho wa gari, liwe barabarani na siyo limewekwa pembeni vile hatuna kazi na 'tuvyama,'

Nafasi ya kuwa karibu na Mwalimu aliipata baada ya kuteuliwa kuwa Waziri wa Ulinzi.

Aliwatuliza wanajeshi walipotaka kuiangusha serikali, miaka michache, baada ya uhuru kwenye maasi ya Januari 1964.

Katika maasi hayo Rais Nyerere na Makamu wa zamani wa Rais, Rashid Kawawa, walichukuliwa na watu wa Idara ya Usalama wa Taifa, na kupelekwa kwenye sehemu ya usalama, kwa tahadhari.

Alikuwa Kambona aliyethubutu kwenda kuongea na wanajeshi, na kukubaliana nao.

Madai ya wanajeshi yalikuwa nyongeza ya mishahara na walitaka pia maofisa wazungu waondoke, na nafasi zao zichukuliwe na maofisa Waafrika.

Kulikuwa na hofu na wasiwasi kuwa baadhi ya viongozi serikalini na wale wa wafanyakazi, walihusika kuwashawishi kisiri wanajeshi, wafanye maasi ya kuipindua serikali ya Mwalimu Nyerere.

Ilidhihirika kuwa Kambona hakuwa mmoja kati ya waliowashawishi wanajeshi kuasi, kwani kama angekuwa mmojawao, basi angetumia muda huo kujitangazia madaraka ya kuiongoza nchi.

Baada ya Nyerere kutoka mafichoni, alimshukuru Kambona, kwa kudhibiti hali ya mambo.

Kimsingi ni Kambona aliyemshawishi Nyerere kuomba misaada ya kijeshi, kutoka Uingereza, ili isaidie kuzima maasi hayo.

Viongozi hao walikuwa marafiki wa karibu katika mambo ya kisiasa, na baadaye ya kibinafsi kutoka wakati wa harakati za kutafuta uhuru wa Tanganyika.

Ndio waliokuwa vinara na wasemaji wakuu kwenye michakato ya kuelekea uhuru.

Hata Kambona alipomwoa aliyekuwa Miss Tanganyika wakati huo, katika kanisa moja jijini London, nchini Uingereza, Nyerere alikuwa mpambe wake.

### WATOFAUTIANA

Viongozi hao walianza kutofautiana katika baadhi ya mambo miaka michache baada ya uhuru.

Kwanza ilikuwa mwaka 1964, wakati wa maasi ya wanajeshi, na baadaye mwaka 1965, pale Tanzania ilipoamua kufuata mfumo wa siasa ya chama kimoja.

Akiwa mbunge, Kambona aliafiki mpango wa kuwa na serikali moja kwa shingo upande.

Hakukubaliana na mabadiliko hayo kwa kuona hapakuwa na namna ya kubadilisha serikali kwa kufuata mfumo wa kikatiba, katika nchi inayoongozwa kwa mfumo wa chama kimoja.

Aliona kuwa, hapakuwa na kinga ya kikatiba ambayo ingezuia nchi kuongozwa kidikteta.

Eneo lingine walilotofautiana na Mwalimu Nyerere, lilijitokeza Februari 1967, wakati Tanzania, iliporidhia kufuata misingi ya Azimio la Arusha, azimio lililoweka mabadiliko katika misingi ya kiuchumi na kisiasa kwa ajili ya kuibadilisha Tanzania kuwa taifa la kijamaa.

Kambona hakukubaliana na misingi ya mabadiliko hayo yaliyoainishwa kwenye Azimio la Arusha, na alitoa ushauri kuwa kwanza, ufanywe utafiti wa kisayansi wa kuona kama sera za misingi ya Azimio la Arusha, zitasaidia umma wote wa Watanzania.

Sera za Ujamaa zilijikita zaidi katika uanzishwaji wa vijiji vya Ujamaa, ambavyo kwa kiwango zilifanana na zile zilizoanzishwa nchini Israel za Kibbutz au za Communo.

Katika sera hizo, wananchi walitakiwa waishi na kufanya kazi pamoja kwa faida ya wote, na iwe rahisi kwa serikali kuwapa mahitaji muhimu kama ya maji, matibabu, elimu na mengineyo.

Kambona alitoa hoja kuwa, ilikuwa muhimu kwanza kuwashawishi wananchi kuwa maisha ya kuishi pamoja katika vijiji vya ujamaa yalikuwa na faida, kuliko walivyokuwa wakiishi katika mtawanyiko kwa kipindi hicho.

Alishauri kuwa hilo lingewezekana baada ya kuanzisha vijiji vya ujamaa vya mfano katika maeneo mbalimbali nchini, ili kuwapa ushawishi wananchi kuwa maisha ndani ya vijiji vya Ujamaa yangekuwa na faida kubwa, baada ya wao kujionea ustawi ambao ungejitokeza.

Majadiliano, mara nyingi yalifanywa kwa siri na baadhi ya wajumbe wa chama tawala cha TANU, wakati wanachama walio wengi walikuwa wakijadili Azimio la Arusha katika mikutano mbalimbali.

Majadiliano mazito yalikuwa kati ya kundi la Kambona, na lililokuwa kundi la Mwalimu Nyerere, pamoja na Makamu wake, Mzee Kawawa.

# Wenye sifa tutumie fursa hii kujiandikisha kwenye Daftari



Ofisa wa NEC, Meshack Mgovano, akitoa elimu ya mpigakura kuhusu uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura iliyofanyika katika Shule ya Sekondari Mwalimu Nyerere Mjini Tunduma mkoani Songwe. **PICHA: NEC**

**Na Christina Njovu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), inaendelea na uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura, ambalo ni mahsusi kwa ajili ya kuandikisha wapigakura wapya wenye sifa ya kuwamo katika daftari hilo na hatimaye kupiga kura.

Miongoni mwa sifa hizo ni pamoja na kutimiza umri wa miaka 18 na kuendelea ambao hawakuwahi kujiandikisha hapo awali na wale watakaotimiza umri wa miaka 18 ifikapo siku ya uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2020.

Vijana hawa ni wale waliozaliwa mwaka 2002 kuanzia Januari hadi Oktoba, wawe raia wa Tanzania, pia wenye akili timamu.

Zoezi linalokwenda sambamba na utoaji wa elimu ya mpigakura kwa njia ya gari la matangazo, ikiwa ni moja ya michakato muhimu kuelekea uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani utakaofanyika mwaka ujao wa 2020.

Utoaji wa elimu ya mpigakura unaofanyika hivi sasa ni kwa ajili ya uboreshaji wa daftari hilo unaolenga kuelimisha, kufahamisha na kuwajulisha wananchi juu ya sifa za mtu kujiandikisha kuwa mpigakura ili kupata kadi ya kupigia kura.

Kadi ambayo ndio atakayoitumia kupiga kura siku ya uchaguzi mkuu ujayo na chaguzi ndogo zitakazojitokeza.

Uboreshaji huo ambao unafanyika kikanda unaambatana na utoaji wa elimu ya mpigakura kulingana na mwenendo mzima wa zoezi lenyewe.

> Raia wa Tanzania, umri wa miaka 18 na yule atakayetimiza umri huo ifikapo siku ya uchaguzi mkuu, lakini kuwa na akili timamu.

Gari la matangazo linapita katika baadhi ya mikoa, miji na viunga vyake zikiwamo shule za sekondari ambako ndiko kuna wapigakura wapya kwa lengo la kutoa elimu ya mpigakura juu ya umuhimu wa kujiandikisha.

Kwa kutumia njia hiyo ya utoaji wa elimu ya mpigakura kwa njia ya gari la matangazo, Tume imeweza kuwafikia wananchi wengi, makundi mbalimbali yakiwamo yaliyo maalumu na hasa vijana ambao ni wapigakura wapya katika maeneo ya shule za sekondari, maeneo yenye mikusanyiko ya watu yakiwamo masoko, stendi na magulio.

Moja ya malengo ya NEC ni kuwafikia wapigakura wapya ambao wengi wao ni vijana waliotimiza umri wa miaka 18 ambayo ni miongoni mwa sifa kuu zinazomwezesha mtu kuwapigia kura wagombea.

Sifa zingine kama zilivyoelezwa hapo juu ni kuwa raia wa Tanzania, lakini mwenye akili timamu.

### KUKOSA SIFA

Sambamba na hilo, mtu atakosa sifa za kuandikishwa katika daftari hilo akiwa ni raia wa nchi nyingine, au amethibitika na daktari kuwa hana akili timamu.

Vilevile kama yuko kizuizini kutokana na uhalifu kwa maana ya kuwa amefungwa jela, akiwa amehukumiwa adhabu ya kifo, au mwenye kutumikia adhabu ya kifungo kinachozidi miezi au sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge.

Katika shule mbalimbali za sekondari ambapo NEC kwa kutumia gari la matangazo limeweza kupita, wanafunzi waliweza kupata elimu sahihi ambayo iliwaimarisha katika somo la uraia na waliweza kuuliza maswali na kujibiwa papo kwa papo na hatimaye kukuza uelewa wao.

Mmoja wa walimu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mpanda (Mpanda Girls), ameishukuru NEC kwa kuweza kuchagua shule yake kuwa moja ya shule ambayo imetembelewa na Tume na kupatiwa elimu ya mpigakura na kwamba elimu hiyo ni miongoni mwa elimu inayotolewa katika somo la General Study (GS).

Baadhi ya wanafunzi katika shule zilizopatiwa elimu hiyo na Tume wanaeleza kuwa elimu hiyo imewasaidia kujua sifa za mtu kuandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura, sambamba na sifa za kuwa mpigakura.

Sifa hizo ni pamoja na kuwa "raia wa Tanzania, umri wa miaka 18 na yule atakayetimiza umri huo ifikapo siku ya uchaguzi mkuu, lakini kuwa na akili timamu" anasema Agnes Kilangi wa Shule ya Sekondari ya Mtakatifu Maurusi, iliyoko Sumbawanga, mkoani Rukwa.

Elimu ya mpigakura inayotolewa na Tume kwa njia ya gari la matangazo imewezesha wananchi kupata uelewa wa pamoja kuhusu masuala ya uchaguzi, ambapo wamekuwa wakiuliza maswali mbalimbali na kujibiwa na maofisa wa tume.

Aidha, wananchi wamepatiwa pia vipeperushi vinavyowasaidia kuelewa zaidi mchakato mzima wa uchaguzi.

Mikoa ambayo gari la tume limepita ni pamoja na Mkoa wa Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Simiyu katika viwanja vya Nyakabindi wakati wa Maonyesho ya Nanenane, Mara, Geita, Mwanza, Bukoba, Tabora, Katavi, Rukwa, Mbeya, Dodoma na hivi sasa lipo mkoani Iringa likiendelea na shughuli ya utoaji wa elimu ya mpigakura kupitia maofisa wa NEC.

Gari la matangazo liliweza kupita katika mikoa hiyo na kutoa elimu ya mpigakura katika maeneo mbalimbali yenye mkusanyiko wa watu, sambamba na kwenye maonyesho ya NaneNane yaliyofanyika kitaifa mkoani Simiyu katika viwanja vya Nyakabindi.

Lakini stendi na katika maeneo ya masoko na kutoa fursa kwa wananchi kuuliza maswali na kujibiwa papo kwa papo.

Sambamba na utoaji wa elimu ya mpigakura kwa njia ya gari la matangazo kuwafikia wapigakura, elimu hiyo inatolewa pia kwa njia ya redio za kijamii zinazopatikana katika mikoa yote nchini, ambapo maofisa wa NEC wamekuwa wakizungumza na wananchi na kujibu maswali sambamba na kutoa ufafanuzi katika masuala mbalimbali ya uboreshaji wa daftari na uchaguzi kwa ujumla.

Hivyo wananchi tutumie fursa hii adhimu tunapoliona gari la matangazo la Tume, tusogee na tutege sikio kusikiliza elimu inayotolewa na NEC.

Kadi Yako, Kura Yako, Nenda Ukajiandikishe.

# Ajira za watoto zinakiuka haki zao, zipigwe vita



Mama akiwa katika machimbo na mtoto ambaye angepaswa kuwa shuleni. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Reubeni Lumbagala**

AJIRA ni shughuli yeyote halali anayoifanya mtu ili kujiingizia kipato na hatimaye kuweza kumudu kuendesha maisha yake.

Mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18, yaani kuanzia umri 0 hadi 17. Kwa hiyo, ajira ya mtoto ni hali ya mtu chini ya miaka 18 kufanyishwa kazi za ujira maalum.

Kimsingi, mtu anayepaswa kufanya kazi ni yule mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea kwani mwenye aina hiyo ya umri huchukuliwa kuwa ni mtu mzima, mwenye uelewa na uwezo wa kumudu kufanya kazi na kuwa na uwezo wa kudai malipo yanayowiana na kazi anayoifanya. Mtoto hapaswi kufanyishwa kazi kwa sababu umri wake hauruhusu.

Na ikumbukwe kuwa, kazi ya mtoto ni kwenda shule kusoma na kupata maarifa ya kumwezesha kuja kufanya kazi baadaye atakapofikisha umri sahihi kisheria.

Haki ya kupata elimu ni haki ya msingi ya mtoto. Haki hii haipaswi kuvunjwa kwa sababu nyingine yeyote kutokana na ukweli kwamba elimu kwa mtoto ni maandalizi ya kutengeneza mustakabali wake mwema wa maisha yake ya sasa na ya baadaye.

Hivyo, mtoto anaposhirikishwa katika ajira ni dhahiri haki zake, ikiwamo ya kupata elimu inavunjwa kwa sababu muda ambao mtoto atapaswa kuwa shuleni, atakuwa katika maeneo mengine ya shughuli kama sokoni, vituo vya mabasi, migodini, baharini nk.

Pamoja na changamoto ya umaskini kwa baadhi ya kaya, haki ya mtoto ya kupata elimu inapaswa kubaki palepale.

Baadhi ya kaya huamua kuwatumia watoto wao kufanya shughuli za kiuchumi kama vile kuuza maandazi, peremende, ndizi, keki, ili kuweza kupata kipato.

> “Serikali imeamua kutekeleza ahadi yake ya kutoa elimu bila malipo kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne ili kuwapatia nafasi kila mtoto kupata elimu.



Watoto wenye umri mdogo wakijishughulisha na ajira mbali mbali ili kuweza kujikimu kimaisha huku wakikosa hudumu muhimu ya elimu.

Ni lazima jamii itambue kuwa ipo faida kubwa ya kupeleka watoto wao shule kulinganisha na kuwatumikisha kwenye shughuli za kiuchumi.

Suala la kusoma linaweza kuonekana kama jambo lisilo na faida kwa baadhi ya jamii kutokana na matunda ya kusoma kuchukua muda hadi kuja kuonekana.

Hata hivyo, ukweli utabaki kuwa uwekezaji unaolipa na wenye tija ni ule wa wazazi na walezi kupeleka watoto wao shule ili kuelimika.

Elimu ni uwekezaji pekee ambao hauna kufilisika wala kupata hasara kwani maarifa, ujuzi na stadi zinazoingia katika ubongo wa msomaji hubaki kichwani daima.

Jamii ijifunze kwa familia ambazo ziliamua kupeleka watoto shule (watoto wa kiume na wa kike) na matunda ambayo kwa sasa wanayapata kupitia watoto wao.

Wazazi na walezi wazitumie raslimali walizonazo katika kuwasomesha watoto wao ili baadaye wanufaike na matunda ya elimu watakayopata watoto wao.

Mzazi anaweza kudhani kumfanya mtoto wake mchungaji wa mifugo kama mbuzi, ng'ombe, kondoo ni faida kwake lakini mifugo hiyo inaweza kufa na familia hiyo kuingia katika lindi la umaskini huku mtoto huyo akiwa mjinga kwa kutopata elimu.

Mzazi anaweza kupeleka mtoto wake kuuza peremende, maandazi sokoni ili kupata kipato, lakini kipato hicho kikaendelea kuwafanya wazidi kuwa maskini na mtoto huyo akibaki katika lindi la ujinga na familia nzima kuwa maskini.

Jamii zote yaani wakulima, wafugaji, wavuvi, wawindaji wanapaswa kuelimishwa kuhusiana na umuhimu wa kusomesha watoto wao na kuachana na tamaa ya kupata fedha kwa kuwatumia watoto hao kama njia ya uzalishaji mali, kwani kwa kufanya hivyo ni kosa kisheria na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Serikali imeamua kutekeleza ahadi yake ya kutoa elimu bila malipo kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne ili kuwapatia nafasi kila mtoto kupata elimu.

Kuendeleza kuwatumikisha watoto ni kuikwamisha serikali katika mipango yake ya kupata wasomi wa kutosha katika nchi hii kwa kutoa elimu bila malipo.

Serikali hutumia Sh. bilioni 24 kila mwezi kutekeleza sera ya elimu bila malipo. Fedha hizi ni nyingi na kama si utashi wa serikali wa kutaka kila mtoto kupata elimu, fedha hizo zingeweza kutumika katika matumizi mengine yasiyo ya lazima kama semina, warsha na makongamano mbalimbali.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwa ziarani mkoani Singida aliwaagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi kufanya msako kwenye stendi za mabasi ili kuwabaini watoto wasiokwenda shule.

Waziri Majaliwa alisema “Hatutaraji kuona vijana wadogo wauza biashara kwenye vituo vya mabasi...Mkurugenzi chukua OCD siku moja, nenda kwenye miji yenu midogo, saka watoto wote wanaofanya biashara stendi, watambue wazazi wao, halafu kamata wazazi wao wajieleze ni kwanini wanawaacha watoto wao waende stendi badala ya kwenda shule... tunataka kila mtoto wa Kitanzania aende shule”.

Agizo hili ni kwa viongozi wote nchini katika kuhakikisha kila mtoto anapata elimu na kuachana na ajira za watoto.

Familia na jamii kwa ujumla tushirikiane katika vita hii ya ajira za watoto ili watoto wapate elimu. Sote tuwe na sauti moja kusema “Shule kwanza, ajira baadaye”. Tafakari, chukua hatua.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni, ushauri: (+255) 764 666349.***



# Waanza ujenzi madarasa kidato cha kwanza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kata ya Utengule - Usongwe iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, wameungana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuanza ujenzi wa vyumba tisa vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Usongwe, ili kukabiliana na tatizo uhaba wa vyumba vya madarasa.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Elimu katika Mkoa wa Mbeya, halmashauri hiyo inakabiliwa na uhaba wa vyumba vya madarasa 11 kwa ajili ya wanafunzi 550 waliofaulu mitihani ya darasa la saba na kutakiwa kujiunga na kidato cha kwanza ambao majina yao yamezuiliwa kutangazwa.

Wananchi hao walianza ujenzi huo juzi, ikiwa ni siku moja tangu Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, alipowaagiza wakuu wa mikao yote nchini kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa ili vikamilike mapema na watoto wote wanaotakiwa kuanza kidato cha kwanza waanze kwa pamoja.

Wakizungumza walipokuwa wanachimba msingi wa moja ya vyumba hivyo, walisema wao wameamua kushirikiana na serikali kwa ajili ya manufaa ya watoto wao ambao wanatakiwa waanze masomo.

Juma Athuman alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakitafsiri vibaya agizo la serikali la kufuta michango shuleni kwa kukataa hata kuchangia ujenzi wa miundombinu kitu ambacho sio sahihi.

"Rais Magufuli alichofuta ni ada na michango mingine ambayo haikuwa na maana, lakini kwenye ujenzi wa miundombinu ni lazima tushiriki, sisi tumejitoa kuchangia kwa sababu ni kwa ajili ya maendeleo ya watoto wetu wenyewe," alisema Athuman.

Alisema wanafuata falsafa ya Rais John Magufuli kuwa maendeleo ni lazima, Watanzania wajiletee wenyewe kwa kufanya kazi kwa bidii bila kutegemea wahisani.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Utengule- Usongwe, Daudi Mbembela, alisema katika kata hiyo watoto 400 wamekosa vyumba vya madarasa kwa ajili ya kuanza kidato cha kwanza mwezi huu na kwamba vyumba vinavyohitajika ni tisa.

Alisema kutokana na idadi hiyo ya wanafunzi waliokosa vyumba vya madarasa ndio maana waliamua kuanzisha kampeni ya kujenga vyumba vipya katika shule hiyo, ili kumaliza tatizo hilo kwa asilimia 100.

"Nawaomba wananchi wote wa Mji wa Mbalizi tuungane tukamilishe vyumba hivi kwa wakati na watoto wote waanze masomo, tunaomba mwenye gari, mwenye kuku, mwenye baiskeli na chochote ambacho mtu anaweza akatusaidia alete tutashukuru," alisema Mbembela.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, aliwapongeza wakati wa kata hiyo kwa moyo wao wa kujitolea katika shughuli za maendeleo, na kwamba vyumba walivyoanza kujenga vitapunguza tatizo kwa kiwango kikubwa.

Alisema walimu wa Shule za Msingi katika wilaya hiyo walishafanya wajibu wao wa kufaulisha watoto na kilichobaki kwa sasa ni jukumu la wazazi kuhakikisha watoto wote waliofaulu wanaanza masomo mapema.

"Hii kazi mliyoanza ina changamoto zake, kuna baadhi ya wanasiasa watawakatisha tamaa kwa kuleta maneno ya ajabu, nawashauri endeleeni kupiga kazi bila kujali maneno ya watu," alisema Mwalingo.

Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, ambaye alihudhuria katika shughuli hiyo, alisema atachangia mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa vyumba hivyo.

Alisema mbali na mchango huo, pia atashirikiana na viongozi wa halmashauri hiyo kutafuta magari kwa ajili ya kubeba vifaa vya ujenzi na akawahamasisha wananchi kujitokeza kila wanapoitwa kwenye shughuli za maendeleo.



Askari wa Jeshi la Kujenga Taifa Kitengo cha Uzalishaji (Suma-JKT), Kanda ya Nyanda za Juu, wakisaidia kupakia kwenye gari mabati yaliyotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila kwa ajili ya kukamilisha vyumba vya madarasa katika halmashauri zote za mkoa huo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Ajali barabarani sasa zadhibitiwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IDADI ya watu waliopoteza maisha kutokana na ajali za barabarani kuanzia Januari 2019 zilipungua kwa asilimia 56.5 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2018, hali ambayo inaashiria kuwa ajali hizo zimedhibitiwa kwa kiwango kikubwa.

Hayo yalisemwa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alipokuwa akitoa tathmini ya matukio ya uhalifu katika mkoa huo kwa kipindi cha miaka miwili.

Matei alisema mwaka 2018 watu waliofariki kutokana na ajali za barabarani walikuwa 92 wakati waliofariki mwaka 2019 walikuwa watu 40 sawa na upungufu wa watu 52.

"Lakini katika kipindi cha kuanzia Januari 2018, watu waliojeruhiwa kutokana na ajali za barabarani walikuwa 132, lakini mwezi kipindi kama hicho 2019 watu waliojeruhiwa walikuwa 78 sawa na upungufu wa watu 54 ambayo ni asilimia 41," alisema Matei.

Hata hivyo, alisema hata makosa ya ukiukwaji wa sheria za barabarani pia yalipungua kwa asilimia 11, huku hata makusanyo ya tozo hizo yakipungua.

Alisema mwaka 2018 yalitokea makosa ya usalama barabarani 84,191 ambayo yalitozwa zaidi ya Sh. bilioni 2.5, lakini mwaka 2019 yalitokea makosa 74,601 ambayo yaliliingizia Jeshi la Polisi Sh. bilioni 2.2.

Pia alisema katika mwaka 2019 hakukutokea ajali yoyote kubwa ambayo iligharimu maisha ya wananchi wengi kama ilivyotokea mwaka 2018, ambapo zilitokea ajali zilizogharimu mpaka maisha ya watu zaidi ya 20 kwa wakati mmoja.

# Rungwe wajipanga ujenzi wa maktaba

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

BAADHI ya wananchi wazawa wa Wilaya ya Rungwe wanaoishi ndani na nje ya wilaya hiyo, ambao wameunda kikundi cha 'Rungwe Yetu', wamekubaliana kujenga maktaba ya wilaya hiyo kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi kujisomea ili kukuza kiwango cha elimu.

Wananchi hao walikubaliana kujenga maktaba hiyo, juzi, wakati wa mkutano wa mwaka wa kikundi hicho ambao ulifanyika katika Mji wa Tukuyu, na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilikubali kutoa eneo kwa ajili ya kufanikisha azma hiyo.

Msafiri Nsajigwa alisema watawatafuta wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi ambao watachangia michango tofauti ili kukamilisha azima yao ya kujenga maktaba hiyo.

Alisema ujenzi wa maktaba hiyo ni sehemu ya mikakati ya kikundi hicho katika kuimarisha sekta ya elimu katika wilaya hiyo, ikiwa ni pamoja na kuinua kiwango cha ufaulu katika ngazi zote za elimu.

"Tunataka watoto wetu, wadogo zetu na vizazi vyote ndani ya wilaya yetu vipate maarifa katika maktaba hiyo kwa ajili ya maisha yao ya baadaye, tutachangisha michango kwa watu mbalimbali ili kupata fedha hizo," alisema Nsajigwa. Katibu wa Rungwe Yetu, Ernest Mazigo, alisema mbali na azma yao ya kujenga maktaba hiyo pia kikundi hicho kimekuwa kikisaidia kuboresha miundombinu ya shule mbalimbali ndani ya wilaya hiyo kwa kuchangishana wao wenyewe.

Alisema baadhi ya vitu ambavyo wamekuwa wakichangia ni pamoja na mifuko ya saruji pamoja na bati kulingana na mahitaji ya shule husika na kwamba wataendelea kufanya hivyo.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Kenny Lawrence, alisema lengo lao ni kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano katika kuboresha miundombinu ya elimu nchini kama ambavyo inasisitizwa.

"Tunataka na sisi wilaya yetu izalishe wataalamu ambao watasaidia katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya taifa letu hasa katika sekta ya viwanda ambayo inahubiriwa na serikali yetu," alisema Lauwence.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Juliua Chalya, alisema baadhi ya mambo ya maendeleo yanapaswa kuamuliwa na wanarungwe wenyewe badala ya kusubiri serikali ifanye kila kitu hali ambayo inachelewesha maendeleo.

Alisema uamuzi huo wa kujenga maktaba ya wilaya ni wenye manufaa kwa Wanarungwe wenyewe na Watanzania kwa ujumla kwa maelezo kuwa sio kila atakayenufaika ni mwana Rungwe.

Naye Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Dk. Steven Mwakajumilo, aliwapongeza wanakikundi hao kwa uamuzi wao wa kufanya shughuli hizo za maendeleo ndani ya wilaya hiyo.

Alisema mambo wanayofanya wanakikundi hao yanasaidia katika kutimiza matakwa ya Ilani ya Uchaguzi ya chama hicho na hivyo akawaahidi chama chake kuendelea kushirikiana nao.





# Ofisi ya CAG yaanika sababu utekelezaji miradi kuchelewa

Na Renatha Msungu, DODOMA

OFISI ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali imesema usimamizi hafifu wa miradi mbalimbali nchini umechangia kwa kiasi kikubwa kutokamilika kwa miradi ya maendeleo na kusababisha utekelezaji miradi hiyo kuwa kwa muda mrefu.

Akichambua Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Toleo Maalumu la Wananchi la Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mkaguzi Henry Naiman, alisema ukaguzi umebainisha upungufu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Alisema CAG amebaini miradi 27 yenye thamani ya Sh. bilioni 5.24 ilikamilika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 16, lakini haitumiki, huku Halmashauri ya Wilaya Mtwara iliongoza kwa kuwa na miradi ya Sh. bilioni 1.96.

Alisema pia imebaini kiasi cha Sh. bilioni 5.02 zilitumika kwenye shughuli zisizokusudiwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 40.

Pia miradi ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 41.95 haikutekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 30 kwa ilivyokuwa imeangwa kutokana na kutopokea fedha kutoka Serikali Kuu au makusanyo hafifu ya mapato ndani.

Pia kazi za miradi ya maendeleo zenye thamani ya Sh. bilioni 8.27 hazikutekelezwa licha ya kuwepo na fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 18.

Alisema pia imebaini usimamizi hafifu wa miradi, umesababisha kutokamilika kwa miradi ya maendeleo na kutelekeza miradi ya muda mrefu, miradi hiyo yenye thamani ya Sh. bilioni 52.43 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 47.

Kutokana na upungufu huo wakati wa ukaguzi, CAG ameshauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha miradi ambayo haijakamilika na iliyotelekezwa inakamilishwa, miradi yote ikikamilika inatumika.

Aidha, Naiman alisema ukaguzi huo umebaini Mamlaka za Serikali za Mitaa 62 (ambazo ni sawa na asilimia 33.5 ya halmashauri zote 185) hazikupeleka asilimia 20 ya ruzuku zilizopokelewa kutoka Serikali Kuu yenye jumla ya Sh. bilioni 3.32 kwenye ngazi za chini (vijiji, mitaa, kata) ikiwa ni fidia ya vyanzo vya ndani vya mapato vilivyofutwa.



Kontena za kuhifadhia takataka zilizowekwa pembezoni mwa soko kuu la Majengo jijini Dodoma zikiwa zimezingirwa maji machafu, hivyo kutoa harufu kali kwa wafanyabiashara wa soko hilo na wapita njia. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mbegu bora za alizeti zapatikana

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

SERIKALI imepata mbegu bora ya alizeti yenye uwezo wa kutoa asilimia 48 ya mafuta inapokamuliwa na kuacha asilimia 52 ambazo in makapi, mashudu na uchafu mwingine.

Aidha, Wizara ya Kilimo inashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuongeza mnyororo wa thamani wa zao la alizeti.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao nchini, Nyasebwa Chimagu, alisema mbegu hiyo wanaamini itakuwa suluhisho la utatuzi wa upatikanaji wa mbegu bora kwa ajili ya zao hilo.

Alisema asilimia 48 ya mafuta kutoka katika mkamuo mmoja ni jambo la kupiga hatua moja mbele ikiwamo wakulima kuondokana na kero ya kulalamikia upatikanaji wa mbegu bora. Alisema wao kama serikali wameshirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya umma na binafsi kuhakikisha wanatatua changamoto ya upatikanaji wa mbegu bora za kisasa ambazo zitaleta tija kwa wakulima wa zao hilo.

"Wakulima wamekuwa wakilalamika kwa muda mrefu kuhusiana na upatikanaji wa mbegu bora ya zao hilo, hivyo serikali kwa kushirikiana na sekta ya umma na binafsi ambao wanahusika na masuala ya mbegu wamekuwa wakikutana kila mara ili kuhakikisha wanaimaliza changamoto hiyo," alisema Chimagu.

Alisema wakulima hivi sasa wategemee mambo mazuri kutoka wizara hiyo hususani suala zima la upatikanaji wa mbegu bora kwa ajili ya zao hilo.

Katika hatua nyingine, Nyasebwa alisema mashine zinazotumika katika ukamuaji alizeti kwa wakulima na wasindikaji imekuwa tatizo kubwa hivyo amewataka wakulima kuwa makini kwa sababu nazo zinachangia upatikanaji hafifu wa mafuta hayo.

"Mashine za mafuta nazo ni tatizo, nyingi zimekuwa zikibakisha mafuta mengi wakati wa kukamua hivyo wanapaswa kuliangalia hilo," alisema Nyasebwa.

Alifafanua zaidi ya kuwa tatizo hilo nalo wamegundua kuwa ni moja ya chanzo cha upatikanaji wa zao hilo.

Naye Meneja wa Chama cha Wakulima wa Alizeti nchini (SUFA), Stephen Henry, alisema kama mbegu hiyo imepatikana itakuwa msaada mkubwa sana kwa wakulima kwa sababu kilio chao kila kukicha ni suala la upatikanaji mbegu bora za kisasa.

"Tumekuwa tukilalamika kila mara kuhusu upatikanaji wa mbegu bora kama serikali imelifanyia kazi itatusaidia kwa kiasi kikubwa," alisema Henry.

Alisema wanaishukuru serikali kwa jitihada inazofanya kuhakikisha zao la alizeti linakuwa mstari wa mbele katika utoaji wa mafuta hapa nchini.

Alisema wanaamini changamoto hiyo kama imetatuliwa basi wakulima watafaidika na kilimo hicho, ikiwamo kufanya kilimo chenye tija badala ya hasara.

## Sheikh aasa wazazi mavazi ya watoto

Na Renatha Msungu, DODOMA

SHEIKH wa Msikiti wa Manchali Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, Shaban Mbaruku, amesema wazazi wanatakiwa kusimamia vizuri suala la mavazi kwa watoto wao ili wasiwe vichocheo vya ngono, ambavyo hupelekea kuharibu maisha yao.

Alisema hayo wakati wa kutolewa kwa mapendekezo ya kutengeneza sheria ndogo zinazotakiwa kuwapo kwenye mazingira ya wanafunzi kuanzia shuleni, nyumbani kwenye nyumba za ibada na kwenye serikali za vijiji, vitongoji.

Sheikk Mbaruku alisema watoto wengi wa kike wamekuwa wakivaa mavazi yasiyo na maadili yanayochochea vitendo vya ngono.

Alisema wazazi wanatakiwa kutimiza wajibu wao katika masuala ya malezi ili watoto wakue kwenye maadili mema na hatimaye kufikia ndoto zao.

Akitoa mfano, alisema kijijini hapo kuna familia ilihamia kutoka mkoani Tanga na watoto wa familia ile walikuwa wakivaa nguo ndefu na kufunika vichwa vyao.

"Baadaye tukaona wameacha ule utamaduni wa kujisitiri kama walivyokuja sasa tukawa tunajiuliza labda ni kutokana na mazingira waliyoyakuta hapa."

Alisema kwenye sheria ndogo zitakazoundwa suala la mavazi ya heshima lipewe kipaumbele, watoto hasa wasichana wavae sketi zinazositiri maungo yao.

" Wazazi na hata walimu wajitahidi kuelimisha watoto juu ya mavazi, kinachomtamanisha mtoto wa kiume ni maumbile ya mtoto wa kike kwenye, nyumba za ibada tunajitahidi kutoa elimu ya kutosha," alisema.

Mmoja wa wazazi, William Mazengo, alisema walimu wanatakiwa kuwasikiliza watoto kabla ya kutoa adhabu.

"Mwanafunzi mwingine ukimchapa sana unampoteza na adhabu zinachangia watoto kufeli," alisema.

Miongoni mwa sheria zilizopendekezwa na wanafunzi hao ni kuwazuia walimu kuwatuma wanafunzi wakati wa vipindi vya darasani, walimu waandike notisi wenyewe ubaoni badala ya kuachia wanafunzi ambao baadaye hukosa muda wa kujisomea.

Pia walitaka walimu kupunguza adhabu kali kwa wanafunzi ikiwamo kuchimba visiki na watoto wasikilizwe kabla ya kupewa adhabu.

Kwenye maoni juu ya nyumba za ibada walipendekeza kupunguza muda wa wanafunzi kuimba kwaya au kwenda kwenye makongamano ya kidini ili wanafunzi wasikose muda wa masomo na ikiwezekana waruhusiwe wakati wa likizo tu.

Mratibu wa Wowap Nasra Suleiman, alisema Shule ya Sekondari ya Manchali inatekeleza mradi wa Sauti Yangu wenye lengo la kuondoa ukatili kwa watoto na kufanya mabadiliko katika mambo yaliyo katika mfumo wenye lengo la kuhakikisha watoto wanashirikiana na shule, wazazi, viongozi wa vijiji na viongozi wa dini.



## Chadema watishia kujitoa uchaguzi mkuu mwaka huu

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimesema kitajitoa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu iwapo hawatoridhishwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) katika kuuendesha.

Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Unguja, Said Mzee Said, aliyasema hayo alipozungumza na waandishi wa habari makao makuu ya chama hicho, Kikwajuni mjini Unguja.

Alisema chama hicho hakitokubaliana kuona taasisi zinazoendesha

uchaguzi zinafanya vitendo vya kuharibu uchaguzi, hivyo kutokuwa huru na wa haki.

"Sisi Chadema tumeelekeza nguvu zetu zaidi kudai tume huru ya uchaguzi na endapo suala hili halitofanyika, sisi tunafikiria kujiondoa katika uchaguzi, lakini tunaamini kwamba tutaendelea kupambana kuhakikisha tume huru inapatikana kwa njia zote," alisema.

Alisema licha ya kile alichodai kuchelewa kupata taarifa za uboreshaji wa daftari la wapigakura, aliwataka wanachama wa chama hicho kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari hilo.

"Tayari NEC imeanza zoezi la uandikishaji wapigakura wapya, nitoe rai kwa wananchi wote wenye sifa kujitokeza katika zoezi hilo kwa sababu uchaguzi unaanzia katika uandikishaji," alishauri.

Alisema chama hicho pia kinafuatilia uboreshaji wa daftari la wapigakura unaotarajiwa kukamilika siku 17 zijazo.

Alisema chama hicho kimeandaa mikakati mitano ya kuelekea uchaguzi huo, akiiomba NEC kuwapa fursa wananchi wenye sifa ya kuingia kwenye daftari la wapigakura, waandikishwe bila kuwapo ubaguzi.

Aliwataka mashekha kutoa barua za utambulisho bila ya kubaguliwa wapinzani kama ilivyokuwa katika uchaguzi uliopita.

# Mwakilishi aipa mbinu serikali kutatua msongamano darasani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, leo anatarajiwa kuzindua shule mpya ya kisasa ya biashara iliyojengwa na mkandarasi mzalendo ambaye ni mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa

Kuteuliwa na Rais.

Akizungumza na Nipashe, mwakilishi huyo, Ahmada Yahya Abdulwakil, alisema ameamua kujenga shule hiyo ili kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani. Alisema kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi darasani katika Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, aliona kuna haja ya kujenga shule hiyo ili wanafunzi wasome katika mazingira mazuri na kuwa na uhakika wa kufaulu.

"Nilianza ujenzi wa shule hii mwaka 2017 na sasa ujenzi umekamilika, kesho (leo) Rais wa Zanzibar ataizindua shule na kuikabidhi Wizara ya Elimu," alisema.

Abdulwakil alidai mradi wa ujenzi wa shule hiyo ya kisasa, mwanzoni alibezwa na baadhi ya wananchi na sasa anafuraha kubwa kuona umekamilika katika muda mwafaka.

Alisema: "Kutoa ni moyo si utajiri, nashukuru mradi huu wa ujenzi wa shule nimeukamilisha na naishukuru serikali haikutoza kodi ya aina yoyote katika uletaji wa vifaa vya ujenzi wa shule hii," alisifu. Alisema jengo la ghorofa la shule hiyo limejengwa na wataalamu wazalendo na limezingatia miundombinu rafiki kwa watu wenye mahitaji maalum.

Alisema shule hiyo itakuwa na madarasa tisa, maabara za kisasa, ofisi za walimu na huduma zingine za kijamii.

Aliwataka walimu na wanafunzi wa shule hiyo kuitunza ili idumu kwa muda mrefu na kuhakikisha wanazipa kazi kampuni za usafi kufanya usafi shuleni hapo badala ya kuwategemea wanafunzi kutekeleza jukumu hilo.




Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Ahmada Yahya Abdulwakil, akionyesha ofisi ya mwalimu mkuu katika shule mpya ya kisasa ya biashara aliyoijenga, ambayo leo itazinduliwa na Rais wa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Taasisi zatakiwa kujipanga huduma sherehe Mapinduzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATENDAJI wa taasisi mbalimbali za serikali zinazohusika na kutoa

huduma katika sherehe za Mapinduzi, wametakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano ili kufanikisha sherehe za miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar Januari 12 mwaka huu.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Shaabani Seif Mohamed, amesema ushirikiano huo utasaidia kufanikisha sherehe hizo kufanyika kwa ufanisi ili kuenzi kumbukumbu ya historia ya Zanzibar.

Aliyasema hayo wakati akikagua maendeleo ya maandalizi ya Uwanja cha Amani utakaotumika kwa sherehe hizo.

Katibu Mkuu huyo alisema kutokana na maandalizi yaliyofikiwa, hakuna shaka yoyote juu ya matumizi ya uwanja huo.

Akizungumzia upatikanaji wa huduma muhimu katika kiwanja hicho, ikiwamo umeme na majisafi na salama, Katibu Mkuu huyo alisema ameridhishwa kutokana na mikakati na jitihada zilizochukuliwa na uongozi wa mamlaka ya maji Zanzibar (ZAWA) kwa kuisogeza karibu huduma hiyo na kufanikisha kuweka maji mengine ya akiba endapo yatahitajika wakati wowote.

"Niseme tu nawapongeza sana ndugu zangu wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa ushirikiano wao mzuri walioutoa katika kuhakikisha huduma hii muhimu inapatikana kiwanjani hapa katika kipindi chote cha sherehe," alisifu.

Katika maelezo yake kwa Katibu Mkuu Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Omar Hassan Omar, alimwambia Shaaban kuwa maandalizi ya uwanja huo yamekamilika kwa kufanya marekebisho sehemu ya uwanja ikiwamo kuweka alama ndani ya kiwanja zitakavyoviwezesha vikosi vya ulinzi na usalama kucheza gwaride bila ya usumbufu.

Alisema wizara inajitahidi kuhakikisha usafi wa mazingira ya nje na ndani ya uwanja huo yanakuwa yenye haiba nzuri yenye kuvutia, huku mafundi wengine wakiendelea kukamilisha baadhi ya mambo yanayohitajika kiwanjani hapo.

# Wajadili mbinu kuvutia uwekezaji

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

HALMASHAURI za wilaya mkoani Tabora zimetakiwa kuhakikisha zinamaliza migogoro ya ardhi kwa ajili kuweka mazingira ambayo yatawavutia wawekezaji.

Rai hiyo ilitolewa na Mtaalamu Mwelekezi kutoka Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Jamii (ESRF), Dk. Hoseana Lunogelo, kwenye kikao cha kupata maoni ya juu ya mwongozo wa uwekezaji wa Mkoa wa Tabora.

Alisema Mkoa wa Tabora una maeneo mengi ambayo yanafaa kwa uwekezaji, lakini uwekezaji unaweza kukwama panapokuwapo na eneo ambalo linaonekana lina mgogoro kati ya jamii na halmashauri husika.

Dk. Lunogelo alisema Tabora ni moja ya mikoa nchini ambayo ina jiografia nzuri na miundombinu yake inayoiunganisha na mikoa inayoizunguka, hivyo kuwa na uwezo wa kusafirisha bidhaa zinazozalishwa na kufika sokoni kwa urahisi.

Aliongeza kuwa mkoa huo una fursa kubwa kwa uwekezaji wa asali kwani wilaya zake zimezungukwa na misitu ya miombo ambayo ni malisho mazuri ya nyuki.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu, alizitaka halmashauri za wilaya kuhakikisha zinatenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji, na pale inapoonekana kuna vikwazo kutokana na wananchi kudai fidia dhidi ya maeneo yao, wawalipe mapema.

Alisema sio vizuri wawekezaji wapewe eneo ambalo lina migogoro, hatua hiyo itasababisha waende maeneo mengine kwa ajili ya kutafuta maeneo ambayo wana uhakika wa uwekezaji wao.

Aidha, Makungu aliwaomba wenyeviti wa halmashauri kutumia vikao vya mabaraza ya madiwani kuhakikisha zoezi hilo linafanikiwa, na wananchi wanalijua ili wawekezaji wasikwamishwe na migogoro ya ardhi.

Baadhi ya wachangiaji mbalimbali kutoka halmashauri za wilaya hiyo walisema ni vema maeneo ya uwekezaji yakawa na miundombinu mbalimbali, ukiwamo upatikanaji wa maji, barabara, umeme na maeneo kuwa na hati ili kuwavutia wawekezaji.

Mkutano huo ni matokeo ya Jukwaa la Biashara na Uwekezaji lililofanyika mkoani hapa Novemba mwaka jana na kufunguliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

# Wataka Tanroads, Tarura kupewa fedha sawa

**Na Happy Severine,** SIMIYU

WAJUMBE wa kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Simiyu wameishauri serikali kutenga fedha za bajeti ya miradi ya barabara kwa uwiano kwa Wakala wa Barabara (Tanroads) na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Wajumbe hao walitoa ushauri huo juzi, kufuatia taarifa ya Tanroads kupokea fedha asilimia 70, huku Tarura ikipata asilimia 30 pekee, hivyo kutokidhi utekelezaji wa mahitaji ya ujenzi na ukarabati wa barabara.

Walisema serikali ni vema ikaweka uwiano wa fedha kati ya Tanroads na Tarura ili kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi.

"Tunaomba serikali iangalie upya kiwango cha fedha wanachokitoa Tarura na Tanroads, fedha zitolewe kwa uwiano ili kurahisisha utendaji kazi ulio rahisi," alisema mmoja wa wajumbe.

Kaimu Meneja wa Tanroads Mkoa wa Simiyu, John Mkumbo, alisema katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2019/20, kazi za matengenezo ya barabara ambazo zipo kwenye utekelezaji ni kilomita 108.12 na madaraja 14.3 sawa na asilimia 54.3.

Mratibu wa Tarura Mkoa wa Simiyu, Dk. Philemon Msomba, alisema wametekeleza jumla ya miradi 30 ambayo imekamilika yenye thamani ya Sh. bilioni 3.6 bila VAT.

Aliongeza kuwa Tarura wanahudumia jumla ya kilomita 4,038.16 za barabara kwa uhakiki, huku akibaini barabara nzuri ni kilomita 667.08 sawa na asilimia 16.52, barabara za wastani ni kilomita1,555.91 sawa na asilimia 38.53 na barabara mbaya ni kilomita 1,815.17 sawa na asilimia 44.95.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Wilaya ya Meatu, Dk. Joseph Chilongani na Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya hiyo, Fabian Manoza, walisema ni vyema Tanroads na Tarura kuona haja ya kutengeneza na kuboresha madaraja yaliyopo wilayani kwa kujenga madaraja ya juu badala ya yaliopo sasa ambayo ni ya chini ili kupunguza uharibifu wa barabara.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Jumanne Sagini, alitoa wito kwa wakurugenzi wa mkoa huo kuhakikisha wanashughulikia suala la vyumba vya madarasa, huku akiongeza kuwa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka 2020 wote watakiwa kupangiwa shule na wanapaswa kuripoti Januari 6 bila kisingizio chochote.



Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi, Erasto Yohana Sima, akiwa katika ziara ya siku 2 ya kikazi akikagua utengenezaji wa mizinga 700 ya nyuki kwa ajili ya mkakati wa 2020 kwa wilaya zote za Mkoa wa Arusha. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wafugaji wa nyuki wapata ukombozi

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

JUMLA ya Sh. milioni 495 zinatarajiwa kutumika katika uanzishaji wa kiwanda kikubwa cha kuchakata asali katika eneo ambalo lilikuwa Kituo cha Maendeleo ya Vijana cha Tulu wilayani Sikonge mkoani Tabora.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, Peres Magiri, wakati wa mkutano na wanahabari baada ya kikao cha kupata maoni ya juu ya mwongozo wa uwekezaji wa kiasi hicho ni sehemu ya fedha ambazo zinatakiwa ziwe sehemu ya kampuni kurudisha katika jamii kutokana na miradi ya barabara inayojengwa kutoka Tabora kupitia Sikonge kwenda Mpanda.

Magiri alisema kuwa wameamua kuanzisha kiwanda cha kuchakata asali katika eneo hilo kutokana na uwapo wa miundombinu mbalimbali katika eneo hilo ikiwamo maghala na majengo mengine ambayo yanafaa kwa uanzishaji wa kiwando hicho.

Alisema wameona kuwa watumie majengo hayo baada ya kuona hayatumiki kwa ajili ya kuleta faida kubwa kwa wakazi wa eneo la Sikonge na Mkoa wa Tabora.

Magiri alisema kuanzishwa kwa kiwanda katika eneo hilo ni sahihi kutokana na Wilaya ya Sikonge kuwa na eneo la hifadhi ya misitu hekta milioni 1.9 ambayo inaweza kusaidia katika uzalishaji wa asali ya kutoka kwa ajili ya malighafi za kiwanda.

Alisema kuwa lengo ni kuwa na kiwanda cha asali katika Wilaya ya Sikonge ni kuachana na ile tabia ya kugeuza eneo hilo kuwa sehemu ya ukusanyaji asali ghafi na kuwa sehemu ya uchakataji na uongezaji wa thamani asali kwa ajili ya kutangaza eneo la Sikonge na Mkoa wa Tabora kwa ujumla.

Magiri alisema hatua itachochea wafugaji kuendesha ufugaji wa kisasa wa nyuki kwa ajili ya kuwaongezea kipato wao na halmashauri kwa ujumla.

Wilaya ya Sikonge ni miongoni mwa maeneo yenye hifadhi kubwa ya misitu ambayo ni asilimia tano ya ardhi yote inatumika kwa shughuli za kilimo na makazi.

## HABARI KIMATAIFA

## Waandamana kupinga Marekani kuwashambulia wanamgambo

**BAGHDAD,** Iraq

WAOMBOLEZAJI walikusanyika nje ya ubalozi wa Marekani mjini Baghdad, kulaani mashambulio ya ndege za Marekani yaliyolenga vituo vya wanamgambo wa Kishia.

Waombolezaji hao walizingira ubalozi huo uliopo kwenye eneo lenye ulinzi mkali, wakiwa wamebeba bendera za kundi la wanamgambo lenye ushawishi mkubwa.

**Wakati huo huo**, Saudi Arabia imewalaani wanamgambo wanaoungwa mkono na Iran kwa kuyashambulia majeshi ya Marekani yaliyoko nchini Iraq na kusababisha mkandarasi mmoja wa Marekani kuuawa.

Marekani ilijibu kwa kuwashambulia kwa ndege wanamgambo hao wa Kataib Hezbollah siku ya Jumapili iliyopita.

Hata hivyo, Waziri Mkuu wa Iraq, Adel Abdul Mahdi, ameilaani kitendo cha Marekani kwa kufanya mashambilio ya ndege yaliyolenga vituo vya wanamgambo wanaoungwa mkono na Iran. **DW**

## Maharamia wavamia meli, wateka nyara mabaharia

**YAOUNDE,** Cameroon

MAMLAKA ya Ugiriki imesema jana kwamba mabaharia wanane wametekwa nyara na mmoja wao amejeruhiwa baada ya maharamia waliokuwa na silaha kuingia ndani ya meli moja ya mafuta ya nchi hiyo.

Tukio hilo limetokea katika pwani ya Cameroon. Wizara ya Usafirishaji wa Baharini nchini Ugiriki. imesema kwamba meli hiyo inayoitwa 'Happy Lady' iliyosajiliwa nchini Ugiriki, ilikuwa maili mbili kutoka kwenye Bandari ya Limboh ndipo ilipovamiwa na watu hao wenye silaha.

Jumla ya wafanyakazi 28 walikuwamo ndani ya meli hiyo. **DW**

# Maelfu sasa wakimbilia baharini kujinusuru moto

**SYDNEY,** Australia

MAELFU ya watu nchini Australia, wamekimbilia katika fukwe ya bahari kujinusuru na moto wa nyikani ambao unaoelekea maeneo ya pwani.

Wakazi wa Mallacoota wameuelezea moto huo kuwa kisa cha kuogofya, huku wakisimulia jinsi walivyoona anga ilivyobadilika rangi nyekundu wakiwa ndani ya boti.

Maofisa wamethibitisha kuwa watu wawili wamefariki kutokana na moto huo katika mji wa New South Wales, na kufikia idadi ya vifo 12 tangu kuibuka kwa moto huo.

Mamlaka pia zinasema watu wanne hawajulikani waliko katika miji ya Victoria na New South Wales.

Miili ya waathiriwa wa hivi punde ambayo inaaminiwa kuwa ya baba na mwanawe wa kiume, ilipatikana katika mji wa Corbargo ambao ulikumbwa na moto siku ya Jumanne.

"Hali ya kusikitisha," alisema Naibu wa Kamishena wa Polisi, Gary Worboys. Aliongeza: "bila shaka walikuwa wanajaribu kujinusuru kutokana na moto huo kwa sababu ulizuka mapema saa za asubuhi."

**Ilikuwa mchana lakini kulikuwa na giza sawa na usiku wa manane, na kile tulichosikia ni sauti ya moto mkali uliokuwa ukisambaa kwa kasi ya ajabu.**

Mjini Mallacoota, wahudumu wa kitengo cha kuzima moto walisema mkondo wa upepo umebadilika na kuongeza kuwa hali hiyo imegeuza mkondo wa moto kuuelekea maeneo ya makazi.

Maeneo kadhaa ya kujivinjari msimu wa sherehe katika mwambao wa pwani kati ya miji ya Sydney na Melbourne kwa sasa yamekatazwa kutokana na moto huo.

Gavana wa Jimbo la Victoria Daniel Andrews, amesema meli huenda zikatumwa kuwapelekea waathirika wa moto huo chakula, maji na nguvu za umeme katika maeneo hayo.

Kutokana na hali mbaya barabara kuu ya Princes Highway imefungwa, hivyo ni vigumu kuwafikia watu hao.

"Baadhi ya watu waliotengwa wanaweza kufikiwa kupitia bahari," alisema.

Mamlaka zilitoa wito kwa watu wa eneo hilo, wengi wao watalii kutoondoka haraka. Hata hivyo ilipofika Jumatatu hali ilikuwa mbaya zaidi na kulazimisha kuwahamisha.

Moto wa nyikani katika eneo la kaskazini mwa nchi hiyo umetokana na ongezeko la viwango vya joto, upepo mkali na radi ya wakati wa ukame.

Mamlaka pia zinasema zimeripoti kwa watu saba hawajulikani waliko katika eneo hilo, wanne kutoka Victoria na watatu wa New South Wales.

"Tunahofia usalama wao. Wamekuwa katika mazingira ya moto na hatuwezi kubainisha waliko kwa sasa," alisema Waziri Mkuu wa Victoria, Daniel Andrews.

Baadhi ya wakazi wameiambia BBC kuwa hali ilikuwa ya kuogopesha huku majivu yaliyotokana na moto huo, yakianguka katika fukwe za bahari. Mji wa Mallacoota, umeathiriwa zaidi na moto huo, na siku ya Jumanne wakazi walilazimika kukimbilia usalama wao.

"Ilikuwa mchana lakini kulikuwa na giza sawa na usiku wa manane, na kile tulichosikia ni sauti ya moto mkali uliokuwa ukisambaa kwa kasi ya ajabu," alisema David Jeffrey, mmoja wa wafanyabiashara.

Moto huo umeharibu majengo kadhaa, lakini ulikatiza makali yake baada ya mkondo wa upepo katika ufuo wa bahari kubadilika. **BBC**



Mkazi wa Carbago nchini Australia, akipita kandokando ya barabara kuukimbia moto jana, ambao uliteketeza misitu na makazi ya watu. **PICHA: AFP**

# Madaktari kujifunza uchawi chuoni India

**NEW DELHI,** India

DUNIA ina maajabu yake! Unaweza kushangazwa na jambo hili, lakini ndivyo ilivyo kwa wasomi kuamua kujikita kujifunza uchawi ili kupambana na mapepo.

Kulingana na taarifa kutoka chuo kimoja maarufu nchini India, kimeanza kutoa kozi ya ngazi ya cheti kwa madaktari wanaotaka kujifunza uchawi ambao utawawezesha kutibu wagonjwa wanaopatwa mapepo au huyaona.

Kozi hiyo ya miezi sita itatolewa katika Chuo Kikuu cha Banaras Hindu (BHU), kilichoko kwenye Mji wa Kaskazini wa Varasanasi. Kozi hiyo itaanza kupokea wanafunzi mwezi huu.

Na pia kozi hiyo itakuwa inatolewa na kitengo cha afya ya akili na magonjwa yasiyo ya kawaida.

Msemaji wa chuo hicho, aliliambia shirika la habari la India, kuwa kitengo cha masomo ya uchawi kimeanzishwa.

"Kitengo hicho kinaitwa Bhoot Vidya na kunajihusisha na magonjwa yasiyo ya kawaida ama matatizo ya akili" anasema Yamini Bhushan Tripathi, mkuu wa kitengo hicho.

Aliongeza pia chuo hicho kitakuwa cha kwanza kuanzisha kozi ya namna hiyo ambayo itafundisha masomo ya utabibu wa majini, mapepo na mizimu.

Matibabu yatatolewa kwa njia ya dawa za asili, miti shamba na masaji.

Kwa mujibu wa utafiti wa 2016 wa kitengo cha magonjwa ya akili (Nimhans), karibu asilimia 14 ya watu nchini India ni wagonjwa wa akili.

Mwaka 2017 Shirika la Afya Duniani WHO inakadiria asilimia 20 ya Wahindi wanaweza kupatwa na msongo wa mawazo katika kipindi fulani katika maisha yao.

Lakini kuna chini ya wagonjwa 4,000 wa akili huwa wanaenda hospitali kupatiwa matibabu rasmi, kuna uelewa mdogo sana juu ya afya ya akili.

Lakini kutokana na unyanyapaa kusambaa, wagonjwa wachache ndio wanaenda hospitali, wengi huenda kwa waganga wa kienyeji na kudhani kuwa watatibiwa matatizo yao ya akili.

Hata hivyo, watu wengi wameonesha kulidhihaki tangazo hilo katika mitandao ya kijami, baadhi wamehoji kama serikali ya India suala hilo ni moja ya vipaumbele vyake.

Taarifa ya kuwa chuo hiko cha serikali kitaanza kutoa kozi hiyo, imepokelewa kwa maoni mbalimbali katika mitandao ya kijamii, wengi wakiuliza ni namna gani kozi hiyo itatolewa? **BBC**

# Kigogo Mambo ya Nje kortini tuhuma ufisadi

**Na Hellen Mwango**

KIGOGO wa Fedha wa Wizara ya Mambo wa Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Athanas Madebe, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam akikabiliwa na mashtaka 15 ikiwamo kuisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 472,684.

Madebe ambaye ni mwambata wa fedha wa wizara hiyo alifikishwa katika mahakama hiyo jana na kusomewa mashtaka hayo, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, akisaidiana na Mawakili wa Serikali, Yemiko Mlekano na Elia Athanas, walimsomea mshtakiwa mashtaka yake kwamba kati ya Oktoba Mosi mwaka 2014 na Desemba 31, mwaka 2016 katika Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania, nchini Ethiopia alitenda kosa hilo.

Wankyo alidai kati ya mashtaka 15 yanayomkabili mshtakiwa huyo, 10 ni ya kughushi, mawili ya wizi akiwa mtumishi, moja la kutumia nyaraka za uongo kumdanganya mwajiri wake, moja la utakatisha fedha na kuisabishia hasara serikali.

Ilidaiwa kati ya Oktoba Mosi, 2014 na Desemba 31, 2016 katika Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania, jiji la Addis Ababa, Ethiopia, mshtakiwa akiwa mwajiriwa wa wizara hiyo alitengeneza nyaraka ya benki inayoendeshwa na ubalozi wa Tanzania uliopo mchini Ethiopia, akionyesha kuwa akaunti hiyo ina akiba ya Dola za Marekani 472,787 huku akijua si kweli.

Mlekano alidai katika mashtaka ya wizi, mshtakiwa akiwa mtumishi wa umma, kati ya Mei 3 na Juni 3, 2018 katika Ofisi za Ubalozi wa Tanzania nchini Ethiopia, aliiba Dola za Marekani 14,422 mali ya serikali kwamba alijipatia kupitia nafasi yake ya kazi.

Pia kati ya Julai Mosi mwaka huu na Agosti 31, mwaka huu, katika Ofisi za Ubalozi wa Tanzania nchini Ethiopia, mshtakiwa aliiba kiasi cha Sh. milioni 25, mali ya serikali, kupitia mikononi mwake akiwa mwambata wa fedha.

Ilidaiwa kati ya Februari 28,2017 katika ofisi hizo, kwa kutumia nyaraka za uongo kumdanganya mwajiri wake, alimwandikia barua Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje, akionyesha kuwa dola za kimarekani 236,000 kati ya dola 472,684 zilitoka Mfuko maalumu wa amani wa Umoja wa Afrika kwenda Benki Kuu ya Tanzania (BoT), wakati akijua si kweli.

Katika shtaka la kutakatisha fedha, mshtakiwa huyo anadaiwa kutenda kosa hilo, Mei 3, na Agosti 31, 2018 akiwa katika Ofisi za Ubalozi wa Tanzania nchini Ethiopia, alijipatia kiasi cha dola za Marekani 15,752 na fedha za Ethiopia 289,900.

Katika shtaka la kuisababishia hasara serikali, mshtakiwa anadaiwa kutenda kosa hilo kati ya Aprili 5, 2013 na Juni 30, 2015 ambapo kwa makusudi yeye na wenzake ambao hawajafikishwa mahakamani , aliisababishia serikali hasara ya dola za Marekani 472,684, ambapo fedha hizo zilipitia mikononi mwake kupitia nafasi yake ya kazi.

Hata hivyo, kutokana na mahakama hiyo kutokuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo, mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi haujakamilika.

Hakimu Chaungu alisema kesi hiyo itatajwa Januari 14, mwaka huu, na mshtakiwa apelekwe mahabusu.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Kanda ya Serengeti, Esther Matiko, akizungumza na wanahabari mkoani Shinyanga, kuhusu uchaguzi mkuu wa mwaka huu. Wa kwanza kulia ni Mbunge wa Viti Maalum mkoani Shinyanga, Salome Makamba, na kushoto ni Katibu wa Kanda ya Serengeti, Renatus Nzemo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Ataka jamii kusaidia watu wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOBA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amewataka Watanzania kuwajali na kuwapenda watu wenye ulemavu ambao hawawezi kumudu baadhi ya majukumu bila kupata msaada, lakini kwa vipawa vyao wanaweza kuisaidia jamii na taifa kwa ujumla.

Dk. Bashiru amesema kuwasaidia watu hao baadhi ya majukumu ya kila siku ambayo kwa maumbile yao hawawezi kuyafanya, itasababisha vipaji vyao kuonekana na kuwa msaada zaidi kwa jamii.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa makazi ya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Amon Mpanju, kijijini kwao, Nyakibimbili wilayani Bukoba. Inatakiwa tuwapende zaidi watu ambao kwa maumbile yao, hawawezi kutenda baadhi ya mambo bila msaada lakini wana vipawa vya kusaidia jamii yao na nchi kwa ujumla.

"Amon (Mpanju) ni miongoni mwa watu wanaotusikia, lakini hawatuoni, ila ninamfahamu vyema ni miongoni mwa vijana wachapakazi zaidi hata wanaoona na haya majukumu aliyo nayo hajapewa kwa sababu haoni ila ni kwa kuwa ana uwezo wa kuyamudu sawasawa," alisema.

Dk. Bashiru aliongeza kuwa: "Tuendelee kuwapenda watoto na mapenzi makubwa ni namna ya kuwandaa kupata elimu. Amon amefika hapo alipo kwa kuwa hao waliompenda walifanya kazi ya kumwelimisha licha ya changamoto zote.

"Na katika hili nipende kuwapongeza walimu nchi nzima kwa kazi mnayoifanya ambayo ni kazi ya kitakatifu. Ni kazi ya ukombozi na leo mmemkomboa Amon mpaka hapa alipofika."

Awali, akimkaribisha Katibu Mkuu, Mpanju alianza kwa kushukuru ujamaa kwa kuwa anaamini bila ujamaa yeye leo asingekuwapo, kwa kuwa alifiwa na wazazi wote akiwa na umri mdogo sana lakini alilelewa na watu wengi na wengine hata asiowajua kwa sababu ya uwapo wa ujamaa na undugu miongoni mwa Watanzania.

# Uhaba wa madarasa waikumba H/mashauri Bunda

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

HALMASHAURI ya Mji wa Bunda mkoani Mara, inakabiliwa na upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari.

Hali hiyo imeelezwa kuwa huenda ikasababisha wanafunzi wanaoingia darasa la kwanza na wale waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu kukosa mahali pa kusomea.

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, alisema hayo jana wakati akitoa salamu za serikali kwenye Kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, kilichofanyika katika ukumbi wa halmashauri mjini hapa.

Kutokana na hali hiyo, Bupilipili aliwataka wananchi katika halmashauri hiyo na wilaya nzima kwa ujumla, kutumia nguvu zao ili kujenga vyumba hivyo na ifikapo Februari, mwaka huu.

Bupilipili alisema vinahitajika vyumba vya madarasa 31 katika shule za sekondari na kwamba visipojengwa wanafunzi 1,700 waliochaguliwa kuingia kuanza kidato cha kwanza watakosa mahali pa kusomea.

"Kuna upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari. Kwa mfano katika shule za sekondari vinahitajika takribani vyumba 31, ambapo wanafunzi 1,700 waliochaguliwa kujiunga sekondari mwaka 2020 kupata mahali pa kusomea na tukiwaacha watoto hawa wakaingia mitaani ni hatari sana," alisema.

Baadhi ya madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Abraham Mayamaya, walimpongeza mkuu huyo kwa maelekezo yake mazuri ya serikali.

Pamoja na kupongeza, walisema suala la elimu ni la msingi, hivyo watawahamasisha wananchi wote katika maeneo yao wakiwamo wao wenyewe kujenga vyumba hivyo.

Walisema ni vyema wananchi wakahamasishwa ili kujenga vyumba vya madarasa kwa ajili ya kuwaokoa wanafunzi hao na kuwawezesha kupata haki yao ya msingi ambayo ni elimu.

Katika hatua nyingine, mkuu huyo wa wilaya aliwaonya watu aliowaita kwamba wameanza kupiga kampeni katika kipindi hiki ambacho si cha siasa.

Bupilipili alisema watu hao wamekuwa wakitumia kaulimbiu kwamba Bunda bila Mabegi inawezekana kwa maana kwamba hawataki wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi, katika uchaguzi mkuu ujao, ambao si wakazi wanaoishi katika Halmashauri ya Mji wa Bunda, kwa kuwa wakishachaguliwa hawawezi kuonekana tena.

Aidha, alisema kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo inafuatilia kwa ukaribu zaidi kumjua mfadhili wa kikundi hicho.

# MAN UNITED YAWANIA KUMSAJILI FERNANDES




**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inawania saini ya kiungo wa Benfica, Gedson Fernandes.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 raia wa Ureno, ni chaguo lao kwanza kwa klabu hiyo katika usajili wa dirisha dogo la Januari hii.

Hajaichezea Benfica katika mechi saba zilizopita na inaaminika kwamba hayupo kwenye mipango ya kocha, Bruno Lage.

Wawakilishi wa mchezaji huyo wameripotiwa kwamba wapo nchini Uingereza kwa ajili ya kujaribu kukamilisha usajili wake kwa mkopo wakiwa na pauni milioni 34, huku wakitaka kumnunua moja kwa moja.

Inaaminika kwamba, ada ya kuvunja mkataba wa Fernandes ni pauni milioni 102 , lakini Benfica wanajua kwamba hawatapata kiasi hicho cha fedha kwa mchezaji huyo ambaye kwa sasa anaonekana kutokuwa kwenye kiwango chake.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer amesema kwamba ataingia sokoni kama tu atapatikana mchezaji anayefiti kusajiliwa kwa muda mrefu klabuni hapo.

# Boateng atakiwa kuamua majaliwa yake Bayern Munich

**MUNICH,** Ujerumani

HANSI Flick amesema beki Jerome Boateng atatakiwa kusema kuhusu majaliwa yake baada ya kutokuwa na namba kwa sasa kwenye kikosi cha Bayern Munich.

Boateng ameanza katika mechi nane kati ya 17 ambazo Bayern imecheza kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, msimu huu na amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka wakati wa usajili wa Januari hii.

Juventus na Paris Saint-Germain zimekuwa zikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, huku pia Arsenal wakiripotiwa kumnyatia.

Na kocha wa muda, Flick amesema atamuachia Boateng kuamua mwenyewe, ambaye mkataba wake unamalizika msimu ujao, kama ataamua kubaki hapo kwenye dimba la Allianz Arena au kutafuta changamoto sehemu nyingine.

"Nimezungumza naye kwa uwazi kwa ka kirefu," alisema Flick akiliambia gazeti la Kicker la Ujerumani.

"Dhidi ya Wolfsburg aliingia na alikuwa na matatizo, lakini alionyesha ana ubora wa kuichezea Bayern.

"Jerome anatakiwa kufanya maamuzi kuhusu majaliwa yake kwa sababu muda wake unaelekea ukingoni."





# *Boca Juniors wampuuza Maradona kwa Pochettino*

**BUENOS AIRES,** Argentina

KLABU ya Boca Juniors imemteua kocha wa zamani, Miguel Angel Russo kuchukua mikoba ya Gustavo Alfaro.

Alfaro alijiuzulu mapema mwezi huu na gwiji wa klabu hiyo, Diego Maradona - ambaye kwa sasa anainoa timu ya Gimnasia y Esgrima La Plata inayoshiriki Ligi Kuu ya Argentina - alishauri kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino kupewa nafasi hiyo.

Hata hivyo, Boca wamemrudisha Russo, ambaye aliwahi kuwanoa miamba hao wa soka la Argentina mwaka 2007 na kuiongoza klabu hiyo kutwaa taji la Copa Libertadores (Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini).

"Mara zote nakuwa na hisia za aina yake ninaporudi Boca," alisema Russo akiwaambia waandishi wa habari.

"Makocha waliopita ambao walikuwa na bahati ya kutosha kushinda Copa Libertadores wamerudi.

"Nilijua kwamba, kuna wakati nitatakiwa kurudi na kamwe hilo halikunitoka akilini. Huu ndio wakati na nafasi nzuri."

"Nina matumaini naweza kushinda taji la Copa Libertadores na kusherehekea taji la ligi," alisema.

Russo mwenye umri wa miaka 63, amerudi kwenye jiji la Buenos Aires baada ya kukaa na klabu ya nchini Peru ya Alianza Lima na Cerro Porteno ya nchini Paraguay mwaka 2019.

Russo aliiongoza Cerro Porteno kwenye robo fainali ya Libertadores mwaka huu na walitolewa na washindi wa pili wa michuano hiyo, River Plate.

Wakiingia mwaka mpya, Boca wapo nafasi ya pili kwa pointi moja dhidi ya Argentinos Juniors baada ya mechi 16 za Ligi Kuu ya Argentina.

HABARI MICHEZO

# Klopp: Liver haitaanza kushangilia ubingwa

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema hawataanza kusherehekea ubingwa wa Ligi Kuu licha ya kuongoza kwa pointi nyingi, akisisitiza mbio za ubingwa huo bado hazijafika mwisho.

Wekundu hao leo wanaanza mwaka mpya wakiwa kileleni kwa tofauti ya pointi 13 baada ya Jumapili kushinda 1-0 dhidi ya Wolves kwenye dimba la Anfield.

Liverpool imerekodi ushindi mara 17 mfululizo kwenye Ligi Kuu ya England na wameendeleza rekodi ya kutofungwa nyumbani na kufikisha mechi 50 baada ya bao la Sadio Mane la Jumapili.

Wakati Liverpool inakaribia kutwaa ubingwa wake wa kwanza wa Ligi Kuu tangu mwaka 1990, Klopp amewaambia waandishi wa habari kikosi chake hakiwezi kushangilia ubingwa wa mapema baada ya mechi 19.

"Nafikiri mashabiki kwa uhakika kabisa wanaipenda timu yao," amesema Klopp ambaye ameiongoza Liverpool kushinda mechi 18 na sare moja kati ya mechi 19 za Ligi Kuu msimu huu na kuwa mbele ya Leicester City na bingwa mtetezi, Manchester City.

"Hawafikirii hilo kwa wakati huu. Hawataki kusherehekea sasa hivi. Wanaichukulia kama ilivyo tu. Wanatafuta ushindi kila mchezo na kwa uhakika mashabiki wana hamasa kubwa.

"Sisi ni wamoja na tutaendelea kupambana hadi mtu asema 'inatosha' na 'una pointi nyingi' au sio.





# XAVI: GUARDIOLA KAGEUKIA UEFA

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola kipaumbele chake kitakuwa kwenye taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Liverpool ikiwa imetawala kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya England, kwa mujibu wa Xavi.

City kwa sasa wanaangalia uwezekano wa kutwaa taji la tatu mfululizo la Ligi Kuu chini ya Guardiola, hata hivyo, mabingwa hao watetezi wapo nafasi ya tatu kwenye msimamo na wamepitwa pointi 14 dhidi ya wapinzani wao ambao hawajafungwa, Liverpool ambao wana mchezo mmoja mkononi baada ya mechi 20.

Huku kukiwa na uvumi kuhusu majaliwa ya muda mrefu ya Guardiola kubakia hapo Manchester, nyota wa zamani wa Barcelona, Xavi anaamini raia mwenzake huyo wa Hispania kipaumbele chake kitakuwa ni Ligi ya Mabingwa Ulaya kuelekea kwenye mchezo wa kwanza hatua ya mtoano wa timu 16 dhidi ya Real Madrid.

"Pep amezaliwa kuwa bingwa," amesema Xavi kocha wa klabu ya Al Sadd, ambaye alicheza chini ya Guardiola pale Camp Nou, akiliambia gazeti la The Mirror. "Itamuumiza kwamba, Manchester City wako nyuma na mbali dhidi ya Liverpool kwenye Ligi na hatakata tamaa.

"Ingawa anaujua ukweli. Pengo ni kubwa na wakati huu haionyeshi kama anaweza kutwaa taji kwa mara ya tatu mfululizo. "Huku hilo likiwa akilini, nafikiri kuna nafasi kubwa kwa Pep kipaumbele chake kuwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kutakuwa na mechi mbili kubwa zinakuja dhidi ya Real Madrid - na pengine kutakuwa na nafasi kwa wachezaji kupumzika kabla ya mechi hizi.

"Pep atataka kushinda kila taji analoweza, lakini kama ungemuuliza mwanzoni mwa msimu lile analolifikiria zaidi, nina uhakika kabisa angekuambia Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Alitaniana na Klopp kwamba pengine Manchester City na Liverpool zitatwaa kila moja taji mwaka huu, lakini kulikuwa na ukweli fulani kwenye utani ule nafikiri.

# *Vidal njoo Inter Milan - Zanetti*

**MILAN,** Italia

KUMSAJILI Arturo Vidal kutoka Barcelona kunaweza kuipaisha Inter Milan kwenye daraja la juu, kwa mujibu wa Makamu Rais wa klabu hiyo, Javier Zanetti.

Vidal mchezaji wa kimataifa wa Chile, amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua kwa 'Nerazzurri' hao Januari hii na alishindwa kukanusha kuhusu hilo alipoulizwa wiki iliyopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ameanza katika mechi sita tu katika mashindano yote msimu huu kwa Barca, ingawa amefunga mabao matano kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Inter imeripotiwa kwamba inatumaini kumsajili kwa mkopo huku kukiwa na kipengele cha kumnunua kiungo huyo mzoefu na Zanetti anahisi ujio wake utakisaidia kikosi hicho.


"Tutaona namna usajili utakavyokwenda, kwani tuna mwezi mzima wa kukamilisha kila kitu," alisema akiiambia ESPN.

"Vidal ni mchezaji wa daraja la juu na mwenye uzoefu, hivyo tutaona kitakachotokea. Tunafikiria kuhusu wachezaji ambao pengine watatunyanyua katika daraja jingine, na tayari tupo kwenye daraja zuri."

Inter inaongoza msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwa tofauti ya bao moja dhidi ya Juventus na itacheza na Napoli Jumatatu Ijayo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RAIOLA AMUWEKA POGBA MGUU NDANI NJE UNITED

## Anapaswa kuwa katika klabu inayopigania ubingwa wa ligi na ninatumai Ligi ya Mabingwa...

**MANCHESTER,** England

WAKALA wa Paul Pogba, Mino Raiola amesema "moyo" wa kiungo huyo upo Manchester United, lakini akaongeza kuwa anahitaji kuichezea timu yenye uwezo wa kushinda mataji.

**Pogba, ambaye alirudi United akitokea Juventus mwaka 2016, mapema Juni alikiri kuwa angependa kuondoka Old Trafford kwenda kutafuta "changamoto mpya", wakati Raiola mwezi mmoja baadaye aliongeza kuwa yupo katika mchakato wa kumtafutia mteja wake klabu mpya.**

Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amebaki United na Ole Gunnar Solskjaer, mwezi uliopita alisema Pogba hatauzwa katika dirisha la usajili la Januari.

Alipoulizwa kama yeye na Pogba walikuwa ni wenye furaha na hali hiyo, Raiola katika mahojiano maalum na Sky Sports News, alisema: "Paul mara zote anaiheshimu Manchester United, kama ambavyo Manchester United inavyomheshimu Paul.

"Mtu pekee anayezungumza kwa Manchester United na Paul ni Ole. Ninafuata kwa kile anachosema; hataondoka. Hilo sawa na tunakwenda nao.

"Paul anasumbuliwa kidogo na jeraha na ndiyo shauku yetu kuu sasa. Kuna lengo moja ambalo Paul analo na hilo ni kuonyesha kiwango kadri iwezekanavyo na Manchester United.

"Yeye ni mchezaji wa kulipwa wa kiwango cha juu na nadhani kwamba moyo wake uko mahala sahihi na Manchester United. "

Hata hivyo, Raiola ambaye ni wakala wa wachezaji kama Zlatan Ibrahimovic, Matthijs de Ligt na Erling Haaland - ameonya mustakabali wa baadaye wa Pogba unaweza kuwa na maswali kama United itaendelea kupata wakati mgumu wa kushindana na timu kubwa Ulaya.

Alipoulizwa kuhusu endapo bado anaweza kumuona Pogba akiwapo United kwa muda wa mwaka mmoja, Raiola alisema: "Ndiyo ninaweza kuona, lakini katika klabu ambayo inapigania ligi na ninatumai Ligi ya Mabingwa.

"Je hiyo ni ya kushangaza? Mimi ni pekee ambaye nina hofu? Ni mmiliki ni siye hofu? Nadhani kuwa yupo katika upendo na Manchester United ana hofu kuhusu hilo.

"Nina hofu kuhusu hilo kwa mchezaji wangu. Mimi si shabiki wa Manchester United lakini nina shauku ya moja kwa moja.

"Muda huu Paul yupo Manchester United, anataka kushinda mataji na Manchester United. Ndio aina ya mchezaji alivyo na hataigiza tofauti.

"Kama Ole alivyosema, ni kazi inayoendelea sasa katika klabu hii. Anasema anafanyia kazi timu ya mwaka ujao. Wacha tutegemee kuwa inaendelea vizuri kwake kwa sababu dunia inaihitaji Manchester United kuwa juu. "Ni wazi si mahali wanapofikiria wanapaswa kuwa."

Raiola pia alifunguka kuwa hajawahi kuzungumza na Solskjaer, akielezea: "Ikiwa Ole ana maoni juu ya mchezaji wangu na anataka kuzungumza na mimi juu yake, anajua namba yangu."

## ZISIKUPITE

### CHELSEA YAMFUATILIA WERNER

CHELSEA inachunguza undani wa tetesi za kipengele kinachomruhusu mshambuliaji wa RB Leipzig, Timo Werner kuununua mkataba wake. Straika huyo mwenye umri wa miaka 23, amefunga mabao 23 katika mechi 24 alizoichezea klabu yake msimu huu. ***(Telegraph)***

### AUBAMEYANG AMTESA ARTETA

MIKEL Arteta anakabiliwa na suala gumu la kumshawishi mshambuliaji Mgabon Pierre-Emerick Aubameyang, 30, kubaki klabuni hapo mwishoni mwa msimu. ***(Telegraph)***

### KLOPP KUMPOTEZA LALLANA

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amenyoosha mikono juu kuhusu kumpoteza kiungo wa England, Adam Lallana, 31, mwishoni mwa msimu. ***(Telegraph)***

### HENRY ANUKIA BARCELONA

THIERRY Henry atakuwa mshindani wa kuwa kocha wa Barcelona kama kocha wa sasa, Ernesto Valverde ataondoka klabuni hapo mwaka 2020. ***(Sport - in Spanish)***

### FERNANDES WA JANUARI UTD

MANCHESTER United pia inazingatia uwezekano wa kwenda kumsajili kiundo wa Ureno na Benfica, Gedson Fernandes, 20, katika dirisha la Januari. (Sky Sports)

### KUMVUTA UPAMECANO

ARSENAL inaweza kumfuata beki wa kati wa RB Leipzig, Dayot Upamecano, 21, baada ya kocha mpya wa 'Gunners', Mikel Arteta kuweka kipaumbele cha kuimarisha safu ya ulinzi. ***(Mirror)***

### ABRAHAM AITESA CHELSEA

MAZUNGUMZO ya mkataba mpya wa mshambuliaji wa kimataifa wa England, Tammy Abraham na Chelsea yamesimama kwa sababu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, anataka kulipwa mshahara kiasi cha pauni 180,000 kwa wiki sawa na anavyolipwa winga, Callum Hudson-Odoi, 19. ***(Goal)***

### CARLOS KUMSAIDIA VAN DIJK

LIVERPOOL ipo katika mazungumzo na beki wa Sevilla, Diego Carlos, 26, ambaye anakipengele kinachomruhusu kuvunja mkataba wake kwa pauni milioni 65 na inamtazama kama 'pacha' wa muda mrefu wa Virgil van Dijk. ***(Eldesmarque via Mirror)***

### MADRID KUMREJESHA VALLEJO

REAL Madrid itamuita kwa mara nyingine beki Mhispania Jesus Vallejo, 22, kutoka Wolves anapocheza kwa mkopo katika usajili huu wa dirisha la Januari kwa sababu ya kukosa muda wa kutosha uwanjani. ***(AS - in Spanish)***

### EVERTON KWA RODRIGUEZ

EVERTON inaongoza mbio za kumsajili winga Mcolombia James Rodriguez, 28, kutoka Real Madrid. ***(El Desmarque - in Spanish)***

### ROJO KUTIMKA OLD TRAFFORD

BEKI wa Argentina, Marcos Rojo, 29, anajiandaa kuondoka Manchester United katika dirisha la usajili la Januari. ***(Manchester Evening News)***

HABARI MICHEZO

MBIO...




Baadhi ya timu za mbio za mitumbwi zikijiandaa kuanza mashindano hayo juzi kwenye Ufukwe wa Ziwa Victoria, katika Kijiji cha Bukima mkoani Mara, ambayo yalishirikisha timu kutoka kata 11. **NA MPIGAPICHA WETU**

# 10 kutifuana soka la ufukweni Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

JUMLA ya timu 10 za Soka la Ufukweni (Beach soccer) zinatarajia kucheza michuano ya Mapinduzi Cup kwa upande wa soka hilo hapa visiwani Zanzibar, inayotarajiwa kuanza Januari 5, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili Mwenyekiti wa Kamati ya Soka la Ufukweni, Abubakar Mohmed, alisema michuano hiyo inatarajiwa kuchezwa katika Fukwe ya Bambuu iliyopo Bububu Mkoa wa Mjini Magharibi hapa Kisiwani Unguja.

Alisema tayari maandalizi yote kwa hatua ya awali yamekamilika ikiwamo fukwe ya kuchezea michuano ambayo kamati ilitembelea na imeridhika na mazingira halisi.

Akizitaja timu zitakazoshiriki michuano hiyo kuwa ni Green Rivers, Malindi, Young Boys, Zanzibar Swimming, Blue Sea, Dikoni, Manchester, Beach Boys, La Vister na Gold Swimming.

Alisema michuano hiyo ambayo kwa hatua ya awali itaanza kwa mtoano hadi pale zitakapobakia timu tano ndio zitacheza mtindo wa ligi, bingwa atapatiwa zawadi ambayo hata hivyo hakuitaja.

# MKWASA: HAIKUWA RAHISI KUFURUKUTA KWA BIASHARA



**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kupata ushindi wa mbinde dhidi ya Biashara United juzi, Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa (pichani), amekiri kwamba haikuwa kazi rahisi kwao kupata matokeo mbele ya 'Wafanyabiashara' hao kutoka mkoani Mara, huku akiwamwagia sifa vijana wake kwa kupambana hadi mwisho wa mchezo.

**Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Taifa juzi, Yanga ililazimika kusubiri hadi dakika ya 84 kuweza kupata bao pekee lililowapa ushindi wa 1-0 kupitia kwa mtokea benchi aliyesajiwa katika dirisha hili dogo, Tariq Seif.**

Ushindi huo, ukaifanya Yanga kukwea hadi nafasi ya pili huku ikiishusha Kagera Sugar hadi nafasi ya tatu, lakini timu hizo kila moja ikiwa na alama 24, hivyo kutofautiana kwa mabao ya kufunga na kufungwa tu.

"Kila timu inapocheza na Yanga huwa inapambana sana jambo linaloongeza ugumu kwetu, hivyo tulikutana na upinzani mkubwa lakini tulipambana hadi mwisho.

"Kwa ujumla nawapongeza wachezaji na mashabiki kwani huu ni mwendelezo mzuri na tutaendelea kupambana kupata matokeo chanya, hivyo sasa tunaelekea kujiandaa na mchezo ujao," alisema kocha huyo wa zamani Taifa Stars na Twiga Stars.

Yanga itashuka tena dimbani Jumamosi, ikiwa na matumaini ya kuendeleza ushindi wao huo itakapokutana na watani zao, Simba kwenye mechi itakayopigwa uwanja huo wa Taifa.

# *KMC yawatoa hofu mashabiki Ligi Kuu*

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kushuka dimbani mara 13 na kuambulia alama tisa tu, huku ikiwa katika nafasi ya 17 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, Mwenyekiti wa Bodi ya KMC FC, Benjamin Sitta (pichani), amewatoa hofu mashabiki wa timu hiyo na kuwataka kuamini timu hiyo itarejesha makali yao ya msimu uliopita.

Akizungumza na mwandishi wetu kuhusu mwenendo wa timu hiyo kwenye Ligi Kuu, ambayo msimu huu zitashuhudiwa timu nne zikishuka daraja, alisema ana imani KMC itarejea mchezo na kufanya vizuri katika ligi hiyo.

Alisema lengo lao ni kumaliza nafasi tano za juu na hilo linawezekana kwa kuwa timu hiyo inacheza vizuri ikiwa ni pamoja na kumiliki mpira kwa asilimia kubwa, jambo ambalo anaamini muda si mrefu wataanza kupata ushindi.

"Lengo letu ni kumaliza nafasi tano za juu, unajua ukiwa na imani unaweza hata kuhamisha milima kama ambavyo maandika yanavyosema, timu itabadilika na kuanza kushinda," alisema.



Kuhusu kuboresha kikosi hicho wakati huu dirisha dogo la usajili likiwa wazi hadi Januari 15, mwaka huu, Sitta alisema hawaoni sababu ya kukusanya wachezaji katika klabu hiyo kwa kuwa waliopo bado wanacheza vizuri.

Msimu uliopita, KMC FC ilimaliza nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa nyuma ya mabingwa watetezi, Simba walioimaliza kileleni wakifuatiwa na Yanga na Azam FC.

Michezo
Jumatano Januari 1, 2020
Nipashe



Raiola amuweka Pogba mguu ndani nje Utd HABARI UK.30

KARIBU 2020...



Francis Kahata (Jezi Na. 25), akishangilia na wachezaji wenzake wa Simba, baada ya kuifungia timu hiyo bao la kuongoza dhidi ya Ndanda FC, wakati wakishinda 2-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba yaingia 2020 na salamu za Yanga

## Kahata na Kanda waigeuza Ndanda daraja la kupeleka ujumbe Jumamosi huku...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara wameukaribisha mwaka 2020 kwa kutuma salama za ushindi kwa watani zao, Yanga baada ya kuichapa Ndanda FC kwa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana.

**Mabao mawili ya wachezaji wa kigeni, Mkenya Francis Kahata na Mkongomani Deo Kanda ndiyo yaliyopeleka salamu hizo Jangwani huku yakiifanya timu ya Simba kuongeza pengo la pointi 10 kati yake na Yanga, baada ya kuichapa Ndanda FC 2-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.**

Ushindi huo unakuja siku chache kabla ya mechi ya mahasimu wao wa jadi, Yanga Jumamosi ambayo nayo juzi ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Biashara United.

Faulo ya dakika ya 13 iliyopigwa na Kahata kutokana na Sharaf Shiboub kufanyiwa madhambi ndani ya eneo la hatari ilikwenda moja kwa moja wavuni na kuiandikia Simba bao la kuongoza.

Dakika tano kabla ya pambano kumalizika, Kanda aliandika bao la pili baada ya kuugusa mpira wa krosi uliopigwa na Gadiel Michael, ukapoteza uelekeo na kumchanganya kipa Ally Mustapha 'Barthez', kabla ya kujaa wavuni.

Hilo linakuwa ni bao la tatu kwa Kanda aliyesajiliwa msimu huu kutoka TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa mkopo, aliyeingia kuchukua nafasi ya mfungaji wa bao la kwanza, Kahata.

Kipindi cha kwanza Simba ilitawala mpira kwa kipindi chote, ikicheza pasi fupi na soka la taratibu, huku wachezaji wengi wa Ndanda wakiwa nyuma kwa kuzuia mashambulizi.

Straika aliyekuwa anacheza mechi ya kwanza ya Ligi Kuu tangu msimu huu uanze, John Bocco nusura afunge bao dakika ya nane, baada ya kupigwa kichwa mpira wa krosi ya Shiboub, lakini ukatoka juu ya goli.

Said Ndemla akiwa nje ya eneo la hatari aliachia kombora kali, lililopanguliwa na kipa Barthez, huku kipa huyo pia akiokoa mpira wa hatari uliokuwa umepigwa kichwa na Bocco, dakika chache kabla ya mapumziko.

Kipindi cha pili Ndanda ilibadilika na kuibana Simba kwa muda mrefu, lakini mabadiliko ya kuingia kwa Kanda, Mzamiru Yassin aliyeingia badala ya Jonas Mkude na Claotus Chama badala ya Ibrahim Ajibu, yaliirudisha timu hiyo mchezoni na kufanya mashambulizi mfululizo dakika za mwisho.

Shambulio pekee kali kwa Ndanda ilikuwa ni mpira wa faulo dakika ya 75 iliyopigwa na Kigi Makasi, lakini ulidakwa na Aishi Manula.

Kwa matokeo hayo Simba sasa inafikisha pointi 34, ikiongoza ligi, ikifuatiwa na Yanga yenye pointi 24, lakini Simba ikicheza mechi 13, watani zao wakiwa wameshuka dimbani mara 11 msimu huu.

Simba na Yanga sasa zinaingia msituni kujiwinda mechi yao ya watani wa jadi itakayopigwa Uwanja wa Taifa Jumamosi.

# Molinga atimka kwa bodaboda

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa Yanga, David Molinga, amewashangaza mashabiki wa timu hiyo na wadau wa soka baada ya kufanyiwa mabadiliko ['sab'] wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Biashara United kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi.

Katika mechi hiyo, Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, alimtoa Molinga (pichani chini) dakika ya 46 na kumuingiza Tariq Seif aliyesajiliwa katika dirisha hili dogo, mabadiliko ambayo yalizaa matunda, lakini yalionekana kutopokelewa vema na straika huyo kutoka DR Congo.

Tariq aliifungia Yanga bao pekee katika dakika ya 84 ikiwa ni baada ya kupata nafasi mbili na kukosa kabla ya nafasi hiyo ya tatu kucheka na nyavu, hivyo kudhihirisha kuwa Mkwasa hakukosea kufanya mabadiliko hayo kwa kumtoa Molinga ambaye alikosa nafasi nyingi awali.

Hata hivyo, baada ya Molinga kutolewa alitoka moja kwa moja na kuelekea lango kuu ambapo alitoka nje na kuita dereva bobadoda kisha kuondoka zake.

Lakini akizungumzia tukio hilo, Ofisa Mhamasishaji na Msemaji wa Yanga, Antonio Nugaz, alisema kuwa Molinga anapenda kuisaidia timu wakati wote na kitendo cha kutolewa kilionekana kumkera kwa kuwa bado alihitaji kuipigania timu.

Hata hivyo, Nugaz alikana Molinga kuondoka kwa bodaboda na kudai kwamba alirejea na kuondoka na basi pamoja na wachezaji wenzake.

"Nilikuwapo kwenye basi wakati wachezaji wakiingia na yeye alipanda na kuondoka na wachezaji wenzake," alidai Nugaz kauli ambayo ilizua gumzo kubwa jana kwenye vyombo vya habari ikiwamo mitandao ya kijamii.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >